**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Tano – Tarehe 20 Juni, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**KIAPO CHA UAMINIFU**

Mjumbe aliyetajwa chini aliapa Kiapo cha Uaminifu na kukaa katika nafasi yake ndani ya Ukumbi wa Bunge.

Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):-**

Nakala za Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha Mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:-**

Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Elimu Tanzania kwa Mwaka 2004 na 2005. (*The Annual Report of the Tanzania Education Authority for the year 2004 and 2005).*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 39

**Sura za Waasisi Wetu kwenye Fedha**

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwepo na pendekezo la kuwaenzi Viongozi na Waasisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Abeid Amani Karume kwa kuweka sura zao katika noti za fedha za Tanzania, lakini hadi hivi sasa ni sura ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere tu ndiyo inayoonekana katika noti ya Sh.1,000/= ya Tanzania:-

(a) Je, uamuzi wa kuweka sura za Waasisi wetu hao katika noti ni jukumu la nani?

(b) Je, kuna tatizo gani linalofanya sura ya Muasisi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Hayati Abeid Amani Karume isiwekwe katika noti mojawapo kama ilivyokuwa kwa Muasisi Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere?

(c) Je, kama kuna tatizo Serikali ina mpango gani wa kulishughulikia suala hilo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mbunge wa Mbuyuni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Jukumu la kuweka alama za usalama (*Security Features*), sura za Waasisi wetu, pamoja na vitu vingine ndani ya noti na sarafu za Tanzania, ni la Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania baada ya kupata kibali cha Waziri wa Fedha kama ilivyoainishwa katika kifungu Namba 30(b) cha Sheria ya Kuanzisha Banki Kuu ya Tanzania (*Bank of Tanzania Act, 1995*).

(b)Hakuna tatizo linalofanya sura ya Muasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar Mheshimiwa Abeid Amani Karume, asiwekwe katika noti mojawapo. Utaratibu uliokuwepo kuanzia mwaka 1965 hadi 1995 ni kwamba, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania ilikuwa ikiweka katika noti na sarafu sura ya Rais aliyekuwa madarakani wakati ule. Kwa hiyo, kwa muda wa miaka thelathini noti na sarafu zilikuwa kwanza na sura ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na baadaye zilikuwa na sura ya Rais Mstaafu Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi. Baada ya mwaka 1995, Mheshimiwa Rais Mstaafu Benjamin William Mkapa hakutaka sura yake iwekwe kwenye noti na sarafu za nchi yetu. Hivyo noti zilizochapishwa na sarafu zilizotengenezwa baada ya uamuzi huo hazina sura ya Rais aliye bado madarakani, isipokuwa tu noti ya shilingi elfu moja ina sura ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Baba wa Taifa.

(c) Kwa kuwa hakuna tatizo, Serikali itaiagiza Benki Kuu kuchapisha noti yenye sura ya Muasisi Mheshimiwa Abeid Amani Karume.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Pamoja na majibu hayo nina maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, ni kwamba ikiwa kama nia ya Serikali ni kuwaenzi viongozi wetu hao waasisi. Lakini sasa hivi kuna tabia ya baadhi ya wananchi kama wauza samaki magengeni au wachoma mahindi unapompatia noti ya Tanzania hata ikiwa mpya namna gani ataipikicha na kuinyonga nyonga ionekane kwamba imezeeka kama ya miaka 6. Je, Serikali inasema nini kuhusu suala hili?

La pili, bahati nzuri mimi ni Mswahili wa kuzaliwa si Mswahili wa Kamusi. Ni kwamba kuna sarafu ambayo ni sarafu ya shilingi mia hasa na sarafu ya shilingi 50 ambayo kwa bahati hizi zina sura za viongozi wetu. Lakini sarafu hizi imefikia hatua kwamba wananchi wengine wanazikataa kwa jinsi zilivyochakaa. Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuzifanya sarafu hizi zikaonekana kwamba ni sarafu zinazoenzi kuliko jinsi zilivyokaa kwamba hauitambui hii ni sura ya hayati mwalimu Julius Kambarage Nyerere au hii ni sura ya hayati Abeid Amani Karume au hii ni sura ya mstaafu Mheshimiwa Ali Hassani Mwinyi? Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, kwa kweli hilo ni kosa kuvuruga noti na pale popote ambapo atashikwa mtu anakosa na anaweza kushitakiwa na kupelekwa Mahakamani. Kwa hiyo, hilo ni la kushirikiana kati yetu wananchi na unapowakuta watu kama hao ni vizuri ukaliripoti haraka.

Kuhusu sarafu ya shilingi 100 na 50 zilizochakaa kama tulivyokuwa tunajibu katika maswali ya siku za nyuma ni kwamba hizi sarafu zote zikiwa na hali hiyo benki wanatakiwa washike na wazirejeshe Benki Kuu ili *circulation* ya sarafu nyingine iweze kutolewa ili wananchi waweze kuzitumia.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba niulize swali moja la nyongeza. Ili kuweka alama katika noti ni utaratibu au ni utashi wa mtu. Kama ni utaratibu kwa nini Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa aliyetangulia alikataa wakati ni utaratibu umewekwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la msingi kwamba sheria ya mwaka 1965 inaruhusu kwamba kwenye noti ziwekwe picha za viongozi wetu. Lakini vilevile viongozi wana hiari ya kusema kwamba picha yangu isiwekwe kwenye noti.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Baada ya maelezo mazuri na ya ufasaha ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kulieleza Bunge hili pale Rais alipochapishwa sura yake katika noti kuna malipo yoyote Rais analipwa na ni kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais halipwi. *(Makofi)*

Na. 40

**Tatizo la Ajira ya Watoto Nchini**

**MHE. DORAH H. MUSHI** aliuliza:-

Kwa kuwa, idadi kubwa ya Watanzania ni watoto chini ya umri wa miaka 18, na wengi wao wako katika shule za msingi, sekondari na wengine wako katika mazingira magumu na wengine wameajiriwa; ingawa Serikali imeanzisha Mpango wa Elimu ya Msingi kwa waliokosa MEMKWA, mafunzo ya ufundi stadi *(VETA)* lakini bado tatizo linazidi kuongezeka siku hadi siku:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dorah Mushi, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kupambana na tatizo la ajira ya watoto kwa lengo la kulipunguza na hatimaye kutokomeza kabisa. Hatua hizo ni pamoja na kuridhia Mkataba wa Shirika la Kazi Duniani Na. 182 wa mwaka 2001 unaohusu kutokomeza utumikishwaji wa watoto katika kazi za hatari.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Bunge lako Tukufu ilipitisha Sheria ya Ajira na Mahusiano ya Kazi Na.6 ya mwaka 2004 ambayo inakataza kuwaajiri watoto katika kazi za hatari kama vile machimboni, viwandani na kwenye mashamba makubwa ya mazao ya biashara. Aidha, kanuni za Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 zimerekebishwa ili kuhakikisha watoto wote wanaanza na kubaki shuleni na hatimaye kuhitimu vizuri. Kanuni hizi mpya zinawadhibiti wazazi kuhakikisha kuwa watoto wote wanaenda shuleni badala ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, mpango huu wa awamu ya kwanza uliotekelezwa kama mpango wa majaribio katika Wilaya 11 ambazo ni Arumeru, Arusha, Ilala, Iramba, Iringa, Kinondoni, Kondoa, Mufindi, Simanjiro na Temeke na Urambo. Kwa msaada

wa Shirika la Kazi Duniani *(ILO)*, katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mpango huu, Serikali imeweza kuwatoa watoto 15,429 kati ya watoto 57,531 katika Wilaya hizo 11 ambao waliokuwa katika utumikishwaji wa kazi za hatari. Aidha, watoto 19,060 waliokuwa katika hatari zaidi walizuiwa (*prevented*) kuingia katika ajira. Awamu ya pili inaendelea kutekelezwa katika kipindi cha mwaka 2006 hadi 2008 ambapo Wilaya 5 zitaongezeka. Wilaya hizo ni Kilwa, Lindi, Mwanza, Micheweni (Pemba) na Kaskazini Unguja.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana zinaendelea na jitihada za kupunguza tatizo la ajira kwa watoto. Lengo ni kuhakikisha kuwa watoto wanaotumikishwa wanaondolewa na kuzuiwa kujiingiza katika ajira hizo ili kuziwezesha familia ziweze kujiongezea kipato na vilevile kuhakikisha kuwa watoto wanapata elimu ikiwa kama moja ya haki zao za msingi.

**SPIKA:** Tunaendelea, swali linalofuata.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimekumbusha mara kwa mara kwamba anayeuliza swali la nyongeza asiache muda ukapita kiasi cha kumpa shida Spika. Kwa sababu tunakwenda na wakati ni lazima kujiandaa vizuri. Kwa hiyo, naruhusu kwa sasa, lakini nadhani itaendelea kuwa vigumu kuruhusu namna hiyo. Mheshimiwa Dorah Mushi, swali la nyongeza.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Pamoja na majibu hayo nauliza kwa nini Serikali ipende kuwasaidia watoto ambao tayari wamekwishaingia katika mazingira magumu?

La pili, ikiwa asilimia 30 ya watoto wote wanaomaliza elimu ya msingi ndiyo wanaopata nafasi ya kuingia katika elimu ya sekondari. Je, hii asilimia 70 inayobaki Serikali ina mbinu gani ya kuweza kuwasaidia watoto hao kabla hawajaingia katika mazingira magumu?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, Kwanza, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi Serikali katika mpango wake wa kuwatoa watoto katika ajira mbaya imekuwa na mikakati katika Wilaya zote 11. Najua katika Wilaya ya Simanjiro ambapo Mheshimiwa Mbunge anatoka mpango huu umekuwa ukitekelezwa.

Tunapenda kukupongeza kwa jitihada kubwa ulizofanya huko kuhakikisha kwamba vijana hao wanatoka katika ajira hizi mbaya wanawezeshwa kufanya shughuli mbalimbali kama vile za kutengeneza vito lapidali. Lakini vilevile watoto wa kike

wanawasaidia katika miradi ya saloni. Serikali itaunga mkono na kuhakikisha kwamba mnapewa uwezo na wale watoto wanabaki katika zile kazi ambao ni salama na siyo kwenda tena katika kazi zile tulizowatoa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, napenda kusema tu kwamba lengo la Serikali ni hatimaye kuhakikisha kwamba watoto wote wanakwenda katika shule za sekondari. Sasa hivi asilimia kama ulivyosema ni pungufu kama 30 wanaokwenda katika shule za sekondari.

Lakini kuna maeneo mbalimbali ambapo wanaweza kuchukuliwa watoto hao wanaomaliza darasa la saba ikiwa ni pamoja na Vyuo vyetu vya Maendeleo ya Jamii, ikiwa ni pamoja na *VETA.* Lakini hatimaye Serikali ina mpango wa kuhakikisha kwamba Watanzania wote wanapata elimu ya sekondari kama ilivyo elimu ya msingi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na swali linalofuata. Ninafurahi kuwatambulisha wageni wa Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mbunge wa Vunjo, ambao ni Madiwani 16 kutoka *Moshi District Council* wako kulia kwangu pale. Naomba wasimame. Hao ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Halmashauri ya Moshi. Karibuni sana.

Naomba Waheshimiwa Wabunge wale wanaokuwa na wageni ili tusiingilie kipindi cha maswali kwa sababu utaratibu ni kuwatambua wageni kabla ya kipindi cha maswali. Naomba taarifa ziwe zinakuja mapema tunapoingia tu ili tuweze kuwatambua wageni wetu kabla ya kuendelea na kipindi cha maswali si vizuri kukikatiza. Tunaendelea na swali linalofuata la Wizara ya Nishati na Madini. Mheshimiwa Beatrice Shellukindo endelea.

Na. 41

**Wananchi Kufaidika na Rasilimali ya Madini**

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Tanzania ina rasilimali nyingi ikiwemo, misitu na madini. Aidha, Serikali imelenga rasilimali hizo ziweze kuwanufaisha wananchi waishio katika maeneo yenye rasilimali hizo. Katika Wilaya ya Kilindi panapatikana madini ya aina mbalimbali yakiwemo madini ya dhahabu na vito. Kulingana na sheria hiyo ya madini, madini yote ni mali ya Serikali, hivyo kusababisha vibali vyote kutolewa na Wizara pamoja na kodi na malipo mengine kuwasilishwa Serikalini:-

(a) Je, katika Wilaya ya Kilindi ni leseni ngapi za *PLS* zilizotolewa na ni katika maeneo gani, na ni fedha kiasi gani zimepatikana na wananchi husika wamepatiwa kiasi gani?

(b) Je, Serikali inayo taarifa ya mkataba uliotolewa kwa niaba ya wachimbaji wadogo na kumilikishwa kwa wawekezaji wakubwa kutoka nje katika maeneo ya Mafulira na ambayo hao wachimbaji wadogo hawaruhusiwi kufika katika maeneo hayo?

(c) Je, wananchi hao wamepata faida gani hadi leo kwa eneo hilo walilopewa wawekezaji bila ridhaa yao na Serikali imepata fedha kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo, Mbunge wa Kilindi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Kilindi, kuna leseni za utafutaji mkubwa wa madini saba (7) pamoja na ombi moja la leseni. Kati ya leseni hizo *Prospecting Licence (PL)* ni tano (5) na *prospecting Licence with Reconnaissance Period (PLR)* ziko mbili (2). Mchanganuo wa leseni hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) PL 2385/2003 inayomilikiwa na Dar es Salaam *Depertamental Store Limited* ambayo ilitolewa tarehe 15/12/2003;

(ii) PL 3118/2005 inayomilikiwa na *Atlas Africa Limited* iliyotolewa tarehe 29/03/2005;

(iii) Leseni tatu *PLR 2282/2003*, *PL 2283/2003* na *PL2284/*2003 zinazomilikiwa na *Hari Singh and Sons Limited* zilizotolewa tarehe 18/07/2003;

(iv) *PL 3048/2005* inayomilikiwa na *Mafulira Village Mining Company Limited* iliyotolewa tarehe 10/02/2005; na

(v) *PLR 2683/2004* inayomilikiwa na *Hydro Geos Consulting Group Limited* iliyotolewa tarehe 14/09/2004; na

(vi) Maombi namba 3608 ya Kampuni ya *Majo One Company Limited* ambayo tayari ada ya maandalizi ya leseni imeshalipiwa na leseni iko mbioni kutolewa.

Mheshimiwa Spika, leseni hizo zote, isipokuwa *PL 3048/2005* ya *Mafulira Village Mining Company Limited*, ziko nje ya eneo lililotengwa na Wizara yangu kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Leseni hizo ziko Magharibi na Kaskazini mwa eneo la wachimbaji wadogo.

Katika kutoa leseni katika maeneo hayo, Serikali imekusanya jumla ya Dola za Marekani 24,003.09 zikiwa ni malipo kwa ajili ya ada ya maombi na maandalizi ya leseni. Vilevile, kuna ada ya mwaka na ya kuandikisha ubia.

Mheshimiwa Spika, fedha zote zinazokusanywa na Wizara yangu kutokana na shughuli za madini zinaingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali (HAZINA). Aidha, fedha hizi hutumiwa na Serikali kwa shughuli za maendeleo katika maeneo yote hapa nchini. Hivyo, ni vigumu kujua kiasi ambacho Serikali imekitoa kwa ajili ya shughuli za maendeleo katika Wilaya ya Kilindi kati ya fedha zilizokusanywa na Serikali kutokana na shughuli za madini Wilayani humo.

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ina taarifa na Mkataba kati ya Kampuni ya Mafulira *Mining Company Limited* inayomiliki leseni *PL 3048/2005* na kampuni ya nje ya *Ashanti Exploration Tanzania Limited* inayomilikiwa na Kampuni ya *Anglo Gold Ashanti Limited* uliotiwa sahihi tarehe 23/10/2005. Katika Mkutano wa Wakurugenzi wa Kampuni ya Mafulira *Village Mining Company Limited* wa tarehe 20/10/2004 walifikia maamuzi ya kufanya sihia (*transfer)* ya leseni hiyo kwenda kwa kampuni ya *Ashanti Exploration Tanzania Limited.* Sihia hiyo iliandikishwa kwenye rejesta na Kamishna wa Madini tarehe 03/3/2005 na baada ya hapo kampuni ya *Ashanti Exploration Tanzania Limited* iliingia ubia na Kampuni ya *Anglo Tanzania Gold Limited.* Vilevile, ubia huo uliandikishwa kwenye rejesta na Kamishna wa Madini tarehe 9/09/2005. Hivyo, kwa sasa Kampuni ya *Anglo Tanzania Gold Limited* ndiyo inayofanya shughuli za utafutaji wa madini katika leseni *PL3048/2005.*

Wachimbaji wadogo wanazuiwa kuingia na kuendesha shughuli za uchimbaji katika eneo linalofanyiwa utafiti na kampuni hiyo ili kuepuka muingiliano wa shughuli za utafutaji madini.

(b) Mheshimiwa Spika, wananchi wa maeneo yanayofanyiwa utafutaji wa madini Wilayani Kilindi wanafaidika na shughuli za utafutaji wa madini kwa kupata ajira na pia uuzaji wa mazao na bidhaa mbalimbali zinazopatikana katika eneo hilo.

Wawekezaji wanaofanya utafutaji wa madini katika eneo la kijiji cha Mafulira wameingia katika eneo hilo kwa ridhaa ya Wakurugenzi wa kampuni ya *Mafulira Village Mining Company Limited*, ambao ndio wawakilishi halisi wa kampuni hiyo.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo nina uhakika hata huko Kilindi kama wanasikiliza wameshtuka sana na kwa njia nyingine pengine tumepewa changamoto.

Sasa kwa sababu kutokana na majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri ni dhahiri kwamba kuna viongozi mamluki wanajiita Wakurugenzi ambao hawafahamiki hata kwa wananchi. Je, Serikali inatuambiaje sisi wananchi wa Kilindi kuhusu kuwachukulia hawa watu hatua kabla hatujachukua hatua sisi wenyewe?

La pili, pamoja na majibu yake ya msingi ni kweli kabisa pengine mkataba huo umeingiwa na hao viongozi mamluki walioko huko ambao tunawafahamu. Lakini nilikuwa ninasema kwa sababu madini ni rasilimali ya Taifa tuyaache hivi hivi na wananchi hawa wakiwa wamegubikwa na umaskini.

Je, Serikali itaingiliaje kati ili kuahakikisha kwamba hawa wananchi wanarudishiwa imani yao kwa Serikali yao na kuondokana na umasikini hasa ukizingatia Rais ameshasema tupitie mikataba upya?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi, mkataba huo ambao anauelezea sio mkataba ambao Serikali imeingia ni mkataba baina ya kampuni ya *Mafulila Village Mining Co. Ltd* na Kamapuni ya *Angro-Tanzania Gold Ltd.* Kwa habari tulizonazo Wizarani Mafulila *Village Mining Co. Ltd* ni Kampuni ya wananchi wa Kijiji cha Mafulila ambao waliiunda ili kuweza kuchimba katika eneo husika. Kama unavyosema mkataba huu, umeingiwa na Wakurugenzi wa Mafulila *Mining Co. Ltd* bila kufahamu kwa wananchi wa hilo eneo ambalo inasemekana kuwa-*represent*. Tunakushauri Mheshimiwa Shellukindo awasaidie wananchi wako kuchukua hatua dhidi ya hao Wakurugenzi ambao wameingia mkataba bila kuwahusisha wananchi hao.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Wilaya ya Kahama kwa mazingira yake inafanana sana na Wilaya ya Kilindi ambayo swali la msingi limeulizwa.

Nilikuwa na swali dogo la nyongeza kwamba kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba mapato yanayotoka kwenye madini yanaingizwa kwenye mfuko wa kitaifa na vilevile amesema Serikali haijui ni kiasi gani kinarudi kwenye eneo linalohusika kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya sehemu hiyo, na kwa kuwa utaratibu huu umekuwa ukilalamikiwa sana na wananchi wa maeneo hayo.

Je Serikali haioni kwamba ni muda muafaka umefika wa kuangalia utaratibu huu ili walau kiasi fulani kiwe kinapatikana kinarudi kwenye eneo hili ili kusaidia madhara yanayotokana na shughuli za madini kwenye maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi mapato ambayo yamepatikana kutokana na madini yanasambazwa katika nchi yote kwa ujumla, lakini kama anavyofahamu Mheshimiwa Maige Serikali ya awamu ya nne imeshughulika kuhakisha kwamba angalau zile kodi ambazo zinatakiwa kufika kwenye Halmashauri ambazo zina maeneo ya migodi tumehakikisha kwamba hizo kodi zimeanza kupatikana. Kodi ya dola 200,000 imeshalipwa kwenye Wilaya za Biharamulo, Tarime na Kahama katika siku tatu zilizopita.

Na. 42

**Mradi wa Kupeleka Umeme Kambi ya Nduguti**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati Serikali ilipotoa fedha za kujenga na kupeleka umeme Nkungi ilikuwa inafahamu kabisa kwamba hiyo ilikuwa sehemu ya mradi wa kupeleka umeme Iambi na Nduguti:-

(a) Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya kufikisha umeme Iambi na Nduguti?

(b) Je, ikizingatiwa kuwa sheria ya kwanza kutekeleza mradi na kupeleka umeme vijijini, Serikali ina mpango gani wa kusambaza umeme Iramba Mashariki maeneo ya Nkalankala, Mwanga, Kidarafa, Mwangaza, Mtongo, Msingi, Gumanga, Mkalama na Ibaga?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, napenda nitoe maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Umeme (*TANESCO*) liligharamia mradi wa kupeleka umeme hadi Hospitali ya Nkungi kwa gharama ya shiingi milioni 432. Mradi huu ulihusu ujenzi wa laini ya 33 *KV* yenye urefu wa kilometa 26 na haukuhusisha upelekaji wa umeme Iambi na Nduguti.

Baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umeme (*TANESCO*), imepanga kufikisha umeme hadi kijiji cha Ibaga kwa kupitia Iambi, Nduguti na Mkalama ikiwa ni umbali wa kilomita 57 kwa gharama ya shilingi milioni 827. Ili kufikisha umeme katika vijiji hivyo, Serikali na *TANESCO* inaendelea kuwasiliana na Benki ya Dunia kuhusu kufadhili mradi unaoitwa *Energizing Rural Transformation* ambapo maeneo tajwa yamejumuishwa katika mpango wa mradi huu wa kuyapatia umeme maeneo mbalimbali hapa nchini.

Kuidhinishwa kwa fedha na Benki ya Dunia kunategemea makubaliano na utekelezaji wa masharti ya Benki hiyo. Mojawapo ya masharti ni kuhakikisha *TANESCO* inakuwa na hali nzuri kifedha na pia iwe na uwezo wa kulipa madeni yatakayotokana na mikopo itakayotolewa.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kusambaza umeme kwenye maeneo tajwa ya Jimbo la Iramba Mashariki kunahitajika jumla ya shilingi milioni 1,560. Serikali inaendelea na majadiliano na Benki ya Dunia kuhusu upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa mpango

wa *Energizing Rural Transformations (ERT)* kama nilivyoeleza kwenye jibu la sehemu (a) hapo awali. Benki ya Dunia bado haijaidhinisha fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huo. Aidha, maeneo yanayohusika kwenye mradi huo ni Iambi, Nduguti, Gumanga, Mkalama na Ibaga.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza kwa kuwa Serikali na Benki ya Dunia wanajiandaa kwa hiyo. Je, vile vijiji vingine ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri hakuvitaja yaani Nkalankala, Mwanga. Kidarafa na Mwangeza, awamu itakayokuja na vyenyewe vitaunganishwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, hivyo vijiji tutaviangalia na kuangalia uwezekano wa kuviingiza katika *ERT Phase One* au *ERTA Phase Two.*

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa umeme huu unaokwenda Iramba Mashariki unaanzia Singida, na kwa kuwa mwaka 2004 Serikali iliahidi kwamba umeme unaotokea Singida chini ya ule mradi ungepelekwa katika shule ya wasichana ya sekondari inayoitwa *Muli Girls Secondary School* iliyoko katika Kata ya Mahojoa katika Jimbo la Singida Kaskazini. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri anihakikishie tu kwmba umeme huo chini ya huo mradi utapita Kinyeto Mahojoa na kuhakikisha kwamba zile sekondari mbili zinapata umeme kwa sababu hii nchi ni moja?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, hayo majina ya hivyo vijiji tumevipokea na ningemwomba Mheshimiwa Nyalandu aje Ofisini tukae tuangalie namna ya kuhakikisha kwamba hivyo vijiji vinaingizwa kwenye mpango wa *ERT*.

Na. 43

**Kuzuiwa kwa Bidhaa zisizo na Viwango**

**MHE. USSI AMME PANDU** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inafanya jitihada za kuzuia kuingia/kuingizwa kwa vitu visivyo na ubora wa viwango nchini kupitia *TBS*:-

(a) Je, ni wafanyabiashara wangapi wamekamatwa kwa kipindi cha mwaka 2006?

(b) Je, ni hatua gani za kisheria zilizochukuliwa kwa wafanyabiashara hao?

(c) Kwa kuwa, pamoja na juhudi hizo za Wizara bado kuna vitu madukani visivyo na ubora wa viwango Je, Serikali haioni kuwa ni tatizo kwa watumiaji?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Amme Pandu, ningependa kutoa maelezo yafuatayo:-

Katika kudhibiti ubora wa bidhaa zinazotoka nje ya nchi, Serikali ilitoa Tangazo Na. 672 la tarehe 25 Desemba 1998 chini ya Sheria Na. 3 ya mwaka 1975 iliyoanzisha Shirika la Viwango Tanzania, *TBS.*

Tangazo hili linalojulikana kama *Compulsory Batch Certification of Imports Regulations, 1998* linaweka sheria ndogo za kusimamia ubora wa bidhaa zinazotoka nje ya nchi. Tangazo hili pia linaipa *TBS* madaraka ya kusimamia utekelezaji wa sheria hiyo kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Serikali ikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) na Mamlaka ya Chakula na Dawa (*TFDA*) Katika utekelezaji huo Shirika la Viwango huchukua sampuli katika bandari ya Dar es Salaam na vituo vingine katika mpaka yetu kwa lengo la kupima ubora wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Amme Pandu, Mbunge wa Mtoni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Katika mwaka 2006 jumla ya shehena mbili (2) zilizuiwa kuingia katika soko la Tanzania shehena hizo ni:-

Kontena moja la viberiti kutoka India lenye thamani ya dola za Marekani 12,000. Shehena hii ilizuiwa katika kituo cha Mtukula, Mkoani Kagera ambayo ilikuwa iingie nchini kupitia Uganda. Vilevile aina sita ya vyakula zilikamatwa aina nne zilikamatwa na aina mbili za vipodozi zilikamatwa Bidhaa nyingine ni Katoni 1,034 za *Oil* ya injini za dizeli kutoka nchi za Falme za Kiarabu kupitia Zanzibar. *Oil* hii ilikuwa na thamani ya shilingi 22,256,520. Katoni hizi zilizuiwa katika bandari ya Dar es Salaam (majahazini) zikitokea Zanzibar.

(b)Hatua zilizochukuliwa dhidi ya wafanyabiashara hao ni kwamba bidhaa zao zote zilizuiliwa kuingia nchini na wakawajibika kuzirudisha zilikotoka lakini kwa upande wa chakula bidha hizo ziliharibiwa.

(c) Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba baadhi ya bidhaa madukani zisizo na ubora wa viwango ni tatizo kwa watumiaji. Hata hivyo kwa kawaida bidhaa hafifu huingizwa kwa njia za panya. Aidha, Serikali kupitia *TRA* imeweza kukamata baadhi ya shehena hizo na kupeleka sampuli *TBS* ili kuchunguza ubora wa bidhaa husika kabla ya waingizaji kulipa kodi zinazohusika pamoja na faini. Kwa zile bidhaa ambazo hupenya na kufika kwenye soko kupitia njia za panya, tunaomba wananchi watoe taarifa, *TRA*, *TBS TFDA* na Polisi ili bidhaa hizo zifanyiwe ukaguzi wa ubora.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali hili la kuuliza. Kimsingi hata hizi bidhaa ambazo zimepita kihalali katika bandari zinaweza zikawa hazifai kwa matumizi ya binadamu baada ya kukaa kwa muda mwingi madukani. Je, Serikali ina chombo gani cha kufuatilia mambo haya kwa sababu nchi za wenzetu unakuta kuna watu hasa wanafuatilia hizi bidhaa zimepitwa na wakati wanaziharibu, hapa kwetu naona kitu hicho hatukioni sana. Hivi Serikali ina chombo gani cha kufuatilia masuala hayo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwa bidhaa ambazo ziko madukani tayari kuna ukaguzi wa aina mbili. Ya kwanza ni *surveillance inspection* yaani wanafanya ukaguzi wa ghafla ambapo mwenye duka au mwenye stoo haarifiwi siku ya ukaguzi. Lakini pili wanafanya *marketing surveillance TBS* pamoja na *TFDA* wananunua zile bidhaa halafu wenakwenda kuzifanyia ukaguzi. Wanapogundua kwamba zimepitwa na wakati ama hazina ubora kutumiwa na wananchi wa Tanzania basi nidhaa hizo zinaharibiwa.

*(Hapa Kulitokea tatizo la kiufundi)*

Na.44

**Matumizi ya Dawa za Kichina nchini**

**MHE. DR. ALI TARAB ALI** aliuliza:-

Kwa kuwa dawa za binadamu kutoka China zimezagaa kila sehemu nchini, zikiwa na maelezo kwa lugha hiyo ya Kichina ambayo haifahamiki nchini na kwa kuwa inasemekana kuwa dawa hizo hazijahakikiwa:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa afya za wananchi zinahatarishwa kwa kiwango kikubwa?

(b) Je, Serikali ina mipango gani ya kuzihakiki dawa hizo?

(c) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwaagiza waagizaji na hasa viwanda vinavyotengeneza dawa hizo kuandika maelezo ya matumizi yake kwa lugha zinazoeleweka kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dk. Ali Tarab Ali, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na wauzaji wa dawa za binadamu za miti shamba *(herbal drugs)* kutoka China katika soko la dawa nchini zisizokidhi matakwa ya kisheria ambazo zinaweza kuhatarisha afya za wananchi. Tatizo

hili limechangiwa kwa kiasi kikubwa na uingizaji, usambazaji na uuzaji kiholela wa dawa hizo unaofanywa na wafanya biashara wasio waaminifu.

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inatambua athari zinazoweza kutokea kutokana na matumizi ya dawa hizo na katika kukabiliana na matatizo kama hayo, Serikali kupitia Bunge lako Tukufu ilipitisha Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Na. 1 ya mwaka 2003. Sheria hiyo ilipelekea kuundwa kwa Mamlaka ya Chakula na Dawa (*TFDA*) ambayo moja ya majukumu yake ni udhibiti wa dawa za miti shamba.

(b)Mheshimiwa Spika, mojawapo ya hatua za awali zilizofanywa na Serikali katika kuhakiki ubora wa dawa za miti shamba zikiwemo dawa za China ni kuandaa mwongozo wa usaji wa dawa za miti shamba. Mwongozo huu ulioandaliwa na *TFDA* unawatakawafanya biashara walioomba kusajili dawa za miti shamba nchini Kuwasilisha taarifa za kisayansi za dawa zao ili zifanyiwe tathimini ikiwa ni pamoja na uchunguzi wa kimaabara. Dawa hizo zinapaswa kuwa na *label* zenye maandishi ya lugha ya Kiswahili au Kiingereza au lugha zote mbili.

Katika kuimarisha udhibiti wa dawa za miti shamba kutoka China, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imetoa maelekezo kwa Kamati za Mikoa ambazo zinafanya kazi chini ya Uenyekiti wa Mkuu wa Mkoa, kuzitoa kwenye soko dawa zote za kichina ambazo hazikidhi matakwa ya Sheria. Vile vile wafanya biashara wa dawa hizo wanaokiuka masharti ya vibali walivyopewa kuchukuliwa hatua za kisheria.

(c) Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha dawa za miti shamba za China zinazingatia mahitaji ya kisheria ya kuandika maelezo ya matumizi yake katika lugha zinazoeleweka kwa wananchi, Serikali imewaagiza watengenezaji na waagizaji dawa hizo kuandika maelezo ya dawa hizo katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza.

Aidha, mwezi Machi, 2006, Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii alitoa tamko kupitia vyombo vya habari:-

Kuwaonya wanaouza dawa hizo kuwa wamevunja sheria na kwamba iwapo wataendelea watachukuliwa hatua.

Kuwatahadharisha wananchi kuwa kutumia dawa hizo ni hatari kwa afya zao na maisha yao kwa kuwa hazijahakikiwa.

Kuwashauri wananchi kupata dawa zao kutoka kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na maduka ya dawa yaliyosajiliwa.

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Spika, kwa vile dawa hizi zimezagaa nchini kwetu si za miti shamba peke yake. Ningeomba kwamba dawa hizi zizuiwe mara moja mpaka pale zitakapothibitishwa kwa sababu tunahatarisha maisha ya wananchi wetu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Swali la misingi lilikuwa linaulizia dawa za kichina, lakini kama nilivyoelezea katika jibu langu la msingi ni kwamba *TFDA* na Serikali kwa ujumla inafanya udhibiti wa dawa zote na kama nilivyozungumza katika majibu yangu ya awali nimesema katika Mikoa kuna Kamati ambayo inaongozwa na Mkuu wa Mkoa ili kuangalia dawa zote zilizoko katika maduka na wananchi wanaotumia zina ubora maalum. Kwa hiyo, ningeomba kutoa tamko tena au kuagiza kwa mara nyingine kwamba kuanzia sasa hivi katika Mikoa, Wakuu wa Mikoa na Kamati zao wapite katika kila maduka na kuona kwamba zile dawa ambazo zimeharibika au hazina ubora maalum basi ziondoke katika soko na vilevile *TDFA* wataendelea kufuatilia na Serikali kwa ujumla.

**SPIKA:** Kabla hatujaendelea na swali linalofuata naomba nimtambue mgeni aliyekaa kwenye *Speaker's Gallery* ambaye sikufahamishwa mapema lakini sasa nimefahamishwa ni mkewe Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Juma Akukweti. (*Makofi*)

Nimefanya hivyo kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wananiandikia karatasi kwamba huyo mgeni wako ni nani? Karibu sana. Swali linalofuata, Wizara ya Miundombinu, Mheshimiwa Kaika Telele, uliza swali lako.

Na. 45

**Ujenzi wa Barabara toka Mugumu – Mto wa Mbu**

**MHE. KAIKA SANING'O TELELE** aliuliza:-

Kwa kuwa yamekuwepo malalamiko na kero nyingi kutoka kwa wananchi husasani wasafiri na wafanyabiashara kwa upande mmoja na wanamazingira na wahifandi kwa upande mwingine kuhusu na barabara inayopita katikati ya hifadhi ya Serengeti na Ngorongoro:-

(a) Je, Serikali inao mpango wowote wa kujenga barabara kutoka Mugumu (Tabora B) kupitia Loliondo, Engaresero, Engaruka hadi Mto wa Mbu ili kuondoa adha wanayoipata wananchi wanaopita katikati ya Hifandi kwa shughuli zao mbalimbali katika miji ya Arusha, Mwanza na Musoma:-

(b) Je, ni lini barabara hiyo itaanza kujengwa na kwa kiwango cha gani?

*(Hapa kulitokea hitilafu ya mitambo ya sauti)*

**SPIKA:** Kama sauti haisikiki kwenye *microphone* maana yake *Hansard* hawawezi kunukuu na taratibu za Bunge haziendi bila *Hansard* hatuwezi kuwa na kipindi

ambacho *recording* haikufanyika. Kwa hiyo, kama tayari Mheshimiwa Naibu Waziri hebu jaribu tena, uendelee.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON MOKONGORO MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, Mbunge wa Ngorongoro, naomba na mimi nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Yusuf Makamba, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge na kwa kuongezea idadi ya Wabunge wa Dar es Salaam ndani ya Bunge hii Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara ya Mugumu – Loliondo – Mto wa Mbu ipo katika Mikoa ya Mara na Arusha na sehemu kubwa ya barabara hii inapatika wakati wa kiangazi tu. Barabara hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

Mugumu – Tabora B (km. 60), Tabora B- *Kleins Camp* (km. 52), *Kleins Camp* – Loliondo (km.90) na Loliondo – Mto WA Mbu (km 213). Urefu wa barabara nzima ni kilometa 452. Kati ya *Kleins Camp* na Loliondo barabara inapatika wakati wa kiangazi tu. Aidha, takriban asilimia 80 ya sehemu ya barabara ya Loliondo hadi Mto wa Mbu inapitika wakati wa kiangazi tu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuijenga. Barabara hii ili kuibua uchumu wa Mkoa wa Mara na maeneo husika ya Mkoa wa Arusha na kukuza utalii katika Hifadhi za Serengeti, Ngorongoro na katika pori la Loliondo.

Kutokana na umuhimu wa barabara hiyo aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge, Serikali ina mpango wa kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami na tayari mradi huo umewekwa katika mpango wa maendeleo kuanzia mwaka 2006/2007.

(b)Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2006/2007 shilingi 400 milioni zimetengwa kwa ajili ya kuanza kufanya upembuzi yakinifu na tayari Serikali kwa kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) imeitisha zabuni kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu kwa barabara kati ya Natta – Mugumu – Tabora B – *Kleins Camp* – Loliondo hadi Mto wa Mbu. Aidha, tunategemea fedha za mfadhili kuongezea bajeti hiyo endopo haitatosheleza.

Baada ya napo usanifu wa kina utafanyika na hatimaye kuiwezesha Serikali kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami kutegemea na matokeo ya upembuzi yakinifu yatakayokuwa yamechambua kwa kina masuala yote ya kiuchumi.

**MHE. KAIKA SANING'O TELELE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa barabara hii kama

itajengwa nikiungo muhimu sana kati ya Mikoa ya Arusha na Mkoa wa Mara, lakini vilevile ni kiungo kati ya Wilaya nne ambazo barabara hii itakuwa inapita kama itajengwa.

Wilaya ya Monduli, Loliondo, Longido, Ngorongoro na Wilaya ya Serengeti. Kutokana sasa na upembuzi yakinifu ambao unatabia ya kuchukua muda mrefu ni lini upembuzi huo utakuwa tayari ili kuanza ujenzi wa barabara hii ambayo ni muhimu sana kwa wananchi wa Mikoa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, sidhani kama upembuzi yakinifu huwa unachukua muda mrefu kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema.

Lakini ni utaratibu tu kwamba ukimaliza suala la *survey* baadaye utakwenda kwenye *design* na baadaye ndipo ujenzi. Nataka nimhakikishie kwamba Serikali ina nia thabiti kama nilivyosema ya kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami na umuhimu ambao barabara inao katika kukuza uchumu aliyoutaja na Serikali inakubali.

Kwa hiyo avute subira ili Serikali ichukue hatua ambazo nimezieleza na hatimaye barabara hii iweze kujengwa kwa kiwango cha lami ndani ya miaka michache ijayo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya Ziada, Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu!

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ningeomba kuongezea jibu zuri la Mheshimiwa Naibu Waziri wangu kwa kusema kwamba ni kweli nakubaliana na hisia za swali lake kwamba barabara hii ni ndefu sana. Na kwa sababu hiyo ingawa kwa kuanzia tulilenga kutumia fedha zilizotengwa kwenye Bajeti kama alivyosema Mheshimiwa Naibu wangu. Na kwa kuwa hivi karibuni, Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Mara ambayo Makamu Mwenyekiti ni Mbunge mwenetu hapa Mheshimiwa Stephen Wasira, ilikaa na kuniandikia barua yenye kuonyesha hisia hizo hizo kwamba kasi mpya inatakiwa katika kutekeleza mradi huu. Kwa kuwa kuna dalili kubwa kabisa za ongezeko la uwekezaji katika eneo la barabara hii haya maeneo kati ya Nata, Mugumu na tayari Mahoteli Makubwa ya Kimataifa yamekwishajengwa na yanaendelea kubuniwa na kujengwa. Na kwa kuwa kuna mpango kamambe unaoitwa *The North Mara Development Plan* ambao tayari kimsingi umekwisha idhinishwa na Rais lakini kuna kazi ndogo za kufanya. Basi, kuna umuhimu wa kwenda kwa kasi mpya klabisa katika utekelezaji wa barabara hii na mimi ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Telele, kwamba kutokana na hali hiyo, tutaweweka wataalam wengi zaidi yaani kampuni nyingi zaidi za kufanya kazi hizi za awali za kupima, kuchora, za kufanya *Environmental Impact Study* ili kusudi barabara hiyo iweze kutekelezwa kwa kasi kwa sababu ni ndefu sana na inahitaji idadi kubwa na *consentration* kubwa zaidi ya utekelezaji. Kwa hiyo nachukua wazo hilo na nitalishughulikia ipasavyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka tulitumia muda katika Kiapo cha Uaminifu na pia Hati za kuwasilisha mezani. Tuliweka ni kama dakika kumi hivi. Kwa

hiyo, ninaongeza muda ili tumalize haya maswali. Kwa hiyo, namwita sasa Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji.

Na. 46.

**Madeni yanayoachwa na Wapangaji wa Nyumba za Serikali**

**MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI** aliuliza:- Kwa kuwa, katika nyumba nyingi za Ujenzi wapangaji wanaohama huacha madeni ambapo mpangaji mpya hulazimika kulipa madeni hayo ili aendelee kuishi katika nyumba husika:-

(a)Je, Serikali inalielewa jambo hilo?

(b) Kama inalielewa, ni hatua gani zinachukuliwa?

(c) Kwa nini Serikali haifanyi matengenezo katika nyumba hizo, mfano kama maji yamekatwa au vyoo kuharibika na kumwachia mpangaji kufanya matengenezo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDO MBINU (MHE. DR> MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli Serikali inaelewa kuwa baadhi ya wapangaji wanaopanga nyumba za Serikali wanayo tabia ya kuacha madeni bila kuyalipa. Madeni haya yako katika makundi mawili. La kwanza, ni deni linatokanalo na mpangajia au mtumishi kutolipa pango la nyumba anayokaa. Kundi la pili, ni deni linalotokana na mpangaji au mtumishi kutolipa gharama za huduma muhimu kama vile maji safi, maji taka, umeme, simu na kadhalika.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa deni la kundi la kwanza, deni linalotokana na mpangaji kushindwa kulipa kodi ya pango, Serikali kupitia Wakala wa Majengo inaandaa taratibu zitakazowezesha wote wanaoshindwa kujibu kwamba wanachukuliwa hatua za kisheria ili kuhakikisha kuwa deni linalipwa. Kwa upande wa mtumishi ambaye pia anadaiwa, Wakala wa Majengo anaendelea kuwasiliana na mwajiri wake ili kuhakikisha deni hilo linalipwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa deni la aina ya pili yaani deni linalotokana na mpangaji au mtumishi kutolipia gharama za huduma muhimu kama vile maji na umeme, imekuwa vigumu kwa Serikali kuwabana kwa vile mpangaji au mtumishi anaingia mkataba moja kwa moja na watoa huduma hizo bila Serikali kuhusishwa. Hata hivyo, kwa kutambua kuwa watoa huduma kama vile *TANESCO* na Mamlaka ya Maji ni Asasi za Serikali na pia wanajiendesha kibiashara. Wizara yangu kupitia Wakala wa Majengo imekuwa ikitoa nakala ya barua za kupangiwa nyumba *(Alocation Letter)* ya kila anayepangiwa nyumba za Serikali kwa mamlaka husika ili kurahisisha ufuatiliaji wa malipo ya Ankara na huduma zinazotolewa.

Hatua nyingine ambayo Serikali inatarajia kuichukua ni kuweka utaratibu wa kuwa na *Clearance Form* ambayo itamtaka mpangaji wa nyumba kabla hajahama, azipitishe kwenye malaka husika ili mamlaka hiyo ionyeshe katika *form* hiyo kuwa mpangaji hadaiwi.

Hatua hii itasaidia kumfanya mpangaji alipe madeni yote anayopaswa kulipa kabla ya kuhama kwenye nyumba ili mpangaji mpya asipate bughudha yoyote kutoka kwenye mamlaka zinazohusika na kuleta usumbufu usio wa lazima kutokana na huduma hizo kusitishwa.

(c) Mheshimiwa Spika, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa Serikali inao wajibu na imeendelea kuwajibika katika kuzifanyia matengenezo na na marekebisho nyumba zote zinazohitaji kufanyiwa matengenezo ya aina yoyote pale bajeti inaporuhusu.

Aidha, inapotokea kuwa Serikali haina fedha za kutosha kutokana na ufinyu wa bajeti na kwamba ni lazima nyumba husika ikafanyiwa matengenezo katika kipindi hicho hicho, basi mpangaji anaweza kuomba kibali cha kufanya matengenezo ya nyumba kwa gharama zake kulingana na taratibu na viwango vilivyowekwa na Serikali. Baada ya Serikali kupata fedha, hurudishiwa gharama zake. Utaratibu huu wa matengenezo unahusu wapangaji waliomba kibali na kuruhusiwa tu.

**MHE. ELIZABETH NKUNDA BATENGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumezuka mtindo wa baadhi ya watu kumiliki zaidi ya nyumba moja katika eneo moja au mji mmoja. Lakini wapo watu wengine wanaohitaji nyumba hizo. Je, Serikali inalijua hili na inalichukulia hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, Serikali haijui hali hiyo na kama Mheshimiwa Mbunge anajua watumishi wa umma wanaokaa au walipangiwa nyumba mbili za Serikali, basi atusaidie kwa kuleta taarifa husika ili tuweze kuchukua hatua zinazostahili.

Na. 47

**Kero ya Maji Katika Vijiji vya Jimbo la Njombe Magharibi**

**MHE. YONO STANLEY KEVELA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, na mimi nichukue nafasi hii kuungana na Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Yusufu Makamba kuwa Mbunge. Kwa kuwa, kwa kipindi kirefu kumekuwa na kero kubwa ya upatikanaji wa maji ya kunywa katika vijiji vya Lyamluki, Lyadembwe, Saja na vilivyoko Ikulimambo kwenye Tarafa ya Mdandu, Imalinyi na Wanging'ombe ambako huchukua saa nane kwa mwananchi kwenda kutafuta maji ndoo moja:-

Je, Serikali haiwezi kuandaa mradi wa dharura wa kuchimba visima virefu kama ilivyo kwa jirani zetu Rujewa ili kusogeza huduma ya maji karibu na wananchi na kuwaondolea kero wanayopata ya kutafuta maji mbali?

**NAIBU WAZIRI WIZARA YA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Vijiji vya Lyamluki, Lyadembwe na Saja, vinapata huduma ya maji kutoka mradi wa Wanging'ombe ambao chanzo chake ni Mto Mbukwa na unahudumia zaid ya Vijiji 60. Kijiji cha Mdandu kinapata huduma ya maji kutoka mradi wa *Mdandu Gravity Water Supply*. Aidha, Kijiji cha Imalinyi, kinapata huduma ya maji kutoka mradi wa *Imalinyi Water Supply*.

Vyanzo vya maji katika miradi yote hii mitatu, hupungua maji wakati wa kiangazi na kusababisha hali ya kutotosheleza mahitaji katika vijiji hivyo na hatimaye kusababisha kero kubwa ya upatikanaji wa huduma ya maji. Hata hivyo kero hii huwa inatokea wakati wa kipindi wa kiangazi kutokan na wananchi wachache kuharibu kwa makusudi, kupasua mabomba na kufungua vibanio *(valves)* vilivyoko kwenye njia kuu wakati wakiwa na lengo la kunyweshea mifugo na kumwagilia mashamba yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Yono Stanley Kevela kama ifuatavyo:- Ili kukabiliana na kero kubwa ya maji Serikali imekuwa ikichukua hatua mbali mbali ikiwa ni pamoja na:-

(a) Kutoa maelekezo kuhusu kuhifadhi mazingira na hasa vyanzo vya maji kama lilivyotolewa tamko tarehe 1 Aprili, 2006 Jijini Dar es salaam na Mheshimiwa Makamu wa Rais kuhusu Mkakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji. Hivyo, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kutoa Elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kuitunza vyanzo vya maji na miradi yao ya maji.

(b) Pia Serikali imeendelea kukarabati mradi wa Wanging'ombe. Katika kipindi cha mwaka 2004/2005 Wizara yangu ilipewa shilingi milioni 53 kwa ajili ya ukarabati huo. Aidha katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Wizara yangu imetenga jumla ya shilingi milioni 45 kwa ajili ya kuendelea na ukarabati na pamoja na uendeleshaji wa mradi huo.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekili kwamba kuna kero kubwa ya maji na kwa vile sisi tayari tumeishafanya upembuzi yakinifu yaani tathmini, tukaona mradi ule unagharimu zaidi ya milioni 500. Je, Serikali ina mpango gani wa kuukarabati huu mradi kwa sababu ulianzishwa muda mrefu na katika hizi Tarafa zxa Mdandu, Wanging'ombe na Imalinyi. Kwani kwa sasa mabomba yaliyo mengi yanatoa hewa badala ya maji na hii inaleta kero kubwa kwa akina mama na watoto kwa kusababisha magonjwa ya mlipuko hasa hili gonjwa la kipindupindu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu langu la awali nimeeleleza kwamba Serikali iko katika jitihada za kufadhili miradi hiyo. Na pia ningependa kumshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tuna Mpango kabambe wa maji na usafi wa mazingira. Ningemshauri kwa yale ambayo sikuyataja hapa kwamba yanafadhiliwa kwa mwaka huu, namshauri ya kwamba hizo kazi zilizobakia kwa miradi hiyo mingine aiingize katika programu hii akishirikiana na Halmashauri ya Wilaya yake.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa Maswali umekwisha. Tulibakiza swali la Mheshimiwa Juma Said Omar, Mbunge wa Mtambwe ambalo akiridhia kesho tutaliweka mapema ili liweze kuulizwa na kujibiwa kesho. Kabla hatujaendelea na ajenda inayofuata. Ninaomba kutangaza kwamba Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira anaweaita wajumbe wote wa Kamati hiyo ya Maliasili na Mazingira kwenye kikao muhimu kitakachofanyiaka katika jengo la Utawala ghorofa ya kwanza, chumba namna 133 saa tano asubuhi ya leo.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2005, Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2006/2007 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2006/2007

**MHE. DR. MZERU OMAR NIBUKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kwa kuwa wa kwanza wa kuweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha.

Awali ya Yote, napenda niwapongeze Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha kwa jinsi walivyowasilisha hotuba zao ambazo kwa kweli zimetusisimua na zimewapa imani Watanzania kwa jinsi zilivyojieleza.

Mheshimiwa Spika, kama alivyoeleza Waziri wa Fedha kwamba Serikali ina lenga kukusanya mapato yake ya ndani kuwa 2,066,751,000,000/= kama ilivyoeleza kwenye ukurasa wa saba.

Mheshimiwa Spika, lakini wasi wasi wangu unakuja, jinsi ya utekelezaji wa kuzipata hizi pesa ambayo ndiyo Makadirio yaliyolengwa kwenye Mapato ya Serikali. Kwa sababu huko nyuma, Bajeti nyingi zilikuwa zimeishajieleza na zilikuwa na malengo mazuri tu lakini matokeo yake, utekelezaji wake mara nyingi unakuwa siyo mzuri kutokana na watendaji.

Mheshimiwa Spika, sasa ninachotaka kuzungumzia ni kwamba ili tufikie malengo haya ni vizuri kuwe na usimamizi mzuri kama alivyoeleza Waziri wa Fedha jinsi gani tunaweza tukasimamia ili tuweze kupata mapato haya. Lakini, wasi wasi wangu unakuja katika ufuatiliaji. Sasa, ninapenda kutoa ushauri mdogo kwamba ili wananchi kwanza wawe na imani na malengo pamoja na matokeo ya utekelezaji, ninashauri kwamba baada ya Bajeti hii miezi mitatu au sita ijayo, basi Serikali angalau ifanye tathmini na kuwatangazia wananchi kwamba angalau Serikali imepata ongezeko au faida katika hali halisi ya mapato katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini wasi wasi wangu unakuja katika jinsi ya kusimamia Ongezeko la Thamani *(VAT)*. Kwamba katika makusanyo ya *VAT* mara nyingi tunategemea wafanyabiashara wa aina tatu:- Wafanyabiashara wakubwa, wafanyabiashara wa Kati na Wafanyabiashara Wadogo. Hawa wafanyabiashara wakubwa wanajulikana kwa sababu idadi yao ipo na wao wenyewe wamejiandikisha na wao wenyewe ndio wamejiwekea malengo jinsi ya ukusanyaji. Hawa hawana matatizo, lakini ni wachache.

Lakini ninavyojua ni kwamba wafanyabiashara wa kati na wafanyabiashara wadogo, hawa ndio wengi sana na kama Serikali ingekuwa inasimamia vizuri kuhakikisha kwamba hawa wote wanalipa *VAT*, maana yake Serikali ingekuwa na pesa nyingi kuliko hata hizo zinazotokana na wafanyabiashara wakubwa. Sasa, shida inakuja katika jinsi ya kudhibiti. Kwa mfano kama walivyozungumza Wabunge waliopita, ukienda dukani, unaambiwa bidhaa hii bei yake shilingi labda 200, ukitaka nikupe risiti bei inaongezeka.

Lakini ukitaka nikupunguzie, tuondoe risiti. Sasa, wasi wasi wangu unakuja ni kwamba Je, Serikali imejiandaaje katika kuhakikisha inafuatilia suala hili? Na, Je, inawezekana, kwa sababu kwanza wafanyabiashara hawa ni wengi na maduka ni mengi, nafikiri itakuwa ngumu sana jinsi ya kufuatilia. Sasa, sijui Serikali imejipangaje katika kuhakikisha kwamba inakusanya kodi zake kwa wale wafanyabiashara hasa hawa wadogo na wafanyabiashara wa Kati, kwa sababu wafanyabiashara wakubwa hawana matatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilitaka nitoe rai hiyo kwamba Serikali ijipange vizuri angalau tusipoteze mabilioni ya pesa kutokana na wafanyabiashara ambao sio waaminifu.

Mheshimiwa Spika, lakini, bado katika ukusanyaji hasa katika bidhaa muhimu kwa mfano bidhaa za mafuta n.k. Utakuta bado watendaji kama walivyozungumza wazungumzaji waliopita jana ni kwamba bado watendaji wetu siyo waaminifu katika suala hili. Ni kwamba bei za mafuta zimeishapangwa lakini utakuta katika utekelezaji wake muda si mrefu tayari wananchi wananza kupata matatizo, nauli zinapanda, mafuta yanapanda. Sasa, udhibiti wake unaonekana kwamba kama vile bajeti imewadanganya wananchi badala ya kwamba kweli bajeti ilikuwa na nia ya kuwasaidia wananchi. Ninachoomba ni kwamba hapa kuwe na udhibiti wa kutosha ili angalau wananchi wawe na imani na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, ninataka sasa nielezee kidogo katika maamuzi ya Serikali wakati mwingine. Wakati mwingine Serikali kwa nia nzuri tu, inatoa maelekezo kwa wananchi wake ili angalau kuwwe na utaratibu mzuri katika masuala fulani, kwa mfano; kipindi kilichopita Serikali ilitoa amri au maelekezo kuhusu suala la mazingira kwamba mazingira yanachafuliwa kwa mfano katika ukataji mkaa. Mkaa watu wanakata miti hovyo, wanachoma mkaa, kitu ambacho ni kwamba mazingira yanachafuliwa. Lakini, sasa utakuta amri hiyo ikishatolewa kwamba kuwe na utaratibu mzuri jinsi ya ukataji wa mikaa, utakuta watendaji wetu huku chini sasa inakuwa kama vile maaskari wale wa Makaburu jinsi wanavyo watesa wananchi. Kunakuwa hakuna utaratibu mzuri. Kwa mfano kuna wananchi ambao wamekata mkaa wao kwa ajili ya kutaka kwenda kufanya matumizi au kufanya biashara ndogo ndogo za kuweza kukimu maisha yao. Lakini utakuta wafanyabiashara hao wananyang’anywa mikaa yao na mikaa hii haiendio Polisi, haiendi wapi! Sasa, wanaowakamaata, wakiishawakamata wanawadhuruma na mikaa hii wanaitumia wao wenyewe. Sasa, ninaomba kwamba wananchi wapewe utaratibu jinsi gani ya kuhifadhi mazingira lakini siyo kunyanyaswa kwa sababu mkaa sasa hivi ndiyo nishati muhimu au nishati pekee ambayo inawasaidia watanzania wengi na hivi ninavyozungumza sisi Wabunge hapa pamoja na kwamba kipato chetu kiko juu, hakuna Mbunge ambaye anaweza kusema hawezi kutumia mkaa. Watu wote tunatumia mkaa. Kwa hiyo, ni suala tu la utaratibu jinsi gani ya kueleza angalau wasinyanyaswe.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, liko suala la uhamaji, ni kwamba wako wananchi wanaokaa juu ya milima, kwa kukaa kwao kule ni kwamba wanaharibu mazingira kwa sababu wanakata miti mingi lakini pia wanalima kandokando ya mito. Hilo ni kweli, kwa hiyo lazima tufanye utaratibu angalau tuwahamishe. Lakini, kabla hatujawahamisha tuhakikishe tumewaandalia makazi kule wanakokwenda. Tusiwahamishe tu kama tuwahamishe ng’ombe. Unamwambia mtu hama, akakae wapi, akajenge wapi! Hujamwandalia kiwanja, hujafanya kitu chochote, hujamlipa fidia, huyo mtu ataenda kula wapi! Kwa hiyo ninaomba tunapofanya maamuzi tujaribu kuwa wastaarabu, kwa sababu hawa tunaowafanyia maamuzi ndio watu wetu ambaowametupa kura sisi tukaja Bungeni.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, nataka nizungumzie sasa katika suala la matumizi ya chakula. Serikali imetoa tamko, kwa mfano mahindi mabichi, mahindi mabichi yasiuzwe kwa kasi kwa maana ya kwamba tusije tukakosa nafaka muhimu za mahindi kwa ajili ya chakula cha baadaye. Lakini tukumbuke, ni kwamba wananchi hawa

wanalima kwa malengo ya kupata kipato. *Let's say* mtu analima labda heka tatu za mahindi. Yeye mwenyewe kwa sababu ana akili anapanga kwamba heka moja na nusu nitauza mahindi mabichi, heka moja na nusu nitaacha yakauke ili nipate nafaka ya kula mimi pamoja na wananchi wengine.

Katika ulimaji huo hawa wananchi wengine kutokana na hali zao duni wanafanya kukopa pesa kwa wenzao pengine pamoja na riba na riba hiyo pengine mtu anawekewa labda baada ya miezi mitatu awe amerudishiwa. Lakini mwananchi huyo anapotaka kuuza mahindi mabichi, tayari imekuwa kero, hakuna kuuza, hakuna kufanya nini! Huyu mwananchi anauza mahindi mabichi kwa sababu anajua mahindi mabichi ndio yenye faida kubwa kuliko mahindi makavu. Sasa anapanga kamba nusu auze mabichi, lakini nusu yakauke ili aweze kulima. Sasa, unapomzuia sijui Serikali wakati wewe hujamwandalia, hujmpa molea bure, hujampa pesa, hujampa shamba, hujampa trekta la kulima, unakuja kum-control kwenye kuuza. Mimi nafikiri hii siyo haki. Ni kama vile tunawanyanyasa wananchi wetu. Utaratibu uwepo, lakini tuwaelimishe lakini pia tuhakikishe kwamba tunawapa uhuru wa kufanya yale wanayoweza kwa ajili ya kusomesha vijana wao  na vitu vingine.

Kwa mfano yapo mazo mengine kama viazi, mihogo, ndizi. Malori kwa malori yanapelekwa Dar es salaam. Hakuna anayeuliza. Kwa hiyo,  sasa tuchukulie chakula ni mahindi tu au ndizi siyo chakula! Kwa sababu iko mikoa mingine hawali chakula kingine ni ndizi tu, sasa mbona hawaulizwi! Kwa nini wanapeleka Dar es salaam. Kwani ndizi haziwezi kuleta njaa!  Kwa hiyo, ninaomba tusiwaonee tu hawa  wanaolima mahindi, lakini, kama ni kudhibiti, tudhibiti bidhaa zote.

Mheshimiwa Spika, pia yako mazao kwa mfano ya mchele. Mimi nataka nitoe mfano kwa Mkoa wangu wa Morogoro. Mkoa wa Morogoro ziko Wilaya zinalima mpunga kwa wingi, lakini mpunga huu unapokuwa tayari umekomaa, maana yake tunauziana ndani nkwa ndani na mwingine kuupeleka nje ya Mkoa, lakini ndani ya nchi ili kusudi wnanchi waweze kupata chakula. Lakini sasa hivi ziko amri zimetolewa, mchele hauwezi kuuzwa hata kutoka Wilaya moja kwenda Wilaya nyingine. Hasa kwa mfano kuna Wilaya ya Kilombero ambayo ni maarufu sana kwa kulima Mpunga na Wilaya ya Ulanga. Kule kwa sasa hivi bei yake ni shilingi 500/- Lakini ukija Morogoro Mjini pale Manispaa, mchele unauzwa shilingi 1500/- na hii inatokana na hivi kwa sababu mchele huu hauwezi kutoka kule kwenye Wilaya nyingine ukaja mjini. Sasa hii Sheria ya kusema kwamba mchele usiuzwe, sasa watakula akina nani! Kwa sababu sisi wakaazi wa Mkoa ule ndio tunatakiwa tuutumie ule mchele. Mimi ninafikiri Serikali ingekuwa tu ni busara kuzuia ule mchele usiuzwe nje ya nchi.  Lakini siyo hata kuuza ndani ya Mkoa iwe matatizo. Ni kama vile tunawanyanyasa wananchi  wetu. Kwa hiyo, ninaomba Serikali ijipange vizuri katika kutoa maamuzi mazuri kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia suala hilo, sasa nirudi kidogo kwenye suala la Elimu. Kwenye suala la elimu Sera ya nchi yetu inasema kwamba angalau sekondari moja kwa kila Kata ya Tanzania. Na mimi naafiki kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini nimeona hizi sekondari hizi tunazozijenga kwa mtindo wa zima moto, angalau sekondari moja au zaidi kwa kila Kata, ni kwamba sekondari hizi hazina ubora kabisa. Utakuta sekondari hizi zimejengwa, kwanza hata ofisi za walimu hazipo. Utakuta mwalimu anapewa darasa moja miongoni mwa madarasa, inakuwa ndiyo ofisi yake. Sasa utakuta hata heshima ya mwalimu inakuwa ndogo kwa sababu hata mwanafunzi akikosa akiitwa na mwalimu akienda kwenye ofisi ya mwalimu na mwanafunzi huyo anona mwalimu huyo yuko kwenye darasa kama analokaa yeye. Anaona yeye na mwalimu hadhi zao zinafanana hata heshima inakuwa haipo. Kwa hiyo, nafikiri tungefanya juhudi za makusudi angalau tuziimarishe hizi sekondari ili angalau walimu na wenyewe waweze kufanyia kazi mahali pazuri. Kwa sababu mtu anapofanyia kazi mahali pazuri kwanza anapata imani, ana *confidence* na anajiona kwamba kweli anaheshimika.

Mheshimiwa Spika, na sisi wenyewe inakuwa ni mfano. Sisi tulikuwa kwenye jengo la zamani na sasa hivi tumehamia jengo jipya la Bunge. Hapa tulipo tunajisikia kwamba tuko kwenye jengo zuri, la kupendeza na kwamba Serikali imetuthamini kutupa jengo kama hili. Kwa hiyo walimu na wafanyakazi wengine ni vizuri na wenyewe wafanye kazi katika sehemu zenye mazingira mazuri. Lakini samababamba na ofisi shule hizi za sekondari hazina maabara, hazina maktaba, lakini pia hazina nyumba za walimu. Sasa, utakuta mwalimu anakaa labda kilomita 5. Mwalimu huyu kwa mfano kama kule mjini lazima apande basi labda dala dala mbili au tatu ndio afike shuleni. Kwanza, akifika atakuwa amechwelewa, lakini pia hata kama kungekuwa na masomo ya ziada kwa ajili ya wanfunzi masomo ya jioni au masomo ya usiku yanaweza yasifanyike kwasababu mwalimu yule yuko mbali na shule. Kwa hiyo, ninaomba kwamba katika mpango wa MMES sambamba na kujenga madarasa ya shule, lakini nafikiri ingekuwa ni vizuri tungejenga na nyumba za walimu ili angalau kuwe na kwanza tuwajengee mazingira mazuri hao walimu, wakae karibu na shule ili waweze kupata nafasi ya kuweza kufundisha kwa muda wa kutosha na wanafunzi wetu waweze kupata elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka nizungumze hilo na hili hasa, hata juzi nilikuwa Morogoro, nimetembelea baadhi ya sekondari za pale Morogoro mjini na hilo jambo miongoni mwa mambo ambayo waliniambia walimu katika kila risala ya shule nilikuta kwa kweli matatizo haya yanafanana, hakuna ofisi, hakuna maabara, hakuna maktaba na hakuna nyumba za walimu. Lakini jingine ambalo nimeligundua ni kwamba katika shule zetu hakuna maeneo ya kutosha kwa ajili ya sekondari. Utakuta sekondari imekuwa finyu imejibana kwamba hata baadaye ukitaka kufanya maendelezo, uiendeleze ile sekondari labda iwe *high school* au vipi utashindwa kwa sababu eneo halitoshi. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria Serikali kwa sasa hivi kwa kutegemea hawa watendaji wetu wa Wizara ya Ardhi ni vizuri shule za sekondari zinapojengwa zitengewe maeneo ya kutosha ili kwa ajili ya maendeleo ya baadae. Kwa sababu sisi watanzania tuna kawaida moja, tunajiwekea malengo ya miaka ya mitano au kumi ijayo badala ya kuweka malengo ya mika 50 au 100 ijayo. Kwa hiyo nafikiri hilo lingekuwa jambo la busara angalau.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia suala la kilimo, naomba sasa nizungumzie suala la ....

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji Kumalizika)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ni kengele ya pili.

**MHE. DR. MZERU OMAR NIBUKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, naomba niunge hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, kukupongeza wewe kwa jinsi ambavyo unatuongoza. Kwanza kabisa ulipochaguliwa kuongoza Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ulisema kwamba utatekeleza majukumu yako kwa *standard and speed*. Sisi Wabunge leo ni mashahidi wako kwamba yale yote uliyoyazungumza sasa yameanza kuzaa matunda na yanaonekana wazi na ndiyo maana leo tuko katika ukumbi mzuri wa Bunge letu hilo ambalo lina *standard* ya kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia naomba nichukue nafasi hii kutoa rambirambi zangu za dhati kabisa kwa ndugu jamaa wa marehemu wa wale waliopata ajali mbaya kutokana na basi lililokuwa linatokea Mererani kutumbukia kwenye Mto Malala Wilaya ya Arumeru na kuweza kupoteza watu 54. Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, ajali ni ajali lakini kuna ajali zingine zinazochangiwa na uzembe hususan uzembe wa madereva. Hivi inaweza kuingia akilini kweli kwamba basi lenye uwezo wa kuchukua abiria 25 au abiria 30 linaweza kuchukua abiria 74 yaani zaidi ya uwezo wa basi lenyewe? Huu ni uzembe mkubwa Waheshimiwa Wabunge, hili tunatakiwa tulikemee kwa nguvu zetu zote.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jinsi ambavyo alisikia habari hizi na kwenda kutembelea eneo lile na kukutana na ndugu wa Marehemu kwa ajili ya kuwafajiri na kuwapa pole wale ambao walinusurika. Aidha nichukue pia nafasi hii kuunga mkono kauli yake aliyosema katika vyombo vya usalama barabarani kwamba matrafiki watekeleze wajibu wao.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pia kuwapongeza Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwekezaji Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa. Pia nampongeza sana Mheshimiwa Mama Maghji, Waziri wa Fedha kwa hotuba zao nzuri walizoziwasilisha katika Bunge lako tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ni bajeti ya kwanza kabisa katika uongozi wa Awamu ya Nne, baada ya uchaguzi Mkuu wa Rais na Wabunge. Aidha Bajeti hii ni ya kihistoria kuwasilishwa katika Bunge Tukufu na Wizara ya Fedha ikiwa inaongozwa na mwanamke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii inaitwa Bajeti ya Mama Maghji. Watanzania wote wana imani na matumaini makubwa na Bajeti hii kwa sababu ya utendaji wake na

historia yake nzuri ya utendaji kazi. Bajeti hii imejikita katika kujibu kero za kiuchumi zinazowakabili Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na misukosuko iliyotokea katika nchi yetu kama ukame, njaa, kupanda kwa bei za vitu kama mafuta n.k. lakini naipongeza Serikali kwamba imeweza kutekeleza bajeti yake vizuri bila wasiwasi. Hii inaonyesha kwamba mazingira na maboresho yaliyokuwa yanatekelezwa na Serikali yetu sasa yameanza kuzaa matunda na ndiyo imeweza kutekeleza wajibu wake au bajeti hii bila wasiwasi wowote.

Pia nachukua nafasi hii, kuipongeza Serikali katika kupata mafanikio makubwa katika sekta ya ujenzi hasa ujenzi wa barabara, mawasiliano na simu. Naiomba Serikali ihakikishe kwamba kazi ya ujenzi wa barabara iendelee ili kuweza kuboresha uchumi na hata biashara.

Mheshimiwa Spika, barabara nzuri ni vivutio vizuri pia kwa wawekezaji. Nachukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa jinsi ambavyo alitembelea Mkoa wa Manyara mwaka jana katika kampeni zake za uchaguzi na akaweza kuahidi kwamba barabara zote za Mkoa wa Manyara sasa zitajengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 16 mwaka 2006 alitembelea tena Mkoa wa Manyara mara ya pili na pia aliweza kukumbushia kwamba barabara zile zitajengwa. Alitamka wazi kwamba barabara inayoanzia Minjingu kwenda Babati – Kondoa na nyingine Babati hadi Singida, pia Simanjiro kwenda Babati. Hii barabara ni muhimu sana kwa sababu barabara hii ndiyo inayounganisha Mkoa wa Mara. Ni barabara ambayo ni muhimu sana ukiangalia wananchi wa Simanjiro na Kiteto, Makao Makuu yao ni Babati. Mzunguko huo ni mrefu sana ukizingatia pia barabara ni mbaya utakuta mwananchi anaumia sana. Ni Mwendo wa siku mbili hadi afike Mkoani kwenda na kurudi kwa hiyo utendaji wa kazi unakuwa shida.

Mheshimiwa Spika, tungeangalia eneo hilo barabara hiyo inayounganisha Mkoa wa Manyara kutoka Simanjiro hadi Babati iweze kutengenezwa ili kurahisishia wananchi wake shughuli za kikazi. Pia nataka kukumbushia tena barabara inayoanzia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Kilimanjaro *(KIA)* kwenda Mererani katika eneo la *Tanzanite*. Barabara hii ni mbaya na ni chafu sana inachafua mazingira na hata kwa wawekezaji inakua vigumu. Naomba barabara hii nikumbushie tena kwa sababu Rais wa Awamu ya Tatu na Rais wa Awamu ya Nne wote walikwishaahidi kwamba barabara hii itajengwa. Pia nielezee kwamba barabara hiyo umbali wake ni kama kilomita 26 hadi kilomita 30 haina umbali. Ni kwamba Serikali ingeweza ikafanya mipango mizuri hata kuwahususha makampuni makubwa ya wawekezaji tuweze kuona ni jinsi gani ya kuweza kujenga barabara ile.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue pia nafasi hii kuzungumzia suala la umaskini wa kipato. Naomba Serikali itupie macho sana katika haya yafuatayo:- Pamoja na pato la Serikali kufikia asilimia 6.8 bado Watanzania wengi hawana kitu mifukoni.

Naipongeza sana Serikali kwa mpango wake wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini (MKUKUTA). Mpango huu ukitekelezwa vizuri utasaidia kuboresha maisha ya wananchi wetu. Lakini jambo la kujiuliza. Je, huu wananchi wanaelewa maana ya MKUKUTA? Utakuja hata baadhi yetu sisi pia hatuelewi maana ya MKUKUTA. Naomba Serikali, ichukue jukumu la kuwaelimisha au kufanya semina kwa wadau mbalimbali kuelezea na kuelimisha watu waelewe nini maana ya MKUKUTA na ni jinsi gani ya kuweza kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, upande wa madini, mimi ni Mbunge ambaye natoka Mkoa wa Manyara, Wilaya ya Simanjiro, ambapo Mungu ametujalia rasilimali hii pekee inayoitwa *Tanzanite* inapatikana pale. Madini haya kama Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwekezaji alivyoelezea ni kwamba hata Serikali hainufaiki na madini haya. Ukiangalia kiwango anachosema kwamba eti uchumi ulikua kwa asilimia 15.7 mwaka 2005 na ukilinganisha na ukuaji wa asilimia 15.4 mwaka 2004 na kwamba mchango wa sekta ya madini uliongezeka kwa kiwango cha asilimia 3.5 mwaka 2005 kutoka 3.2 katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, hiki ni kiwango kidogo sana hata nimeona mbali na sisi wananchi wa Mkoa wa Manyara kutofaidika na madini haya bado naona Serikali haifaidiki. Naomba niungane na wale viongozi wetu wakuu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Mheshimiwa Edward Lowassa, waliposema kwamba mikataba yote ya madini irudiwe. Nachukua nafasi hii, kuiomba Serikali wakati itakapofanya hivyo naomba iwahusishe pia Wabunge katika kupitia mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba niunge mkono hoja hizi zote mbili. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwawezesha wanawake wa Mkoa wa Mwanza kunipa kura nyingi na kuniwezesha tena kurudi kwa awamu ya pili katika Bunge hili jipya. Naomba niwapongeze Mawaziri wote wawili waliotusomea Bajeti ya Serikali mmoja akituelekeza Mipango ya uchumi wetu unaendaje na mwingine kutuelekeza utekelezaji wa mipango hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi bila kuwa na mipango haiwezi kufanikiwa chochote. Ninawashukuru wananchi wa Tanzania walipoipokea Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kukipa kura nyingi kwa sababu Chama hicho kilionyesha mipango mizuri. Ninaomba waendelee kuamini Chama cha Mapinduzi na kuweka Serikali yao imara, sikivu inayowasikiliza Watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mipango ambayo tumeletewa katika Bunge hili kwa 2006/2007 imelenga sana Ilani ya Chama cha Mapinduzi, imeangalia hali ya uchumi wa Watanzania na imejaribu kutuelezea jinsi ya kuwawezesha Watanzania katika kushiriki kwa mipango mikuu mitatu ambayo imekuja katika awamu hii. Kuna MKUKUTA, MKURABITA na MKUMBITA.

Mheshimiwa Spika, mipango yote hii inaelekeza kuwawezesha Watanzania. Ukichukua malengo ya mipango hii ni ukuzaji wa uchumi na upunguzaji wa umaskini, uboreshaji wa maisha na ustawi wa jamii na utawala bora. Ninaomba sana kwa sababu MKURABITA, MKUKUTA na MKUMBITA ni maneno mazito lakini yote yanamgusa Mtanzania. Niombe basi Mheshimiwa Waziri wa Mipango elimu hii ielekezwe moja kwa moja kwa wananchi ambao ndio watakaoboreka na maisha kwa kutumia mipango yote hii mingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa nichangie katika suala la uwezeshaji. Suala la uwezeshaji watu wachache wanafikiria kwamba wanataka Watanzania wawekewe fedha mifukoni. Lakini suala la uwezeshaji ni katika kuwawezesha Watanzania washiriki vipi katika kuhakikisha kwamba wanakuza uchumi wao, wanashiriki kikamilifu katika biashara na katika utawala bora. Hivyo basi naomba elimu ielekezwe huko kwa wananchi ili nao washiriki katika mipango ambayo tumeletewa na Waziri wa Mipango.

Nitaanzia kwa kuwashirikisha wananchi. Tutawashirikishaje Watanzania tukianza kuwagawa wakulima wadogo kama wa Wilaya ya Kwimba, Wilaya ya Magu watashirikishwa vipi katika kuhakikisha kwamba wamewezeshwa? Zamani tulikuwa tunasema unawezesha katika kuwapa mikopo ya fedha. Lakini sasa nitaomba tuangalie upya suala la hili tuangalie badala ya kutoa fedha kwa nini basi tusiangalie kutoa nyenzo? Kwa mfano kama wakulima niliowataja wa Wilaya ya Kwimba na Magu wakapewa trekta au plau ambazo zinaweza zikawasaidia kwa ukulima mzuri. (*Makofi*)

Tuangalie wavuvi Mkoa wa Mwanza una Ziwa Victoria, tunawashirikisha vipi Watanzania waishio kando kando ya Ziwa Victoria kuna wavuvi wa Ukerewe, Sengerema, Magu na Wilaya ya Geita ambao wamezungukwa na Ziwa Victoria wanashirikishwa vipi katika masuala ya MKUKUTA, MKURABITA? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna wachimbaji wakuu sasa wa dhahabu katika Mkoa wa Mwanza, tunawashirikisha vipi hawa wananchi na sisi bahati nzuri sisi Mkoa wa Mwanza hatuchagui kazi hususan wanawake. Kuna wanawake wanaochimba dhahabu maeneo ya Geita. Tuna washirikishaje hawa wanawake walioko Nyarugusu, Geita, walioko Chifufu Sengerema washirikishweje katika kuhakikisha kwamba wanapewa nyenzo za uhakika za kuweza kuchimbia madini yao. (*Makofi*)

Tuna wafanyabiashara wadogo wadogo, wanashirikishwaje katika kuhakikisha kwamba wamehusishwa na mipango hii mitatu? Kwa mfano hawa wa Wilaya ya Ilemela Nyamagana ambao ni wa mjini huu MKUMBITA huu ni wakati mzuri sana wafanyabiashara wadogo wadogo ambao wanaweza wakawezeshwa kwa kupewa mikopo midogo na kupewa nyenzo ambazo zinaweza kuwasaidia. Lakini bado tuangalie makundi maalum walemavu, watoto yatima na wazee wanashirikishwaje katika kuhakikisha kwamba na wenyewe wanashirika katika kukuza uchumi wao?

Mheshimiwa Spika, kama tutafanikiwa katika mipango hii mitatu basi tutawasaidia wananchi. Mimi naomba nilete ombi kwenu kama kweli tutafanikiwa niombe Waziri wa Mipango, atuletee mkakati halisi wa kubadilisha kilimo. Tulizoea

kilimo cha kutegemea mvua, lakini sasa tuelekee kwenye kuboresha kilimo cha umwagiliaji. Kama kweli tunataka kukuza uchumi na kuboresha biashara za wafanyakazi lazima tufungue njia barabara. Kuna barabara ambazo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi, inasema kwamba barabara zitengenezwe za kufungua Wilaya kwa Wilaya na Mkoa kwa Mkoa. Kama kweli tunataka kuhakikisha kwamba hii mipango mitatu tuangalie barabara hii inayotoka Dodoma kwenda Mwanza, ikiwa ya lami wafanyabiashara watafaidika sana. Barabara ya kutoka Usagala kwenda Kisesa itakuwa imefungua Wilaya za Misungwi, Kwimba na Magu. Tuangalie barabara ya Mwabuu – Kijojia ambayo inakwenda mpaka Malampaka utakuwa umefungua Wilaya za Kwimba, Misungwi na Wilaya ya Malampaka, utakuwa umefungua Wilaya tatu ambao watakuwa wanawasiliana katika biashara zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba tujaribu kuangalia suala la usalama wa wavuvi wadogo. Mkoa wa Mwanza umezungukwa na Ziwa Victoria kuna Wilaya ya Ukerewe, Magu na Sengerema kama tutaweka nyanja nzuri za kuweza kuwalinda hawa wavuvi basi tutakuwa na uhakika wa kwamba watafanyakazi zao vizuri za kuinua uchumi wao kwa usalama zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine kama kweli tunataka kufanikiwa hii mipango ambayo imeletwa na Waziri wa Mipango, wachimbaji madini wadogo wadogo kule Geita na Sengerema ukiwakuta kwa kweli nyenzo za kuchimbia dhahabu zao ni ndogo sisi tunaita magalashi. Kwa nini basi Wizara isije na mikakati ya kuhakikisha kwamba inaleta nyenzo za kuwasaidia hawa wakulima wadogo wadogo badala ya kusema kwamba iwakopeshe fedha? Kwa hiyo, basi tunaomba watuletee vifaa ambavyo vinaweza kuwasaidia wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kwimba na wilaya ya Ukerewe tulikuwa tunalalamika juu ya umeme na bahati nzuri Serikali yetu ambayo ni sikivu imeweza kuleta umeme kwenye Wilaya ya Ukerewe. Ninaomba kupitia Bunge lako tukufu hili wawezekezaji wote wanaokuja katika maeneo ya Dar es Salaam wahamie Wilaya ya Ukerewe kwa sababu kule sasa hivi tuna umeme na kule kuna matunda mengi sana yanadondoka chini hayana soko. (*Makofi*)

Naomba wawekezaji ambao wanaangalia Mikoa ya Kanda ya Pwani ebu sasa tujaribu kutoka nje na kuja hadi Ukerewe ili tugawane hiki kidogo ambacho tulichonacho basi waangalie maeneo mengine ya Kanda ya Ziwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili wanawake uwape haki na kwa kuwa wanawake ni waaminifu sana katika kurudi mikopo, nimuombe sasa Waziri wa Maendeleo ya Jamii na Watoto atapokuja kuleta bajeti yake atuonyesha wazi kweli kwamba wanawake wana imani ya kurudisha mikopo. Tunaomba tuongezewa fedha hiyo fedha ya milioni nne haitoshi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba kwa kuwa imepitwa na wakati hiyo milioni nne, iongezwe ifike milioni kumi. Kwa sababu wanawake ni waaminifu wataweza kurudisha hiyo mikopo tu hawana wasiwasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nihame kwa Wizara ya Mipango naomba nihamie Wizara ya Fedha. Kuna msemo unasema samaki mmoja akioza wote wameoza. Kuna sheria ambazo zilikuwa zimepitwa na wakati zinaletwa hapa tunazirekebisha.

Mimi naomba sana mtu mmoja hawezi kudhalilisha *TRA* ambayo sasa hivi imetunusuru katika kukusanya mapato yetu. Ndugu zangu mtu mmoja hawezi kutoa sifa zote wanazopata *TRA*. Nafikiri hili wamelipata na nitaomba sana sifa ya *TRA* iendelee kama kawaida kwa sababu wanafanya kazi vizuri sana katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ionekane kwamba hilo kwamba kama ni mtu mmoja basi *director* wa mamlaka atalishughulikia hilo. Sasa hivi bahati nzuri sana *TRA* wameelekeza na nguvu zao nyingi katika wenzetu wa Zanzibar. Tulikwenda Kamati ya Fedha na Uchumi, tumeangalia jengo jipya ambalo linatengenezwa la *TRA* huko Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nafikiri yote haya yataweza kufanikisha. Basi niwaombe ndugu zangu wa *TRA* muwe na moyo huo wa kuendelea kutusaidia ili kuhakikisha kwamba tunakusanya fedha zetu na sisi tusiwe tegemezi kwa kutegemea mapato ya kutoka nchi za nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, amegusia suala la soda. Ni kweli tunahitaji kodi, lakini ukiangalia Watanzania wengi walioko vijijini kinywaji cha soda ni wengi wanakitumia sana. Nakuomba Mheshimiwa Waziri, ingawaje tunahitaji kodi uliangalie wengi wanatumia soda angalau basi isipande. Lakini mambo ya bia na *whisky* wewe endelea tu hata ukipandisha sisi tuko tayari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie fedha za Mkoa wa Mwanza za maendeleo kupungua. Ninaomba leo mnithibitishie ni kigezo gani kimefanya bajeti ya nchi hii kupunguza toka asilimia 12 na kurudisha asilimia nne mkijua kwamba kule ni Kanda ya Ziwa, Mkoa wa Mwanza ni *Centre* ya Afrika Mashariki na inategemewa sana na Uganda na Kenya, mmetumia vigezo gani kuhakikisha kwamba mmetupunguzia fedha za maendeleo?

Mheshimiwa Spika, naomba nisiwe na fadhila kwa Rais wetu tuliwaomba Marais wote wawili wa Awamu ya Tatu na ya nne kwamba wanawake tuwe wengi humu ndani.

Rais wa Awamu ya Nne, ametudhihirishia kwamba amekubaliana na Rais wa Awamu ya Tatu kwa kutupa nafasi nyeti za maamuzi ndani ya Baraza la Mawaziri. Ametupa Mawaziri sita pamoja na Manaibu Waziri kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nazungumzia hili la kumpongeza Rais wetu lakini bado najaribu kuliangalia katika elimu ya Vyuo Vikuu, kama kweli tunataka kumwezesha mwanamke akitoka shule za sekondari aendelee mpaka Chuo Kikuu. Utaratibu wa kumfanya mtoto wa kike anapomaliza *form six* asiunganishe kwenda Chuo Kikuu akae mwaka mmoja ndiyo apata nafasi ya kuingia Chuo Kikuu, hatutafika mbali wanawake.

Mheshimiwa Spika, ninaomba hili Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, aliangalie kama mmeweza kweli kuchukua wanafunzi ambao wamepata *division* ya *form six* na *division four* mkawapa ualimu.

Je, aliyepata *form six division one* na aliyepata *division two* kwa nini basi msiwasiliane na Wizara ya Elimu mkawachukua moja kwa moja kuliko kumwacha mwanafunzi wa *form six* anapomaliza anakaa mwaka mzima nyumbani ambako kuna vishawishi vingi. Kishawishi kinachowafanya asifike Chuo Kikuu baada ya huo mwaka mmoja kama atakaa nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mfano kuna binti yuko pale kijiji cha Malya anatoka kwenye Tawi la Mwahalanga anaitwa Maondolo Zenga amemaliza *form six* mwaka 2005 hakupata nafasi na ana *division two* ya *point 10*. Sasa huyu binti amekaa mwaka mzima na mwaka huu nimejaribu hata kufika kwa Naibu Waziri kumwombea hatuna uhakika kama tena atapata nafasi ya kuingia Chuo Kikuu. Ni mtoto wa mkulima ambaye yuko vijijini kule.

Tutawasaidiaje wasichana wengine kama huyu ambao wako vijijini kule ili wapate nafasi ya moja kwa moja ili waweze kuingia katika Vyuo Vikuu. Ninaomba utaratibu huu ubadilike kama kweli tunataka tuje tupate nafasi ya kuwa na Mawaziri wengi ndani ya Baraza la Mawaziri ambao wamesoma waliopitia Vyuo Vikuu tuwashirikishe na watoto walioko vijijini ili waweze kusoma mpaka Chuo Kikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho Rais wa Awamu ya Tatu aliahidi kwamba Uwanja wa Taifa utajengwa na umejengwa kweli. Namshukuru sana. Lakini uwanja tumepata, Chuo cha Michezo cha Walimu ambacho ni cha Afrika kiko Kijiji cha Malya, Kijiji cha Malya pale hakina umeme.

Hivi unategemea nini uwanja ule mzuri utafundishwa na walimu gani ambao watatoka gizani? Ninaomba sasa Wizara ya Nishati na Madini wahakikishe kwamba Chuo cha Malya, umeme unapatikana ili uwanja utakapokamilika watoke walimu kwenye mwanga jamani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa na hayo machache nafikiri ujumbe umefika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba tena nirudie kukushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi basi nichukue nafasi kwa sababu dakika zangu hazijaisha nimkaribishe Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba, nimkaribishe katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nimtakie kila la kheri Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Baraza lake la Mawaziri, sisi tuko pamoja na ninyi ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Serikali ambayo inawajali wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia, Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia machache katika Bajeti hii ya mwaka 2006/2007. Nipende kuwapongeza vile vile Waheshimiwa Mawaziri wote wawili ambao wametoa Bajeti zao kwa ufasaha kabisa. Kila Mtanzania aliyefanikiwa kusoma na kusikiliza ameielewa vizuri na ninafikiri kila mmoja atakubaliana na mimi kwamba ni Bajeti ambayo kwa kweli imejali mambo mengi. Ni pamoja na kujibu hoja na haja za madhara mbalimbali ambayo yametupata hivi karibuni. *(Makofi)*

Lakini vile vile ukiangalia Bajeti hii kwa mara ya kwanza ni Bajeti labda nikimkariri juzi Bwana John Hendra tulikuwa tunazungumza na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ni Bajeti ya kijani. *It is a green budget* ambayo imejali sana masuala ya mazingira na napongeza sana. Lakini vile vile ni Bajeti ambayo imejali jinsia na naomba nieleweke nikisema jinsia hapa ni *both* wanawake na wanaume, si wanawake peke yao. Imejali makundi hayo yote mawili na baadhi ya mambo nitayataja hapo baadaye. Naomba nimpongeze sana kaka yangu Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba, kwa kutuunga mkono hapa Bungeni. Tunamkaribisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipende kuangalia moja kwa moja Sheria ya ushuru wa bidhaa. Naomba nishukuru sana Serikali kwa kuweza kuchukua hatua ya kuongeza au kupunguza ushuru katika baadhi ya maeneo. Moja ya eneo ambalo mimi limenigusa ni hili la kupunguza ushuru katika bidhaa ya mafuta ya taa, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Wanawake tumefurahishwa lakini pia na wananchi wote wamefurahishwa kwa ujumla. Pamoja na kwamba hili lina sura ya kulinda mazingira. Lakini pia sisi kama wanawake au wanawake kwa ujumla limewapa furaha kubwa kwa sababu litawaondolea ile adha ya kubeba kuni kichwani kila siku. Kama azma hii itatekelezwa vizuri haya mafuta ya taa yakasambaa mpaka vijijini kwa bei ndogo tunayoizungumzia kwa kweli wanawake watafurahi sana kwa sababu watayatumia.

Mheshimiwa Spika, lakini ombi langu ni kwa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, ijaribu kuhamasisha *SIDO,* waweze kutengeneza majiko rahisi yanayotumia mafuta ya taa yaweze kusambaa sana katika vijiji hapo ndipo tutaweza kuwaona wanawake wakiyatumia majiko pamoja na mafuta ya taa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba vile vile katika nyongeza za ushuru Waziri ajaribu kuongeza ushuru katika magunia ya *jute.* Hapa nchini tunaingiza magunia ya *jute* mengi sana yako katika masoko yetu na yanatoka mengi sana huko Bangladesh yako hapa nchini. Lakini wakati huo huo sisi wenyewe tuna viwanda ambavyo ni vya magunia huko Moshi na Morogoro labda na mahali pengine ambavyo viko *idle* mpaka sasa havifanyi kazi. Kwa nini, ni kwa sababu haya magunia ya nje yanayokuja ni ya bei rahisi. Kwa hiyo, tunayakimbilia, tunayanunua hayo kwa wingi. Lakini magunia yetu ambayo yangetengenezwa hapa nchini kwa katani yetu hatuyapati.

Kwa hiyo, naomba sana ushuru upandishwe ili uingizaji wake uwe wa kiasi. Hivi sasa tunayo katani ya kutosha kabisa. Kwa mfano, katika kipindi hiki hivi sasa tunazalisha tani 27,793 za katani na ifikapo mwaka 2016 tutafikia kuzalisha katani tani laki mbili. Tutafanya nayo nini? Si tuitumie katika viwanda vyetu. Sasa Watanzania tunakimbilia magunia ambayo yanaingizwa nchini. Tukihamasisha viwanda vikaweza kuzalisha basi ndiyo ajira tumeshaiongeza kama Mheshimiwa Rais alivyodhamiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile naomba tuongeze ushuru katika magunia yanayoitwa ya sandarusi. Magunia ya sandarusi pamoja na kwamba ni rahisi sana na Watanzania wengi wanaweza ku-*afford* kuyanunua lakini hayaozi. Ukiyatupa hayaozi, kwa hiyo, hayako *friendly* kwa mazingira. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha hili pia uweze kuliangalia. *(Makofi)*

Naomba vile vile niipongeze Serikali kwa kuiongezea sekta ya kilimo fedha nyingi kuliko miaka mingine yote. Nashukuru sana, lakini usambazaji wa fedha hii kwenye Wizara mbalimbali mimi napata tatizo kidogo, kwa sababu udhibiti wake sijui Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, anafanyaje. Udhibiti wake na usimamizi wake kuhakikisha kwamba fedha ile imetumika kwa makusudi yaliyopangwa. Sidhani kama ni rahisi.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mmoja mdogo, mwaka 2004/2005 kulitolewa fedha za *STABEX* kwa ajili ya kukarabati barabara za kahawa. Fedha hiyo ikapelekwa miundombinu. Wakati ule Wizara ya Ujenzi. Sasa wenzetu wa Wizara ya Ujenzi bila ushirikishwaji mkubwa na wadau wengine, Mikoa au Wizara nyingine, wakatengeneza barabara iendayo kwenye kilimo cha mahindi. Sasa hapo maana yake nini. Wakati tunataka kuboresha zao la kahawa ambalo linatuletea uchumi mkubwa hapa nchini lakini barabara hiyo iliyojengwa imeenda kwenye mahindi.

Hiyo ni *contradition* ambayo kwa kweli lazima tuirekebishe. Kwa nini Serikali isiliangalie upya suala hili ili kwamba Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, iwe na *say* zaidi kuhusu hii fedha ambayo inatolewa na Serikali kwa dhamira nzuri kabisa badala ya kuipeleka mara *TANROADS* mara TAMISEMI, *okay!* Ni sawa inaweza ikaenda TAMISEMI kwa sababu wao wanaoshughulika wananchi moja kwa moja, lakini vile vile ukizidi kuwaongezea fedha nyingine nyingi zaidi wanaweza wakapata taabu zaidi kidogo.

Mheshimiwa Spika, nimeliangalia suala la ugani, yapo matatizo ya ugani tumekuwa tukiyazungumzia katika awamu zote nne za utawala, kuna matatizo makubwa sana ya *Extension Staff,* hawaendi kabisa vijijini pamoja na maneno makali tunayoyatoa viongozi wa Serikali, Wabunge kwamba ugani waende vijijini wakasaidie wakulima, hawaendi. Wamekaa tu maofisini au hata huko vijijini wamekaa tu, wamekaa kiasi ambacho wakati mwingine wanatia aibu. Utaenda kuangalia shamba la mtu wa *Extension* ni chafu kama shamba la mkulima wa kawaida.

Sasa hii faida ya *extension* ni nini. Kuna haja ya Serikali kwenda kwa undani zaidi kuangalia, tatizo ni nini, badala ya maamuzi ya juu juu tukatoa maagizo nenda mfanye kazi, nenda vijijini mfanye hivi mfanye hivi. Pengine kuna sababu za msingi ambazo sisi hatujaweza kuzifahamu.

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze sana Serikali kwa jinsi ambavyo imeshughulikia suala la njaa mwaka huu, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa halali usingizi amefanya kazi kufa na kupona kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania hawaathiriki kwa njaa. Hilo ni jambo zuri sana na ni sifa kubwa sana kwa Serikali. Sasa tumejielekeza katika mikakati mbalimbali. Lakini juzi kama nilivyochangia kwenye semina, jibu ni umwagiliaji tu, kama wazungumzaji wengine walivyosema. Umwagiliaji mkubwa ni muhimu, siyo wa ekari 3, ekari 4, ekari 5, hapana, uwe umwagiliaji mkubwa wa ekari nyingi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana hapa Bungeni nakumbuka tulitenga fedha kama shilingi bilioni 8. Naomba kiasi hicho mwaka huu kiongezwe badala ya kupunguzwa. Kiwango cha fedha kwa umwagiliaji naomba kiongezwe siyo kupunguzwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru sana Serikali kwa kuwaangalia watumishi wa Serikali kwa kuwaongezea mishahara, hongera sana. Tumeambiwa kwamba Mheshimiwa Hawa Ghasia, atakaposimama atatufafanulia vizuri. Lakini pamoja na kwamba kundi hili ninalojitaja sasa hivi siyo wafanyakazi yaani *pensioners.* Naomba kila tunapowaongezea watumishi mishahara, tuwaangalie *pensioners* vile vile jamani walau hata kwa asilimia mbili mbili tu. Kwa sababu hawa watu wamefanya kazi nzuri sana kama ambavyo baadhi yetu hapa tunaelekea huko. Mkisimama hapa bila kusemea pensheni mnajizika wenyewe. Hili suala lazima muangalie kwa uzito. *Pensioners* ni watu muhimu sana ndiyo sisi tunaoelekea huko baadhi yetu bado wengine tayari. Lakini ni muhimu sana tujielekeze katika kuwatetea hawa watu ambao waliijenga nchi hii kwa juhudi kubwa sana.

Mwisho kabisa natoa wito kwa Watanzania ili kuboresha uchumi wa nchi hii, tubadilike tufanye kazi jamani mpaka leo hivi kuna watu ambao tangu asubuhi kazi yao wanashinda kwa bao tu. Bao, bao, bao, hivi mpaka lini. Kama ni mila basi tuziondoe hizo mila za bao. Tujenge tabia ambayo itatupeleka mbele. Kuna watu ambao nchi hii analima hatua 50 anajisifu mbele ya wanaume wenzie anasema nina shamba kubwa. Kweli shamba kubwa hatua 50. Hatua 100 unapita mitaani unasema mimi nina shamba. Si kweli hata kidogo.

Naomba tushirikiane Serikali, Wabunge tukemee hilo watu wafanye kazi, tusitazamie Serikali peke yake iweze kutukwamua Watanzania hapana na si vema hata kidogo Serikali kila siku iwe inalala kuota wananchi watakula nini, eti kwa sababu kuna watu ambao kazi yao ni kulima hatua 50 wakalala usingizi, haa! Hii haitatufikisha mahali popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi nzuri uliyonipa, mambo ni mengi ambayo ningezungumza hapa lakini bahati nzuri kuna Wizara ambazo zinahusika

baadaye vile vile bila shaka utatupatia nafasi tuweze kufafanua mambo vizuri zaidi kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi na naunga mkono Bajeti zote mbili asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa fursa hii ya mimi kuchangia hoja hizi mbili za Mipango na Fedha.

Ningependa kuchukua fursa hii kuwapongeza sana Mawaziri hawa, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na wataalam wao wote kwa kazi nzuri ambayo wamefanya. Hotuba zao ni nzuri zinaelezea hali nzuri na kweli wanastahili pongezi maalumu kwa kuzingatia kwamba kipindi kilichopita uchumi wetu ulikabiliwa na matatizo makubwa ya ukame, ya upungufu wa umeme na upandaji bei mafuta. Lakini waliweza kushikilia na kuuendeleza uchumi bila kuyumba na sasa hivi kuleta mapendekezo mazuri ya kuvuka katika hali hiyo ngumu na kwenda mbele zaidi.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea na mchango huu, naomba uniruhusu nizungumze suala moja la msingi kidogo. Inaelekea baadhi ya Wabunge hawapendezwi au wananuna pale tunapozungumza kwamba mambo haya au mipango hii na Bajeti hii inaongozwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Hili ni jambo la msingi na ni vizuri likaeleweka vyema kwamba mwaka jana vyama vyote vilipata fursa ya kunadi Ilani zao na hii ndio kawaida inafanyika katika demokrasia yoyote na katika demokrasia chama kinachoshinda, ilani ya chama tawala ndiyo inayotumika kama sera kama miongozo ya kufuatwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tusiwe na wasiwasi tunaposema Ilani ya Uchaguzi ya CCM, kweli tuna dira, kweli kuna *plans* na hizi nyingine hizi lakini hizo ni za muda mrefu. Kipindi cha miaka mitano hiki kinaongozwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM na tunaomba ndugu zetu ambao pengine hawapendi hiyo walielewe watusamehe na hiyo ndiyo hali halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchaguzi ulifanyika, wananchi wakatoa ushindi wa kishindo kwa CCM ikionyesha kwamba hii ni ridhaa kubwa waliotoa kwa CCM na Ilani ya Uchaguzi inakuwa ni kama mkataba baina ya Chama cha Mapinduzi na Serikali kwa upande mmoja na wananchi kwa upande mwingine, hivyo Chama cha Mapinduzi na Serikali zake haina budi kutekeleza haya kwa uadilifu kama dhima kwa wananchi katika kutekeleza ahadi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kueleza kwamba kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 mambo makuu mawili, kwanza ni kujenga uchumi wa kisasa, uchumi unaoendelea kwa kasi kubwa, endelevu. Uchumi ambao utatutoa katika hali ya umaskini na kulifanya taifa letu liwe katika uchumi wa hali ya kati. Pili, ni kuwawezesha wananchi kiuchumi ili waweze kumiliki na kuuendesha uchumi wao. Hotuba hizi za Mawaziri zimejielekeza huko. Ni jitihada kubwa iliyofanywa katika kufanya hayo. Nashukuru kwamba mengi wamefanya kwa nia nzuri na mengi yameanza kufanikiwa.

Hata hivyo, bado kuna maeneo ambayo inabidi tuyatazame kwa uangalifu sana. Moja ya sehemu kubwa ambayo yanatia matatizo makubwa au mashaka makubwa ni kwamba ukuaji wa Pato la Taifa umeongezeka kidogo kwa sababu zilizoelezwa na vile vile kwa upande mwingine ukuaji wa mfumuko wa bei umeongezeka. Pato la Taifa limepungua, mfumuko wa bei umeongezeka kitu ambacho kinaashiria hatari huko mbele na vile vile ukizingatia kwamba urari wa malipo ya nje vile vile umezidi kupanuka dhidi yetu.

Kwa hiyo, hali hiyo inahitaji na inaleta changamoto kubwa kwa sisi kuongeza uzalishaji, uzalishaji katika sekta mbalimbali katika maeneo mbalimbali. Kwa nidhamu zaidi, kwa ari kubwa, nguvu kubwa zaidi na kasi kubwa zaidi. Hayo ndiyo yanafanyika. Nilisema kwamba katika Ilani ya Uchaguzi inaelezea kwamba ifikapo mwaka 2010 matarajio yalikuwa kwamba uchumi uwe umekua mpaka asilimia 10 hadi asilimia 11 kwa wastani kutoka asilimia 6.7 ilivyokuwa mwaka 2004. Sasa hilo kama tulivyosema limetetereka kidogo na sababu zimeelezwa na matumaini tuliambiwa kwamba tutaweza kuvuka mbele na kwenda huko mbele. Kwa hiyo, tuwe makini katika maeneo yetu mbalimbali . Sasa hayo yanahitaji uangalifu kama nilivyoeleza kwamba tuwe makini katika maeneo yetu mbalimbali.

Sasa eneo moja ambalo limewekewa mkazo ni hili la uwezeshaji wananchi. Uwezeshaji wananchi kidogo umekuwa na matatizo. Wabunge wakisaidiana na viongozi wengine tumehamasisha sana wananchi. Wananchi wamehamasika, wamepata ari mpya, tumetumia nguvu mpya ili kuweza kupata kasi mpya ya maendeleo. Lakini jambo moja ni kwamba hii mipango mbalimbali tuliyonayo MKUKUTA, MKURABITA, *SELF*, *TASAF* na mengine yote baadhi imefanya kazi inayoeleweka. Lakini mingi bado haijaeleweka.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri katika hotuba zao hizi imeelezwa kwamba jitihada zinafanywa haya yakamilishwe. Mimi ningependa kupendekeza kwamba ni vizuri yakikamilishwa kwa haraka zaidi. Kwa sababu wananchi wengi wanakata tamaa kwamba jitihada zao wanazofanya ya kujiunga katika vikundi vya uzalishaji, wanajiunga katika *SACCOS* na vyombo vingine vya ushirika, lakini hawapati fedha au mikopo inayotakiwa na baadhi yetu tumewahi kwenda katika benki mbalimbali na Taasisi mbalimbali lakini inaonekana bado hawa hawajapata mwamko kwamba katika hali ya sasa ambayo inataka kasi mpya, taratibu na masharti yanalegezwa. Lakini wao wanasema bado hayajalegezwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, MKURABITA utatekelezwa kama vile ambavyo benki zinafanya kwa kawaida. Nafikiri kwa suala hilo ni vizuri kwa Serikali ikachukua hatua thabiti ya kushauriana na hawa wenye benki na wenye taasisi zingine za mikopo midogo midogo ili kuwapatia wananchi fursa. *(Makofi)*

Kwa upande wa uzalishaji mkubwa shughuli za kilimo na shughuli za kiwanda ni vigumu sana kuweza kuendeshwa kwa utaratibu wa mikopo ya muda mfupi wenye riba kubwa. Nimefurahi kusikia kwamba *TIB* kugeuzwa kuwa Benki ya Maendeleo. Ni vizuri

shughuli hii ikafanywa haraka iwezekanavyo na mtaji uliotajwa nafikiri ni mdogo kidogo. Kuna haja ya kuweza kufikiria kuongeza kwa sababu shughuli hizi ni pana na mahitaji makubwa zaidi. Kwa hiyo, labda kama ni milioni 100 hivi ndiyo ingefaa kwa shughuli hii.

Mheshimiwa Spika, tukija upande mwingine ufahamu na elimu ni suala ambalo linahitaji mkazo mkubwa sana. Hii mipango yote na programu zote zitaishia hivi hivi endapo wananchi hawatapewa elimu ya ufahamu. Kwa hiyo, nasisitiza kwamba maafisa mbalimbali wa maendeleo ya jamii, wa ushirika, watumike kwa nguvu zaidi katika kuelimisha wananchi juu ya masuala haya mbalimbali ili waelewe, ili washughulikiwe vizuri. Pamoja na hilo kuna suala ambalo linawakabili wananchi wengi kwamba wengi wanatakiwa waandae mipango yao rasmi pamoja na michanganuo. Lakini hawana utaalamu wa michanganuo. Kwa hiyo, suala hili lifikiriwe ni namna gani tunaweza kutoa msaada kwa wananchi katika sehemu mbalimbali ili waandae michanganuo na kuweza kupata mikopo hii kwa masharti nafuu. *(Makofi)*

Suala lingine limeelezwa mara nyingi na Waheshimiwa Wabunge waliopita ni suala la ugani. Hawa maafisa ugani ni watu ambao kusema kweli hawatekelezi wajibu wao kama inavyostahili. Serikali inabidi kuweka mkazo zaidi katika kuwakazania hawa maafisa ugani watoe huduma na maendeleo yanayotakiwa. Suala kuu ambalo limeletwa katika suala hili ni utumiaji wa teknolojia za kisasa. Jembe letu hili la mkono ilani inatambua kwamba haliwezi kutufikisha mbali ni suala ambalo tunatarajia kusema kweli lifanywe kwa haraka zaidi.

Nimefarijika kupata taarifa jana kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu alikwishachukua hatua za kuzungumza na baadhi ya mabalozi ili tuweze kupata matrekta zaidi ya laki moja na zaidi ya hapo ili yatusaidie katika shughuli zetu hizi. Nafikiri huu ni mwelekeo sahihi na nalitilia mkazo kwamba hili lihimizwe zaidi. Bila hivyo hatuwezi kwenda popote. *(Makofi)*

Sasa katika mambo mengine ya uwezeshaji kuna suala linaloitwa mifuko ya pembejeo na mengineyo. Hili utaratibu wake kusema kweli hauko wazi sana. Na ni vizuri suala hili likawekwa vizuri katika maeneo mbalimbali ili wote waweze kufaidika kadri inavyostahili. Sasa tukiacha hilo, suala lingine la uwezeshaji ni suala la nishati. Nishati kwenye kilimo, nishati kwenye viwanda. Katika Ilani ya Uchaguzi yamezungumzwa mambo mengi, makubwa na mazito ya kutukwamua kutokana na matatizo yetu ya umeme tuliyonayo hivi sasa ya nishati.

*Stiglers Gorge* imetajwa, mkaa wa Mchuchuma umetajwa. Sasa hivi nafikiri tumepiga hatua mbele ya kusogea katika miaka mitano hii inayokuja ambayo mnatakiwa mambo haya yawe mmetekeleza. Ni jambo la kushangaza sana kwamba katika mpango huu na katika bajeti hii hamna maelezo ya kuonyesha kwamba tutaanza lolote angalau katika kuendeleza nishati kutoka *Stiglers Gorge* au mkaa wa Mchuchuma.

Sasa hilo ni suala ambalo ningeomba Mawaziri na Serikali ilifikirie kwa sababu siyo tu ni *commitment* ya Ilani ya Uchaguzi lakini viwanda vyetu na shughuli zingine za uzalishaji na zingine za biashara tunapata shida sana kwa sababu ya ukosefu wa umeme

na ughali wa umeme. Unaongezea sana gharama bidhaa zetu na kufanya uchumi wetu usiweze kuwa mshindani katika soko la ndani na soko la dunia. *(Makofi)*

Maji halikadhalika, ni kwamba maji sisi katika Kamati ya Uwezeshaji na Biashara, tumetembelea viwanda vingi na moja ya tatizo kubwa linalowakabili wazalishaji, kwa mfano kiwanda cha bia ambacho kinaleta fedha nyingi sana kwa Taifa, mapato mengi sana kwa Serikali, wawekezaji wake, malighafi yake kubwa ni maji. Lakini kiwanda muhimu kama hiki nacho kina matatizo ya maji na viko viwanda vingine vingi sana. Sasa ukiacha tatizo la maji kwamba linawasibu wananchi wote nchini kote. Lakini tatizo hili linakuwa ni hatari zaidi pale linapoathiri viwanda na shughuli za uzalishaji. Nashauri kwamba Serikali iliwekee mkazo suala hili hasa katika kupatiwa maji na vigezo vingine kwa viwanda muhimu kama vile vya bia na vinginevyo.

Suala lingine ambalo linakwamisha jitihada zetu za uzalishaji ni upatikanaji wa malighafi. Nchi yetu ina malighafi nyingi lakini bahati mbaya hatujaweza kujipanga na kujiweka vizuri kuweza kupata malighafi hiyo. Kuna viwanda kwa mfano vya mafuta, mpaka sasa vinaagiza mafuta kutoka Malaysia ambapo nchi yetu hii ina uwezo mkubwa sana wa kuzalisha mawese, njugu, ufuta, ili mradi tunajipanga vizuri katika sehemu mbalimbali inazotoa na hivyo tukapunguza utegemezi wetu katika kuagiza mafuta kutoka Malaysia na kutuletea sisi, sasa hii ni habari ya kujipanga kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo, kuna kiwanda mfano cha kutengeneza mipira cha *General Tyres.* Muheza, Kilombero na Zanzibar tunazalisha sisi mpira, lakini kwa sababu hatujachukua hatua thabiti ya kuendeleza inabidi sasa *General Tyre* waagize malighafi kwa bei ghali sana kutoka nje na sisi humu ndani tuna uwezo wa kutengeneza mipira yenye malighafi mzuri zaidi kuliko ile inayotoka nje. Haya ni mambo ya kujipanga. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nashauri kwamba suala hili tulitazame ili tuweze kujitegemea vizuri zaidi humu ndani ili tupunguze utegemezi wa kutoka nje ambao tunaweza kuupata humu ndani. Nikimaliza hapo napenda niongeze kwamba kuna masuala mengine ya uwezeshaji ambayo yanatokana na utendaji mbaya. Tumesema kwamba azma kubwa ya kuendeleza uchumi wetu kwamba uchumi ukue lakini papo hapo uwawezeshe wananchi wamiliki na kuuendesha uchumi wao.

Mheshimiwa Spika, lakini katika kutembelea baadhi ya viwanda tumegundua kwamba wananchi kwa sababu zisizoeleweka wengine wanakwamishwa sana bila sababu. Ushahidi mmoja, ni kiwanda kimoja cha kutengeneza sigara kinaitwa *Masters.* Hawa wametueleza kwamba wanakwamishwa karibu na kila taasisi katika utengenezaji wao na uendelezaji wa kiwanda hicho. Sasa hatujui ni kwa sababu ya kisheria au ni kwa sababu za kitaalam. Nafikiri Wizara ya Viwanda pamoja na Tume inayoshughulikia masuala ya *Fair Trade Practice* walitazame kwa undani suala hili. Nini kinafanyika, hii inakatisha tamaa, hawa nimewataja kama mfano tu. Lakini wananchi wengi sana wanakomeshwa siyo tu katika kupata mikopo siyo tu katika kupata misaada na vitu mbalimbali. Haya ni masuala ambayo sisi wenyewe tulikwamishwa kutopata kasi ile ya maendeleo inayotakiwa. *(Makofi)*

Baada ya hapo, ninashukuru nimesema kwamba tufanye jitihada ya kuongeza mazao. Nashukuru kwamba Halmashauri za Wilaya zinajitahidi sasa hivi zinapata uelewa na mambo makubwa ya maboresho kujihusisha zaidi katika masuala ya uzalishaji zaidi ya yale ya kukusanya kodi na utawala. Lakini hivi karibuni napenda kushukuru kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu aliitisha kikao cha wadau wa mazao makuu yote, tukazungumza kinagaubaga pale masuala gani yanahusika, malengo yetu ni yapi, wakati gani yafanyike.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri nafikiri katika masuala yetu haya tukafanya vikao kama hivi katika ngazi zote kwa mazao yote, kwa bidhaa zote ili kwamba mipango iwe inahusisha mipango iliyojumuishwa kutoka chini kwenda juu tunagawana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, napenda na mimi niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa ushindi alioupata. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu. Lakini niwapongeze hawa wawili kwa kasi ambayo wameianza mpaka sasa hivi *speed* ipo vile vile na inaongezeka na napenda niwapongeze sana. *(Makofi)*

Napenda nikupongeze na wewe kwa *standards* zako na *speed* zako tumeanza kuona Wabunge. Lakini kikubwa zaidi ni kwamba uko karibu sana na wapiga kura wako ambao ni wapigakura na bila shaka hata Urambo huko vile vile unaishi kama unavyoishi hapa. Napenda nikupongeze sana.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze lakini pia na Waheshimiwa Wabunge ambao tumejaliwa kurudi Bungeni. Safari hii uchaguzi ulikuwa mgumu sana kama unavyofahamu kufuatana na sheria yetu ya Uchaguzi ya mwaka 1985 baada ya mwenzetu alikuwa katika kugombea Umakamu wa Rais sikumbuki chama, CHADEMA nadhani kufariki dunia. Kwa hiyo, uchaguzi ukaendelea kwa miezi minne na nusu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wapiga kura wetu walichoka, wagombea walichoka na vyama vilichoka. Niombe hapa sasa Waziri anayehusika na Sheria hiyo alete Muswada haraka ili sheria hiyo ifanyiwe marekebisho kabla ya uchaguzi mwaka 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema wazi kuwapongeza Wabunge kwa sababu ilikuwa kazi ngumu na wengi hawakurudi hapa. Mimi nafananisha na kwenye Biblia wamesema Wayahudi wakati wanatoka Misri kwenda Yerusalemu nchi waliyoahidiwa, sasa wengi walitarajia kuona Yerusalemu mpya iliyojengwa kwa mawe lakini wengi hawakufika, waliona tu lakini hawakufika. Bunge lililopita jengo hili lilikuwa likijengwa tukiangalia kama Yerusalemu wengi hawakufika, hawakuona Yerusalemu mpya, sisi tumshukuru Mungu na tufanye kazi sasa kwa matakwa ya watu ambao wametuleta hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo historia ya nchi yetu kisiasa, kiuchumi unavyowafahamu na kijamii lakini nitasema kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, wakati wakoloni wanakuja nchi yetu, dunia ilikuwa imeshapitia hatua mbalimbali za maendeleo kutoka ujima, utumwa, kilimo na maendeleo ya viwanda. Sasa walipokuja huku wakaamua wao wakaturudisha kwenye kilimo na kwa Tanganyika wakati ule walisema kuna zao la mkonge pamoja na zao la kahawa, kwa hiyo, wakachagua maeneo hayo na kuwahudumia kwa maana ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa bahati nzuri baada ya Uhuru Serikali zilizokuja hasa awamu ya tatu na ya nne hilo wameliona kwamba sababu za kuweka miundombinu sehemu moja hazipo, zipo sasa kwa sababu ya mahitaji ya uchumi wa dunia ya leo, kuna sababu za kufumua uchumi wa nchi nzima na ndio maana ipo mipango ya *Mtwara Corridor*, *Central Corridor*, barabara za kutoka Tunduma kwenda Sumbawanga, Kigoma iko kwenye programu, barabara ya kutoka Nakanyazi kwenda Kigoma iko kwenye programu, barabara ya kutoka Mbeya kuja Dodoma, ipo na sehemu zingine za nchi, daraja la Mkapa limejengwa. Kwa hiyo, nasema Bajeti za sasa hivi Serikali ya sasa hivi zimeliona hilo na zinataka kufumua uchumi hasa wa nchi za Magharibi.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba hapa kitu kimoja, kwamba tuna uchumi mkubwa sana umetuzunguka Magharibi mwa nchi, kwa maana nchi za Burundi, Kongo na Rwanda. Lakini kwa hali ya miundombinu iliyopo hatuwezi kufanya chochote, inabidi sasa mipango ambayo ipo hiyo iharakishe, Kongo peke yake ina mizigo zaidi ya tani 70 milioni kwa mwaka na sisi kama hatuwezi kulijua wakajua wenzetu ambao sitaki kuwataja na wenzetu wana uwezo zaidi kiuchumi wakilijua watafanya haraka haraka wakatuwahi. Kwa hiyo, ni vizuri na sisi tukawahi hayo.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunashukuru Bajeti zetu zina mtazamo wake wa kuangalia maeneo yote ambayo yako nyuma kidogo. Kwa maana hiyo Bajeti inafuata *population*, idadi ya watu katika maeneo husika, hilo tunashukuru sana, tunasema hivi kwa sababu yako maeneo kwa mfano kwangu Geita kule kuna maeneo ambayo wanalima pamba, kuna maeneo ambayo yana mifugo, kuna maeneo ambayo yana samaki lakini barabara vijijini hakuna na sehemu nyingi tu na kwa sababu hiyo wapiga kura wetu wanadhani sisi Wabunge hayo hatuyasemi hapa Bungeni. Tunasema sana Waheshimiwa wapiga kura mnasikiliza, tunaomba sana hizo barabara zijengwe kwenye maswali ya nyongeza kwenye kuchangia kama hivi na Serikali sasa tunaomba sasa nayo isikie hizo barabara ambazo tunaziomba za vijijini za kusomba pamba, za kusomba mpunga, za kusomba mbao na hasa minofu ya samaki, zitengewe fedha ya kutosha ili wote tuchangie sawa kwenye uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa wapiga kura wetu, kuna wakati wanafikiri kwamba sisi hatufanyi kazi na matokeo yake hasira zao wanaonyesha kwenye uchaguzi. Nilikuwa naangalia takwimu mwaka 2000 kwenda 2005 kuna baadhi, nitoe takwimu kidogo tu kwa sababu ambazo nazisema au nyingine Mkoa wa Mara, Wabunge walikuwa nane wamerudi watatu, mkoa wa Kigoma walikuwa Wabunge nane mwaka 2005 amerudi

mmoja, mkoa wa Ruvuma walikuwa saba amerudi mmoja, mkoa wa Shinyanga walikuwa kumi na mbili wote hawakuona Yerusalemu, *zero. (Makofi/Kicheko)*

Sasa wapiga kura wetu wanadhani kwamba sisi hatufanyi kazi hapa tunaomba chonde chonde wapiga kura tunasema ila sasa Serikali nayo jamani isikie, Serikali huko mchezo huu ni mauti kwetu, tunaomba sana wapiga kura msikilize haya, hilo moja.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka kusema Wilaya ya Geita, sisi tuko watu laki nane, tunakaribia laki nane au tunazidi kidogo. Lakini mfumuko huu wa watu umetokana na kuwepo kwa migodi ya dhahabu pamoja na shughuli zile za kiuchumi. Sasa lakini huduma za jamii athari zake ni kwenye huduma ya jamii, hospitali ya Geita imejengwa mwaka 1956 na wakati huo idadi ya watu ilikuwa kama takribani watu 30,000 leo kuna watu laki nane. Sasa bahati nzuri Halmashauri napenda niipongeze Wilaya ya Geita imeamua kuzipandisha hadhi vituo vya afya vya Kharumwa, pamoja na Nzera na kituo cha afya cha Kharumwa kwa sababu Halmashauri nasema niipongeze, imepeleka vijana wachapakazi wazuri, ma-*nurse*, waganga kituo hicho hicho kinahudumia Wilaya za Shinyanga Vijijini na Kahama na sehemu zingine kama Nzega na Wilaya yenyewe sehemu ya Wilaya.

Kwa hiyo, pale unakuta msongamano wa watu ni mkubwa sana kwenye hospitali, kituo cha afya cha Kharumwa na hawa waganga napenda niwapongeze hususan daktari kiongozi pale anaitwa Dr. Mgema na wenzake wanafanyakazi Jumapili, wanafanya *weekend*, wanafanyakazi siku za sikukuu, wanafanyakazi hata usiku na hawachoki, daktari anaingia anafanya *operation* hata nne, tano kwa siku na matokeo yake ndio watu wanakusanyika, dawa hazitoshi.

Kwanza naiomba Halmashauri, Mganga Mkuu wa Wilaya kama ananisikiliza hii timu ambayo ameipeleka kwenye kituo cha afya asiibughudhi, waache wafanye kazi nzuri na kama wananchi ndio wanataka hivyo wa huko na mimi kama Mbunge nasema hilo, kwa hiyo lakini tuombe kwamba aongeze madaktari wengine. Lakini pia tunaomba vituo hivyo Nzera na Msalala vipewe magari ya wagonjwa ili kuweza kuokoa vifo vinavyotokea mara baada ya vituo hivyo kutoa rufaa kwa wagonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maji katika Mji wa Geita ni tatizo kubwa sana, kuna takribani watu laki moja wako pale na bahati mbaya sana kuna mgodi karibu wa *GGM*. Pale mgodini wakati wa masika maji huwa wanashindwa wafanyaje, kuna ambayo wanatoa Ziwani ya bomba na kuna mengine yapo ya mvua kwenye Mito pale yanawasumbua wafanyaje, lakini wakati yanatokea hayo pale Geita Mjini ndoo moja au lita ishirini inanunuliwa kwa shilingi 150 hadi 200 na ni maji ambayo sio salama ya visima vifupi na magonjwa kama *typhoid* ni kawaida kabisa pale kwa hiyo, tunaomba sana Serikali chonde chonde mnafahamu tuleteeni maji Geita watu wanakufa kwa *typhoid amoeba* tunaomba sana hilo.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la umeme vijijini, Serikali ilitoa umeme kutoka Ibadakuri, Shinyanga kupeleka pale mgodini *KMCL* na ahadi zilikuwa zimetolewa kwamba vijiji ambavyo umeme unapita watapewa umeme, lakini pale Kharumwa kijiji

cha Kharumwa kimepitiwa na umeme huo hawakupewa na tumeomba sana hapa lakini hatujapata jibu la uhakika. Umeme huo sasa unatoka tena *Kahama Mine* kwenda kwenye chanzo cha maji kupeleka Shinyanga unapita palepale Kharumwa sasa Kharumwa iko kwenye herufi "V" ipo katikati bado hakuna mipango ya kupeleka pale umeme, naomba sana Waziri wa Nishati na Madini wakati ana *windup* hotuba yake aseme hili nalo kwamba Kharumwa na kuna watu zaidi 100 wako tayari kutumia umeme sio watumie umeme wa jenereta. Kwa hiyo, tunaomba umeme mji wa Kharumwa.

La pili ni simu, simu tunaomba minara ya simu ya *VODACOM* na *CELTEL* kule ukitaka kupiga simu inabidi uende kwenye mti, upande mti nadhani akina mama hilo hawawezi au uende kwenye kichuguu na hata kwenye makaburi. Mimi wakati wa uchaguzi usiku ndio ulikuwa unapatikana mtandao vizuri na sehemu nzuri ni makaburini, kwa hiyo, nikaonekana na piga simu pale kesho yake mji mzima, kijiji kizima kinasema Musalika alikuwa anawanga kwenye makaburi. Sasa tuleteeni mitandao ya simu waambieni makampuni watu wanahela kuna walimu, kuna wafanyabiashara, kuna wakulima wote wana hela, tuleteeni mitandao ya simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la migodi kutoa laki mbili kwa Halmashauri, hili limo kwenye mkataba na tumeshalisemea sana hapa Bungeni, tunashukuru kasi mpya Wizara ya Nishati na Madini imeufanyia kazi na sasa makampuni yameanza kutoa hizo hela. Lakini wameshatoa kuanzia mwaka huu, tunachoomba kwamba sheria ilikuwa wazi na wataalam jamani ninyi wenzetu kwa nini Halmashauri hamkuziambia juu ya hili, mnasema siri sasa siri imepita miaka sita, Halmashauri hazifahamu, kwa hiyo, tunaomba malimbikizo ya zile dola laki mbili kwa kila Halmashauri. Limo kwenye sheria na wenzetu wenye migodi mtuelewe ninyi haya tu yangefanywa kwenu kwenye nchi zenu mngefurahi Halmashauri zenu ninyi wenye migodi lipeni malimbikizo hayo laki mbili kwa muda wa miaka sita ili Halmashauri zetu mnaona hata hali zilivyo.

Mheshimiwa Spika, nimalizie suala la elimu, kwamba tuna maboma zaidi ya 885 ya madarasa hayajajengwa mpango wa MMEM Geita, maboma 219 hayajajengwa na wananchi waliombwa wajenge, wakajenga tunasubiri hayo, watatuuliza kwenye mikutano, tunaomba sana. *(Makofi)*

La pili, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, mnatuchanganya kwamba namna ya kujiunga na ualimu, mwaka 2003 mlisema kwamba wanafunzi watume maombi, mwaka 2004 Wizara inachagua yenyewe, mwaka 2005 jazeni *self form*, mwaka huu mkasema *self form*, jana Waziri amesema wanatangaza matangazo ya nafasi 10,000, chuo kinaanza mwezi wa saba, leo ni mwezi wa sita, kule kwangu hakuna gazeti, Kigoma Redio Tanzania haifiki, wanafunzi wapo hawajui cha kufanya, hebu jamani twendeni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, inalalamikiwa hili lirekebishe.

Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, najua ni mahili sana, tunamfahamu kutoka Chama cha Walimu hebu rekebisha hili, wanafunzi wetu wanatusumbua, Wabunge sisi ndio kila siku Wizarani kwenda kuomba nafasi za walimu na tunaposhindwa kufanya hivyo ndio huko huko mwaka 2010 wanashindwa kuturudisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBWACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na wewe pia nikupongeze kwanza kwa namna ambavyo unaifanya kazi yako ya Uspika kwa umahiri mkubwa sana na umahili huo unafanana sana kwa kweli na uwepo wetu wa sisi katika jengo hili jipya, zuri na lenye kupendeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa si mwenye fadhila kama sitapongeza namna ambavyo Serikali yetu inayoongozwa na Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa namna ambavyo inafanya kazi kwa *speed* na kwa umahiri wa hali ya juu sana. Nadhani kinachohitajika sasa ni michango yetu katika kusaidia mipango ya Serikali hii ili iweze kutimiza malengo yake.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba tunahitaji maendeleo na ndio linalozungumzwa sana humu na ndio matarajio ya wananchi wetu waliotuchagua. Lakini ni vizuri tukawa na vipaumbele na ndio maana sasa nichukue nafasi hii kupongeza Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji katika hotuba yake ambayo imetolewa na Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, kwamba mipango imechanganuliwa vizuri. Kikubwa hapa ni namna ambavyo tutaiendea na kuitekeleza mipango hiyo, hii ndio *challenge* kubwa kwa Serikali kwamba hata kama ni mizuri namna gani kama haitatekelezeka matokeo yatakuwa ni bure. *(Makofi)*

Lakini pamoja na mipango hiyo Wizara ya Fedha imetoa hotuba yake hapa ya Bajeti na tumepitia na kuona na binafsi ningependa nijaribu kugusa katika maeneo ya Bajeti nikilinganisha na mipango ya uchumi na vipaumbele ambavyo tumejiwekea. Kilimo katika mipango hakikuepukika kuwa kitu cha kwanza kabisa ambacho kinashirikisha ajira na kujikomboa kiuchumi kwa watu wengi zaidi katika nchi yetu, nilivyokuwa naiangalia ile Bajeti, inasema nini juu ya kilimo, sikupata kuona kwamba tuna nia kweli ya dhati ya kujikomboa au ya kufanya mapinduzi ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapinduzi ya kilimo yanahitaji mpango mahususi na malengo ya dhati kabisa yenye kusudio la kumfanya kila mmoja wetu anayeweza kufanya kazi, afanye kazi katika kilimo. Lakini hata pamoja na kwamba kila mmoja wetu anatakiwa kufanya kazi ya kilimo kwa maana tu ya kuwa na ardhi ya kuwa na nguvu. Lipo jambo tunalopaswa kufikiria zaidi ya pale, si kila ardhi inaweza ikalimwa na Mungu hakuumba ardhi inayofanana kiasi hicho, tukubali, tukatae kama tumeweza kuweka *Special Economic Zones* sasa tuweke *Special Agricultural Zones*. *(Makofi)*

Hata huko Ulaya ambako leo wanatupa misaada sisi ya chakula, siamini kwamba watu wote wanalima, tukisema tupange nchi yetu kwamba tunataka pengine mkoa wa Rukwa, Iringa na Mbeya tukawawezesha tukawapa *resources,* mimi nina uhakika kwamba wanaweza wakalisha nchi nzima hii. Kwa hiyo, ni vema tukawa *specific*, tukawa *specific* na tukasema kabisa na tukatunga sheria kabisa kwa ajili ya kilimo, hapa

tunazungumza zungumza tu lakini *at the end of the day* mimi naamini kabisa hatutaweza ku-*implement* kitu chochote katika kilimo kwa Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spik,a tunapozungumzia kilimo, mimi ninayetoka Kibakwe kule shida yangu kubwa ni mbegu ambayo huwa haipo lakini siku zote tuna *researchers*, tuna vyuo, mapesa na mapesa yanatumika ya wafadhili na za kwetu lakini hatuoni *achievement,* ukienda pale Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika pale Temeke ukaangalia matarakimu ya mabilioni kwa mamilioni yanayoingia pale lakini zinaishia kwenye *administration* tu, mipango itaandikwa pale watu wata-*shift* pesa kutoka huku kuweka kwenye akaunti hii biashara inaishia palepale hata kwenye *extension* haifiki.

Mheshimiwa Spika, hii ni *serious case* na ni vema kwa kweli kwa hakika watu sasa wa nchi hii tukaonyeshe uzalendo kwa nchi yetu. Tusizungumze vitu au kupanga vitu halafu tukashindwa kuvitekeleza, ni aibu na ni fedhea kwa nchi yetu na heshima yetu sisi wenyewe binafsi kama Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende katika eneo lingine nizungumzie sasa Halmashauri kwa maana ya TAMISEMI na kwa maana hiyo Ofisi ya Waziri Mkuu. Tumesema kuna *reform* ya *Local Government Authority* kwa maana ya Halmashauri. *Reform* hii itawekwa vizuri sana na Wizara ya Fedha imesema itaunda kitengo maalum kwa ajili ya kudhibiti kwa karibu matumizi ya fedha za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwenye Halmashauri ndiko kwenye matatizo, ndiko kwenye *fungus* inayoharibu maendeleo ya wananchi wetu na mimi nashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu anafahamu hilo, nashukuru sana Mheshimiwa Rais anafahamu hilo na pia juzi tulikuwa kwenye semina na Waziri Mkuu Kamati yetu ya *LAAC* na kwa ajili ya *reforms* niliona *concern* ya Waziri Mkuu, kwa sababu hata yeye alisema kwa kweli hata mimi hamninyimi hiyo semina na mimi lazima nihudhurie mwanzo mpaka mwisho. Lakini yote tunaweza tukayasema, tukafanya *reform* tukaweka katika maandishi hapa tuna-*deal* sasa na uaminifu, uadilifu wa watendaji kwa maana ya Wakurugenzi pamoja na wahasibu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwepo mimi kwenye Kamati ya *LAAC* nimejifunza na sasa ninazijua Halmashauri zote Tanzania nzima. Nimeona mambo gani yanafanyika kule, kumgundua mtu ambaye si mwadilifu, mwizi na ana nafasi hiyo, inatuchukua miaka mitano hadi kumi na tayari ameshatuumiza vibaya sana. Hivi kweli hatuna *mechanism* ya kumgundua mtu huyu ambaye ameamua kutokuwa mwaminifu kwa muda mchache iwezekanavyo ili asituumize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mipango iko wazi kuna mabaraza ya Madiwani pale kuna kila kitu, huyu mtu anafanyaje kwa nini itokee kwamba pesa zinapotea kwa nini malengo yasifikiwe na mimi nasema napongeza *reform* hii ambayo sasa na Waziri Mkuu anaisisitiza sana kwamba Halmashauri ni lazima ziingie mkataba na Serikali na mimi nasema kwa kweli waheshimu sana mawazo yetu sisi kama Kamati ya *LAAC* tutakapokuwa tunatoa kwamba Halmashauri hii haifai ifutwe ili Serikali iweze kuendesha mambo yake, vinginevyo watu hawatapata maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie jambo lingine la elimu, sasa ni ukweli tu uliowazi kwamba shule nyingi tulizozianzisha za kata hazina walimu, hazina viti. Mimi juzi nimekwenda shule yangu moja ya Luhundwa imeanza juzi juzi, wanafunzi walioripoti kutokana na *second selection* wamefika 67 kati ya 80, mwalimu alioko pale hana hata kiti, hata meza, wanafunzi waliokuja pale wenye uwezo wa kununua meza na viti wanafika ishirini na saba, hawa wengine wamekuja na vigoda kutoka nyumbani. Hii ndio hali halisi, lakini sisi katika mkoa wetu tumesema, wacha tu waende kwa sababu tunajua matatizo yetu kwamba tuko nyuma kielimu. Tumekubaliana na *RC* wetu Mheshimiwa William Lukuvi kwamba tuwaache tu twende hivyo hivyo, wawepo labda Serikali itakapopata uwezo itafanya hayo tunayokusudia.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hiyo kwamba viti hakuna, majengo hakuna, hata *administration block* hakuna yule mwalimu nilimkuta anasahihishia madaftari kwenye *tank* lililokuwa limehifadhi maji kwenye kiukuta pale ndio anasahihisha madaftari na mwalimu mwenyewe anaitwa mwalimu Msigala yuko mmoja tu, *this is very serious* uharaka uwepo hakuna vitabu, haya mengine inawezekana yakachukua muda kidogo kujenga *administration block* lakini hata vitabu ambavyo vinapatikana, kutoka Dar es Salaam tu kupelekwa Kibakwe pana matatizo gani vitabu tu hii *ni serious case*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie masuala mengine yanayotokana na Bajeti kama ilivyowasilishwa. Mimi napenda nikubaliane sana na Bajeti hii hasa katika ukurasa ule wa 32 ambapo imezungumzia kwamba kuanzishwa kwa Jeshi la Kujenga Taifa. Lakini tafsiri yangu mimi katika hii JKT inayoanza sasa mimi mawazo yangu ni kwamba angalau hii JKT iwe ni kiwanda cha kupatikana askari watakaojiunga na majeshi yetu. Kikiwa kiwanda hiki tutapima uadilifu wa vijana wanaokwenda kujiunga pale tutaweza kuwajua, hata haya matokeo ya ujambazi sasa yanatokana na kutokuwachuja vizuri hawa wanaojiunga na majeshi yetu. Hawachujwi vizuri anatoka tu huko alikotoka anaomba pale kwa sababu wengine wanasema awe mrefu basi anajaza anakuwa askari lakini haangaliwi kwamba ametokea wapi.

Mheshimiwa Spik,a mimi naamini JKT kama ile niliyoipitia mimi inafundisha watu uzalendo, inawafundisha watu uvumilivu na hivyo ni rahisi sana kuweza kuchuja na kupata askari anayeweza akafaa na akafanya kazi kwa uaminifu, vinginevyo mimi nasema itaanzishwa JKT kwa maana tu ya kwenda kuwaadhibu watu lakini itakuwa haileti manufaa mengine yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie maendeleo ya makazi. Katika Bajeti hii haijaonyesha bei, kodi juu ya saruji na mabati. Lakini maendeleo ya jamii yoyote inapimwa kwa matumizi ya saruji na mabati, kama mtu haishi katika nyumba bora maana yake mtu huyu ni maskini na hata huu MKUKUTA tunaousema, ishara yake kubwa ni watu kuishi katika nyumba bora. Lakini hapa haisemi kwamba kwenye saruji na mabati haisemi kodi yake ikoje na mimi ningesema kwamba hata ile iliyokuwepo ni vizuri ikapunguzwa ili watu waweze kununua saruji kwa bei nzuri na mabati kwa bei nzuri ili huu MKUKUTA uanze kuonyesha *sign*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie sasa barabara, sisi katika Mkoa wa Dodoma tunajivunia kwamba tuko katikati na tunajivunia kwamba wenzetu mnaunga mkono na wanachangia *equally* kama sisi umuhimu wa kuwepo makao mkuu Dodoma. Sitaki nizungumzie kasi yake kwa sababu nilikwisha kuchangia wakati ule baada ya hotuba ya Rais, lakini leo mimi nizungumzie tu kwamba kwa kweli kama barabara ya kutoka Arusha, Dodoma, Iringa itajengwa, italeta mabadiliko makubwa sana katika nchi hii. Fikiria unapotaka kutoka Mbeya uje Kondoa, ni lazima uzunguke kupitia Morogoro, ni gharama kiasi gani, tunakwenda kwenye gharama kubwa bure, tunatumia zaidi mafuta na hivyo kuongeza gharama za matumizi mengine yasiyokuwa ya lazima wakati tungeweza kutengeneza barabara hapa na mimi nimesema kwamba nimesoma mara nyingi katika taarifa mbalimbali zinazungumzia upembuzi yakinifu, sasa upembevu yakinifu basi tunachotaka barabara ijengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuzungumza katika ukumbi huu na hivyo kuchangia katika hoja mbili zilizoko mbele yetu. Nikupongeze wewe mwenyewe kwa kuchaguliwa kuwa Spika wetu kwa kura nyingi na leo tunajivunia kwa kuwa na Spika kama wewe, tunakushukuru sana na kukupongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii vile vile kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa ushindi mkubwa alioupata katika uchaguzi mkuu uliopita na vile vile kwa kazi nzuri ambayo tayari amewadhihirishia Watanzania katika kipindi kifupi kilichopita.

Vile vile Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Waziri Mkuu kwa kuchaguliwakuwa kuwa Waziri Mkuu. Lakini vile vile kwa kazi nzuri na kwa umahiri jinsi anavyofanya kazi yake na nina hakika kwa wale ambao ni wavivu basi saa hizi viti vyao ni moto wanakuwa na wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, leo hii tunashuhudia hali ya usalama wa nchi yetu ikirejea katika mahali pake baada ya majambazi ambao walikuwa tishio katika nchi yetu hii baada ya mizizi na mbinu zao zote kufichuliwa na hatimaye sasa kufikia hatua ya kikomo nina hakika kazi inayoendelea kuwang’oa kabisa itafikia mahali pake na nchi yetu itakuwa na amani.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Mawaziri wote wawili Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa na Waziri wa Fedha Mheshimiwa mama Zakia Meghji kwa hotuba zao nzuri kwa mipango mizuri na Bajeti nzuri ambayo kwa hakika ni Bajeti muhimu sana katika mwanzo huu wa Serikali ya awamu ya nne hakika Bajeti hii inadhihirisha mwanzo mzuri wa uongozi wa awamu ya nne wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na ni tafsiri halisi ya ahadi zetu kwa wananchi kwa vitendo kwa mujibu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Nina hakika wananchi wameipokea kwa furaha kubwa Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzuri wa Bajeti hii mipango hii kwa hakika haina mjadala mrefu lakini kwa vyovyote vile ni vizuri na sisi Wabunge tukaongezea pale ambapo pangehitaji kuwekwa sawa ili iwe *refund* zaidi. Niseme tu katika suala zima Bajeti hii, mipango sina wasiwasi nayo masuala ya uchumi na ukuaji wake sina *comment* mambo yanaenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu Bajeti ambayo nayo ni nzuri ni vizuri kwa Serikali kuangalia masuala yale yanayogusa wananchi hususan mahitaji ya wananchi wetu kule vijijini wenye kipato kidogo kama vile bei ya sukari, mafuta ya taa, kama walivyosema wenzangu walimezungumza masuala hayo. Lakini vile vile katika suala zima la wananchi tunasema waboreshe makazi yao vilevile amesema mtangulizi wangu sasa hivi kwamba bei ya bati, saruji na kadhalika mambo hayo yaangaliwe upya, hii ni katika ku-*refile* Bajeti ambayo kwa kweli tunasema ni Bajeti nzuri au ni Bajeti tangulizi katika Bajeti tano zijazo katika Serikali hii ya Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili Bajeti hii iweze kutekelezwa katika ilivyowasilishwa basi ni lazima kuwe na nidhamu ya hali ya juu, kuwe na uwajibikaji wa hali ya juu kwa viongozi wa ngazi zote Serikalini hususani katika Halmashauri zetu, Ma-*DC* wetu wafanye kazi ipasavyo, Wakurugenzi wafanye kazi ipasavyo na Wakuu wao wa Idara pale ndipo tunaweza kushuhudia ama bajeti hii imetekelezwa vizuri au vinginevyo lakini lazima kila mmoja wetu katika nafasi yake atimize wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Serikali ilitoa taarifa ya hali ya chakula nchini kwa mwaka 2006/2007 na katika taarifa hiyo tumeelezwa kwamba tumejitosheleza ama tunatarajia kujitosheleza kwa kiasi gani na niseme tu kwamba taarifa ile au hali ya chakula nchini kwa vyovyote itakuwa na *impact* katika Bajeti hii ambayo leo tunaijadili hapa Bungeni. Lakini niseme tu kwamba kidogo inasikitisha kuona kwamba taarifa hizi mara nyingine siyo sahihi takwimu siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya yangu ya Babati au niseme katika Mkoa wa Manyara kwa ujumla tunaambiwa tunajitosheleza kwa 121% na wakataja baadhi ya Wilaya ambazo zina upungufu wa chakula lakini Wilaya yangu ya Babati haikutajwa ambako mimi natoka na ninafahamu kuna maeneo kadhaa ambayo hali ya chakula siyo nzuri. Lakini katika taarifa hiyo haikujitokeza sasa nasema wakati utafika hatukujiandaa kwa sababu ya taarifa ambazo si sahihi halafu Serikali inaanza tena kukimbia huku na kule ili kuhakikisha wananchi wake wasife kwa njaa.

Sasa nasema takwimu sahihi ni muhimu katika Wilaya ya Babati kwa mfano ina upungufu wa chakula katika Kata za Ufana, Dabil, Haiti, Mwada na Magugu sasa kote huku lazima Serikali kuwa waangalifu na kuwa tayari kwa kukabiliana na hali hiyo. Sasa mbaya zaidi kule ambako tunasema tuna mavuno mazuri mahindi yote yaliyopo shambani sasa yamekwisha uzwa yakiwa bado shambani yanauzwa gunia moja kwa shilingi 6,000/= na mara nyingine unakuta mtu anauza ekari nzima kwa shilingi 200,000/= mahindi bado yapo shambani na zoezi hili la kuhamisha mahindi kwenda nchi jirani linaendelea sisi tunasema tunajitosheleza kwa 121% tunakaa tumetulia hatuna

wasiwasi kumbe wakati utafika tutaanza kuzungumza habari ya watu wanaokufa kwa njaa lakini miezi sita iliyopita hali ilikuwa nzuri.

Mimi nilifikiri Serikali itafute *controlling mechanism* ya kuhakikisha pamoja na uhuru wa soko tulionao lakini mahindi yale yote sasa hivi siyo yetu yamekwishahama nilifikiri nitoe angalizo hilo kwa Serikali ili tusije tukabaki katika kufurahia au kurudi katika takwimu tulizonazo.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la barabara. Katika hotuba ya Mipango aya ya 59 tunaona Mpango wa Utekelezaji wa Mradi Maalum wa Barabara Kuboresha Miundombinu ya Barabara katika mikoa sita. Imetajwa mikoa sita, lakini mimi naomba Mkoa wa Manyara ulivyo mchanga nao uongezwe katika orodha ya mikoa hiyo yenye matatizo au yenye miundombinu duni. Mkoa huu ni mkoa changa, barabara zake zote ni mbaya na niseme mojawapo ya barabara muhimu ni barabara inayoitwa *The Great North Road* barabara ya Kaskazini, barabara hii ni aibu kwa sababu katika barabara kuanzia *Cape Town* kwenda Cairo ni sehemu pekee ambayo ni changarawe kwa miaka nenda, miaka rudi sasa nilifikiri wakati umefika ku-*reverse* sasa jambo hili na tunapozungumza wenzangu wamezungumza habari ya Makao Makuu Dodoma. Makao Makuu Dodoma yatejengeka kwa kuwa na miundombinu mizuri namna ya kuingia na kutoka Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Serikali ione umuhimu wa barabara hiyo iwekewe lami lakini vile vile mkoa mpya wa Manyara, Makao Makuu yake haifikiki kwa Wilaya za Kiteto na Simanjiro huu ni mwaka wa tano, ndugu zetu hawa inabidi wasafiri kwenda Makao Makuu ya Arusha ndipo waje Babati. Sasa hii tunasema ni kero, zimetengwa fedha pale nadhani shilingi milioni 800 kwa mwaka huu lakini kwa kilometa 10 hatufiki ina maana tuna miaka mingine 20 ili tuweze kuwa na barabara hiyo.

Lakini mimi nasema wataalam au wahandisi wanapotuambia kilometa 10 au 20 kwa shilingi milioni 800 hii ni kutukatisha tamaa, mimi naasema tupate barabara iende moja kwa moja katika hatua ya kwanza hata kama ni ya udongo iwe barabara ambayo ina *shape* ya barabara kwa maana ya una *shape* barabara unafika mpaka Simanjiro au Kiteto hatimaye uanze kuweka hiyo *Engineering Gravel* ambayo mara nyingi wataalam wanatuambia na tutakuwa na barabara ambayo inatumika angalau basi hata kwa wakati au tuseme *seasonally*.

Mheshimiwa Spika, nizungumze habari ya Mazingira. Suala la kuhifadhi mazingira ni *agenda* kubwa duniani na vile vile katika nchi yetu tumeliweka mstari wa mbele na uongozi wa nchi yetu katika ngazi ya juu umelivalia njuga suala hili. Lakini nasema hii imetajwa katika aya 79 katika hotuba ya Waziri wa Mipango ya kwamba Serikali itachukua hatua ya kudhibiti shughuli za kilimo na ufugaji, sasa sambamba na hili Serikali imepanga kujenga na kuendeleza mabwawa na malambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vema zoezi hili likawa *approached* au tukaliendea katika hali ambayo lisionekane ni kama tunawaadhibu wananchi katika maeneo fulani fulani, nasema hivyo kwa sababu Jimboni kwangu pamoja na umuhimu mkubwa wa zoezi hili katika Bonde la Kilwa ambako wananchi wanalima kwa uzuri kabisa mazao ya

wananchi, chakula chao mazao yale yote migomba imefyekwa, ekari 30 zote zimefyekwa chini ni chakula chao ni tegemeo lao sasa wananchi wale wanafikiri walifanya makosa au tuseme wanaadhibiwa kwa kosa ambalo hawalifahamu lakini ni kosa la kujitosheleza kwa chakula. Sasa mimi nilifikiri lilikuwa ni suala la kushirikiana kwa pamoja ingawa hatimaye watafikia hatua hiyo ya kuondoa hiyo migomba lakini nilifikiri ni habari ya wao kuwa *on lookers* katika jambo hilo wasishirikishwe katika jambo hilo wasishirikishwe katika zoezi zima.

Mheshimiwa Spika, nilifikiri suala kama tukienda pamoja na wananchi wale wahusike kwa maana ya wadau wote kwa pamoja ninaamini wananchi hawataona kama tunawaadhibu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema Bajeti hii ni nzuri, kilichobaki ni sisi wenyewe kufanya kazi kwa bidii kila mmoja kwa mahali pake na kutimiza wajibu, naomba nisigongewe kengele kwa mara nyingine niunge hoja ya Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Damas Nakei, sasa namwita Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo. Naona tutakuwa na nafasi pia ya kumalizia nadhani na Mheshimiwa Juma Kilimbah, naye ajiandae.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii kwa mchana wa sasa hivi au asubuhi hii kuchangia hotuba mbili zilizombele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea kwanza nimshukuru Waziri wa Fedha, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, pamoja na wataalam wao wote ambao walishiriki katika mchakato mzima wa kuweka mambo vizuri na kusomeka kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuendelea tu nilizungumzie suala zima ambalo Mheshimiwa Waziri wa Fedha amelizungumza kuhusu suala la Bajeti au mchango ambao inapata SMZ kutokana na Bajeti ya Serikali ya Muungano, alizungumzia kuwa Serikali ya SMZ inapata bilioni 21.1 kwa kila mwaka ambayo hii inaingizwa katika bajeti kulikoni kule nyuma tulipotoka ambapo ilikuwa wanapewa tu kwa mgawo wa mkopo na misaada kwa kweli jambo hili ni zuri na tunalifurahia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini suala hili kwa kweli linasaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika shughuli zake za maendeleo na matumizi yake ya kawaida ambapo tatizo kubwa ambalo linajitokeza kuhusu suala la sekta za Muungano zinavyofadhiliwa au zinavyosaidiwa na Bajeti za Muungano si Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo asilimia fulani inayotokana na Serikali ya Muungano. Kitu cha kushangaza na

cha kusikitisha sana ambacho hivi sasa kipo Zanzibar kuhusu suala zima la Bajeti ya sekta ambazo ziko kule za Muungano, hili tatizo kubwa ambalo wanalisema mara zote na ni kikwazo ambacho haziwezi zikaendelea hata kujijengea ofisi au kujenga mandhari nzuri katika zile taasisi zao ufinyu wa Bajeti ambao wanaupata au fedha wanazopewa hazitoshi au wakati mwingine fedha hazifiki kabisa  na mara nyingine wanasema kwamba fedha ambazo wanatengewa ni za misaada ambazo hazipatikani kwa wakati wala wakati mwingine hazipatikani kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunazishukuru sana sekta ambazo hivi sasa zimejenga majengo yake kule na yanapendeza vizuri mfano *BOT* wamejenga tunawapongeza sana, Ofisi ya Bunge ni nzuri tu, Ofisi za Uhamiaji zinapendeza sana lakini suala zima la kusikitisha ni kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais haipo Zanzibar ni jambo ambalo linasikitisha sana na hili suala zima limezungumziwa mimi katika Bunge hili niko katika kipindi cha tatu lakini linazungumziwa kila siku katika bajeti lakini utekelezaji wake ni mdogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa  hiyo, tunaomba Wizara ya Fedha au Serikali kwa ujumla ya Muungano itenge fungu maalum kwa zile sekta ambazo ziko Zanzibar kuhakikisha kwamba kwa zile Bajeti inayopelekwa  kule inaweza ikatosheleza haja iliyopo kule. Huo ni mfano mzuri hizi sasa Ofisi ya Makamu wa Rais tayari wameshapewa kiwanja, kiwanja cha mwazo kime-*fail* hakikufanyiwa kazi, wakapewa kingine hakikufanyiwa kazi, mambo yanayoendelea ni yaleyale tutaendelea lakini mwisho wake hakuna ambacho kinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta ambayo hivi sasa inasikitisha sana ni Sayansi na Teknolojia ambayo inahama hapa na pale kila siku, tayari imeshapewa viwanja na maeneo ya kujenga ilianza Kaskazini, imehamia Kusini kwa Zanzibar lakini bado hawajapata nafasi ya kujenga, tatizo kubwa ni ufinyu wa Bajeti ambayo wanapewa ni ndogo na  haikidhi haja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa  hiyo, ipo haja  angalau na wao wajenge Taasisi ya *Science Marine* iliyopo kule Buyu Zanzibar, ufinyu wa Bajeti huu utatufikisha mahali ambapo kwa kweli si pazuri. Viwanja vinakatiwa majani tu kila siku wanakata  nyasi tu lakini ujengaji haujawekewa mkazo rasmi. Lakini suala hili ambalo kwa kweli huwezi kuwalaumu sana kwa sababu Bajeti ambazo wanapewa kweli inawezekana kuwa hazikidhi haja ya kujenga maeneo hayo.

Kwa hiyo, ipo haja tusisitize zaidi kuwa hii Bajeti tuliyo nayo hivi sasa kwa kuondosha kero kwa sababu kero zipo nyingi hata kero za ofisi kwa hiyo, kero nyingine kama hizi ambazo tunaweza kuzitatua tuzifanyie ufumbuzi zisilete bughudha katika Jamhuri yetu hii ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ambalo kwa kweli nataka kulizungumzia ni kuhusu suala la mipango. Katika Bajeti ya Mipango imeonyesha vizuri tu sekta  zote ambazo mchango wake katika Serikali unavyoenda lakini sikuona katika sekta ya uvuvi,

je, sekta ya uvuvi katika mpango huu mbona sikuiona wazi wazi inachangiaje katika Pato la Taifa? Je, wavuvi wanasaidiwaje katika sekta hii? Humu haikuelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakapo *wind up* mambo yake atuonyeshe ni jinsi gani sekta ya uvuvi inavyosaidia pato la Taifa au tunavyowasaidia wavuvi katika Maziwa yetu au Bahari yetu kuu tuliyonayo sasa hivi lakini kwa kweli humu katika hotuba yake sikuiona na kama imo basi haikuzungumziwa ambapo mwananchi anaweza akakisoma kitabu hiki au akaielewa kuwa inaweza ikatoa mchango gani sekta ya uvuvi au mvuvi anaweza tukamsaidiaje katika kuhakikisha kuwa na yeye anapata maslahi mazuri katika kuonyesha kuwa Serikali inamjali.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia hivi ni kwamba Mheshimiwa Waziri amewasilisha Bajeti nzuri sana na wananchi wanaipongeza sana lakini tatizo kubwa tulilo nalo nchini kwetu ni udhibiti wa mapato au hizi Bajeti zetu jinsi zinavyotumika kwa kweli Bajeti zinazokwenda katika Wizara, Taasisi, Mikoa au Halmashauri kwa kweli zinatumika vibaya mno ambapo inasikitisha kuonyesha kuwa pesa ambayo ni kodi ya wananchi inavyotumika vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali inaonyesha kuwa nchi hii kama fedha inatumika vizuri basi tutapata maendeleo ya kutosha, lakini ukweli fedha inatumika vibaya mno kwa taarifa yake ambayo ni ya mwaka 2004/2005 inaonyesha kuwa bilioni 35 zimepotea katika Bajeti iliyopita, Wizara tofauti, Mikoa, Halmashauri na Taasisi zilizoko nchini hapa. Kwa hiyo, ni tatizo ambalo kwa kweli kama hatuwezi kuidhibiti Bajeti na matumizi hata tuweke Bajeti nzuri kama nini itakwenda vile vile, inaonyesha kuwa katika Bajeti kuna ufisadi wa hali ya juu katika Mashirika yetu au katika Wilaya zetu au hata katika Halmashauri zetu au katika Mikoa yetu huo ufisadi upo au rushwa imekithiri katika Taasisi hizo au ubinafsi umejijenga katika Taasisi, matumizi mabovu na machafu yasiyoeleweka katika Taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaweza tukapiga makofi hapa tukaifurahia Bajeti lakini kama usimamizi wake haukidhi haja ya wananchi ni kazi bure tu. Mheshimiwa Waziri ni mpya lakini ahakikishe kuwa tupunguze lile pengo la bilioni 35 kwa kupotea katika nyakati tofauti tofauti ni hatari, kwa hiyo, ni suala ambalo kwa kweli aliangalie na kuhakikisha kuwa analifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano tu ninaweza nikatoa zile Taasisi ambazo fedha zimepotea kwa *imprest* tu peke yake yaani pesa zilizopotea ni bilioni 2.1 na kadhalika yaani hizo zimepotea kwa *imprest* tu hazikuwasilishwa kwa Mkaguzi Mkuu hiyo ni hali mbaya kwa kweli na matumizi mengine ambayo kwa kweli yanasikitisha yamo katika Wizara na Taasisi tofauti.

Mfano, Mambo ya Nje, nanukuu kipindi kilichopita fedha iliyopotea ni milioni 266, Waziri Mkuu milioni 32 halafu Ulinzi, Ngome milioni 222 zilizopotea ni *imprest* tu hiyo, Mahakama 410 milioni zilizopotea hizo, Ofisi ya Spika ukiwemo na wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika unadaiwa shilingi milioni 170 ikiwa ni *imprest* iliyopotea haikufika kwa Mkaguzi Mkuu kwa wakati hiyo usishangae Mheshimiwa Spika

ndiyo uhalisi ulivyo. Tume ya Uchaguzi 127 zimepotea hiyo ndiyo hali halisi tuliyonayo hivi sasa katika nchi yetu na Taasisi nyingi na Halmashauri huko hakusemeki ndiyo kwenye uozo na utumbo wa hali ya juu huko chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala kama hayo kwa kweli yanasikisha Bajeti tunayoiweka hapa kama haiwafikii wananchi zinaishia kwa wachache namna hii kwa kweli hakuna maendeleo yatakayopatikana, tutaweka Bajeti nzuri, tutajisifia vizuri lakini kama kwa wananchi haifiki pesa inavyokadiriwa kwa hiyo, ni suala zito ambalo kwa kweli linahitaji kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba hapa inazungumziwa sana *TRA*, *TRA* kwa kweli pamoja na maovu iliyonayo tuisifie sana kwa juhudi zake ambazo wanafanya hivi sasa. Yale mapungufu machache ni ya ubinadamu au ni wale ambao ndiyo wale niliowataja ambao hawajiheshimu katika utekelezaji wa kazi zao, kwa kweli ipo haja tuwapongeze kwa sababu kutoka bilioni 25 mpaka leo bilioni 190 na wanakadiria kufikia bilioni 200 ni kitu ambacho kwa kweli ni lazima tuwapongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo kasoro ambazo zipo tunaomba zirekebishwe, tuhakikishe kuwa wale waovu wanawajibishwa kwa sababu tatizo lipo katika ukusanyaji wa mapato baadhi ya sehemu kwa mfano kama walivyosema katika upande wa Bandari zetu au *Custom* ni mambo kama haya ni lazima tuyachunguze kama Mheshimiwa Waziri alivyosema kuwa anaweza akaondosha matatizo au kero lililopo Bandarini kwa hiyo, hili aliangalie katika mtazamo huo aliondoshe. Lakini kwa kweli mfumo mzima wa *TRA* wanafanya vizuri na lazima tuupongeze kwa hatua ambazo kwa hivi sasa walizonazo ambazo wamejikita kuhakikisha kuwa wanaweza wakafanikisha suala zima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache niseme kuwa naunga mkono hoja, nawashukuru. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimmiwa Spika, kwanza nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi, aidha, naomba niungane na Wabunge wenzangu walionitangulia kupongeza kwa dhati hotuba mbili za Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwekezaji pamoja na ile ya Waziri wa Fedha. Pia naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba, kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mbunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Awali ya yote kwanza naomba kuunga mkono hoja kwa 100%. Baada ya kusema hili labda nianze kwa kusema unajua Bajeti hii ni nzuri, inafurahisha na ina kila dalili ya ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya. Lakini kama kawaida kila kilicho kizuri hakikosi kasoro kidogo, mimi nina mambo madogo madogo hapa nimeyaona, naomba labda nitumie nafasi hii kuyasema. *(Makofi)*

La kwanza, kawaida katika Bajeti ya Serikali karibu 70% inafanywa katika manunuzi lakini Bajeti hii nzuri tunayosifia hapa ina kasoro kwamba haionyeshi mahali popote inapowagusa Maafisa Ununuzi na Maafisa Ugavi ambao wamekuwa wakichukua fedha za Serikali kwa namna moja au nyingine kufanya manunuzi mbalimbali pamoja na huduma ndani ya Serikali. Sasa labda niwaombe Serikali waliangalie hilo kwa mapana na marefu wafanyie marekebisho kidogo kwa sababu katika hali ya sasa watu hawa wasipoelimishwa ajira zilizotajwa humu kwamba kuna ajira zitaongezewa wenyewe hawataji tutapata matatizo mbele ya safari ni lazima tuwe na wataalam walio *qualified* katika kufanya hizi kazi kiasi ambacho kinaweza kusaidia kuongeza tija Serikalini, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Lakini la pili, naomba sasa niseme matatizo ya kule Jimboni, kama kuna mahali kuna matatizo ya maji nchini Tanzania basi Wilaya ninayotoka na Wilaya jirani kwa maana ya Wilaya ya Tandahimba na Wilaya ya jirani ya Newala basi zinaongoza nchini.

Mheshimiwa Waziri Mkuu nadhani unafahamu fika jambo hili kwa sababu ulikuwa Waziri wa Maji katika awamu iliyopita, naomba unisaidie safari hii umekuwa kiranja mkuu wa Serikali, matatizo ya kule unayajua, naomba unisaidie tupate maji kule. Najua tu kwamba pengine kwa kuwa ulikuwa tu Waziri wa Maji hukupata nafasi ya kuibana bana sana Serikali kulikuwa na wakubwa wako mbele kule ikawa tatizo, sasa wewe ndiye kiongozi mkuu wa Serikali msaidiane na Waziri wa Maji mtukomboe kule hali ni mbaya sana. *(Makofi)*

Lipo suala la barabara, hili nitaliongelea katika namna mbili. Namna ya kwanza ni barabara inayotoka Mtwara kwenda Tandahimba, Newala, Masasi na Nanyumbu, katika kutafuta tafuta hivi kujua sifa ya barabara kuwa *trunk road* ni vitu gani nilikuja kupata jibu kwamba mojawapo ni kuwepo na barabara inayounganisha Wilaya zote ndani ya Mkoa. Barabara yetu hii ina sifa hii, lakini barabara hii imeachwa tu haijaunganishwa na imekuwa ikisaidiwa na *TANROAD*. Kwa hali ya fedha wanayopangiwa *TANROAD* kwa mwaka, kwa kuwa ndani ya Mkoa wa Mtwara kuna barabara nyingi zinazohudumiwa na *TANROAD* barabara ile naomba sasa iwekwe iwe chini ya Wizara kwa maana ya *trunk road*. Kwa sababu ndugu zangu uchumi wa Mtwara karibu 90% unapitia barabara ile.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengi yanayofanyika kupitia barabara ile lakini pia barabara ile ni *alternative route* ya barabara ya Masasi huku tukipata matatizo Masasi kwenda Mtwara barabara ile ndiyo *alternative route* ndiyo inatuokoa, kuiacha hali ilivyo ile kwamba kilometa 100 tu kutoka Tandahimba kwenda Mtwara kutumia muda wa saa nne au tano inatisha na inasikitisha.

Mheshimiwa Spika, naomba muiangalie, tuiweke iwe barabara ya Kitaifa, ituhudumie wananchi wa Tandahimba kwa nia nzuri ya kuleta maendeleo ya dhati ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine labda hili nilieleze kwa kueleza kidogo matukio niliyokutana nayo wakati wa kampeni. Ndugu zangu nikiwa nawaomba kura wananchi kule niliweza kupita Tarafa ya Litehu, Kijiji cha Luagala ambapo kuna kituo cha afya, wakati naendelea kuwaomba kura nilisimamishwa, unajua nilifunga spika na

kwa kutumia gari nikasimamishwa kwamba kuna mgonjwa aliyekuwa taabani sana inabidi gari lile liazimwe ili akimbizwe hospitali nikafanya hivyo, lakini baadaye nilipohamia Mahuta nikakutana na tatizo hilo hilo, yupo mama mjamzito anatakiwa ajifungue kwa *operation* na alitakiwa aende Hospitali Newala karibu kilometa 10 kutoka pale Mahuta nikawaachia gari mgonjwa akapelekwa. *(Makofi)*

Lakini juzi nilipokuwa napita kuwashukuru wananchi wa Jimboni kwangu kule nilifika kwenye kijiji cha Namikupa ambako nako kuna kituo cha afya, nikakutana na mgonjwa aliyebebwa kwenye tenga na amewekewa *drip* na anataka kujifungua na anapelekwa hospitali ya Wilaya ya Tandahimba.

Sasa niliona ni majaribu hayo nakutana nayo lakini ninachotaka kukisema nimefurahishwa kwenye Bajeti hii ibara ya 35(7) ukurasa wa 32 inayosema kwamba fedha zimetengwa kwa ajili ya mikoa ya pembezoni na ununuzi wa magari kwa ajili ya Wilaya zenye mahitaji zaidi hasa kwenye Wilaya mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Serikali ni kwamba vituo hivi vya afya nilivyovitaja vya Mahuta, Luagala na Namikupa viangaliwe macho, hizi hela zisije zikaishia tu kwenye Makao Makuu ya Wilaya tuangalie wananchi wale walioko kule wanapata shida hasa akina mama wakati wa kujifungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nirudie lile suala langu la barabara nililosema sasa nataka kusema barabara ya Dar es Salaam kupitia Kibiti, Lindi. Jitihada za Serikali zimeanza kuonekana lakini nina wasiwasi sana kwamba Serikali haipo *serious*, nimeangalia kwenye Bajeti hii kwenye *Public Expenditure Estimate Development Vote page* ya 135, *Vote 98* ya Miundombinu. Kuna suala pale la pesa zimetengwa shilingi bilioni 7.6 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutoka Ndundu kwenda Somanga.

Mheshimiwa Spika, hela hizi ni chache mno kwa barabara ya kilometa 60 kuna haja ya Serikali ku-*re-visit* Bajeti iliyopo. Kwanza cha kusikitisha zaidi katika hizo pesa karibu bilioni 5.6 zinategemea fedha za wafadhili na katika Bajeti hii Mheshimiwa Zakia Meghji alipokuwa anasoma alisema mwaka jana kuna wafadhili hawakutoa fedha kwa sababu ya matatizo mbalimbali nyumbani kwao. Sasa hii ni dalili tosha kwamba huenda hiyo barabara isikamilike katika awamu hii. Mimi naomba tafadhali Serikali m-*re-visit*, tuwe *serious* na maendeleo tunayotarajia. Maana tunalalamika kila siku Kusini watu hawataki kwenda kule kwa sababu ya barabara hiyo hiyo. Tukamilisheni barabara hiyo. *Let us be considerate* kwenye hiyo barabara.

Lingine ni suala la mikopo, kwenye Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameeleza kuanza kwa kutoa mikopo midogo na ya kati. Mimi nataka kusema tuwe makini na hili tu- *concentrate* vijijini kwenye wananchi wengi ndiko kuna matatizo kule. Mijini huku wana *source* nyingi za *income* na kama kuna *NGO's* za matapeli ziko mijini. Lakini vijijini kule ni *serious NGOs* zile zinafanya kazi. Kwa hiyo, tuwa-*consider* wale tusi-*concentrate* mijini. Hiyo mikopo kama kweli ipo itakuja, italetwa ipelekwe vijijini ikiwa ni pamoja na vijiji vya Jimbo langu la Tandahimba. *(Makofi)*

Lingine kwenye Bajeti hii liko suala la mabenki na *infact* tulipitisha hapa Sheria ya Benki Kuu ile. Lakini mimi nataka kuchangia kwa mawazo kwamba mabenki duniani yamekuwa yachangia uchumi wa nchi kwa kiasi kikubwa sana. Katika hali ya Tanzania sasa mabenki yetu tumeyafanya mabenki huria na wawekezaji tumewapa uhuru wa kuwekeza wanapotaka. Yapo maeneo ambayo *infrastructure* yake kwa kuwaachia hawa uhuru hawawezi kufika. Sasa tubadilike kidogo tunapowapa nafasi kwamba wawekeze nchini tuwape na *political strength* kwamba lazima wafike angalau kwenye ngazi za Wilaya zetu. Wilaya kama Tandahimba, Mkuranga, Namtumbo na kadhalika, licha ya kuchangia uchumi wa nchi hii kwa kiasi kikubwa lakini hazina benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi juzi nilifika mahali fulani kule Jimboni kwangu nikamkuta mzee mmoja analalamika kwamba hela zake zimeliwa na mchwa karibu milioni moja hivi. *Of course* tulianza kuelezana vizuri na nini na baadaye akaamua kwamba angepeleka fedha zake benki. Lakini kwa mzee kama yule kuamua kwenda benki mbali kule Newala sijui wapi hawezi. Sasa lazima tuwe- *considerate* tunapoangalia mambo haya kwa nia nzuri ya kuijenga nchi yetu ili tuweze kupata maendeleo ya kutukuka.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kumalizia kwa kusema kwamba ninaunga mkono hoja ya Serikali kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii muhimu hasa katika mchana wa leo kuweza kujadili hotuba mbili ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji pamoja na ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Pia niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kama walivyotangulia kusema nawashukuru sana Mawaziri hawa wawili hasa kwa hotuba zao nzuri sana. Nimshukuru sana Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa hotuba yake nzuri na mipango endelevu kwa nchi yetu na hasa kwa wananchi wetu kwa kipindi cha mwaka 2006/2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda niingie moja kwa moja katika mjadala wenyewe hasa nikianzia na suala la miundombinu. Nitalizungumzia hili suala la miundombinu hasa nikilizungumzia zaidi nikielekea katika Mkoa wangu wa Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba Serikali ya Awamu ya Tatu ilifanya kazi kubwa sana na tunampongeza sana Rais aliyemaliza muda wake Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kazi nzuri hasa ya kuiweka sura ya nchi yetu kuwa katika kioo kinachoweza kuonekana hasa kwa masuala ya mawasiliano hususan masuala ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema kwa masikitiko sana hasa nikizungumzia barabara ya Kati ambayo inatoka Dodoma hadi Singida ambako unafika Singida eneo la Shelui hapo mpakani. *(Makofi)*

Naongelea suala hili kwa uchungu sana kwa sababu naamini kwamba sijui Singida imewekwa katika kisiwa cha aina gani kisichoendelezwa na kweli ipo barabara sasa hivi inaendelea kutengenezwa.

Mheshimiwa Spika, lakini katika kuangalia hata ule utengenezaji wa barabara yenyewe, mimi nimeangalia hata nashindwa kuelewa kwamba je, hawa ma-*contractor* ni wale wale ambao wanateuliwa katika Mikoa mingine. Kuna ma-*contractor* wameteuliwa wa Kichina, tunaye *contractor* anaitwa *CHICO* na mwingine anaitwa *SIETICO*.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha, inasikitisha sana kwamba barabara hii sasa inakwenda muda unakaribia, tuliambiwa kwamba itamalizika kwa kipindi cha miaka mitatu, lakini miaka mitatu hiyo inakwenda, lakini barabara yenyewe ukiona mpaka sasa hivi ilipofikia ni tofauti, ma-*contractor* wanaotengeneza barabara kuanzia hapa Dodoma kwenda Manyoni ndiyo wana afadhali *KONOIKE*. Ma-*contractor* hawa wameshindwa kutengeneza barabara, bado wanairudia barabara hiyo na barabara hiyo imefika wakati wa masika ina rejea kama awali na pengine inaharibika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia eneo la Sekenke, mimi naamini Waheshimiwa Wabunge wanaotoka Kanda ya Ziwa huko wanaelewa. Sekenke sasa hivi kuna kero na kero yenyewe ni kubwa zaidi kwa magari 200 au 300 yanakwama kila leo, yanakwama kwa sababu magari yanashindwa kupandisha milima kwa sababu ya barabara. Barabara hii hata katika kutengenezwa walikuwa wamefanya *diversion*. Hiyo barabara ambayo wanakwepa mlima, wamekwepa mlima vizuri, hii barabara ilitengenezwa mwaka 1992. Kwa bahati mbaya yale makalvati yalichukuliwa yote yakabebwa. Barabara ikawa imesimama. Sasa walipokuja hawa wakasema kwamba tutumie barabara hiyo hiyo ili kuweza kutengeneza.

Mheshimiwa Spika, lakini ninavyoongea sasa hivi ni madaraja matatu tu ambayo ndiyo yametengenezwa na hayajakamilika kati ya madaraja sita ambayo siamini na haya madaraja matatu yatatengenezwa kwa kipindi cha mwaka. Siamini katika kipindi kilichobakia kama wanaweza wakamaliza hayo madaraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba sana Serikali kwamba tuiangalie Singida kwa jicho la huruma, kwa sababu ya hali na mali, Singida imekuwa kiuchumi ndiyo magari yote yanapita hapo, magari yanayokwenda Rwanda, magari yanayokwenda *DRC*, magari yanayokwenda Burundi na magari yanayokwenda Mwanza ndiyo yanapita hapo hapo katika barabara ya Singida. Lakini peke yake tumebaki Singida kisiwani na tunaletewa *contractor* ambao wanasusua.

Mheshimiwa Spika, basi pamoja na hilo ningezungumzia hata suala la uwanja wa ndege, Singida sasa hivi imepanuka. Singida imepanuka lakini naona Bajeti ya mwaka huu tunaambiwa kwamba walikuwa wanatengeneza uwanja wa ndege. Uwanja wa ndege uliotengenezwa ni wa kutua ndege ndogo. Singida sasa hivi kuna watu wana uwezo na ndege za abiria zinaweza zikafika na iliwahi kutokea hata katika kipindi fulani kuna mtu mmoja wa Singida ni mfanyabiashara maarufu sana anakaa Oman anaitwa Salim Ajib.

Huyu aliwahi kukodisha ndege inaitwa *Eagle Air* na akasema alikuwa na hamu sasa afanye biashara ili aende, afike mpaka Singida, lakini akawa hawezi kufika Singida kwa sababu hakuna uwanja wa ndege.

Mheshimiwa Spika, sasa ni kwamba watu wa Singida barabara hatuna hata hicho kiwanja cha ndege hakuna. Sasa leo hata ma-*contractor* tunaopewa ni wa kubabaishaji babaishaji. Mimi naomba nizungumze katika Bunge hili, hivi sasa tuhakikishe kwamba barabara ya Singida inakamilika.Naiomba Serikali katika kipindi cha mwaka huu wa fedha barabara ya Singida ikamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee nizungumzie suala la pili, kuhusiana na ushuru wa bidhaa. Niipongeze sana Serikali kwa kupunguza ushuru wa mafuta ya taa, hii kidogo inaonyesha kwamba imejali walalahoi hasa wananchi waliopo vijijini. Naipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niipongeza Serikali kwa kupandisha ushuru wa vinywaji vikali, bia na sigara. Mimi naipongeza sana Serikali kwa sababu hivi havina matumizi ya lazima kwa binadamu. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mimi napata tatizo moja hasa kuzungumzia ushuru ambao umepanda wa muda wa maongezi kwenye simu za mikononi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni ushahidi kabisa Waheshimiwa Wabunge wenzangu hapa wataungana na mimi, utendaji wa kazi nyingi sasa hata Waheshimiwa Wabunge, hata za Serikali za kiutendaji sasa hivi unachangiwa kwa kiwango kikubwa na kuboreka kutokana na mawasiliano ya simu hizi za mikononi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hapa tulipo sasa hivi ukiwemo wewe katika Jimbo la Urambo naamini unatumia *remote control* ya simu kuweza kuwasiliana na wasaidizi wako ili kazi iende vizuri huko Urambo. Kadhalika wananchi wetu walio na hali ya duni na mimi naamini kabisa tulikuwa tunaomba sasa watu kama wa Iramba Magharibi nilikuwa nafikiri mahali ambapo barabara hazipitiki na mahali ambapo tunaona bado ipo kero tulikuwa tunaomba sasa tuletewa minara.

Mheshimiwa Spika, lakini leo wakati nilikuwa nakuja kuzungumzia kwamba kuwepo uwezekano wa kuyashawishi makampuni ya *Vodacom, Celtel, TIGO* ili yaende yakawekeze kule, lakini sasa naambiwa ushuru wa muda wa maongezi umeongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi wananchi wa kule kwa mfano ambao hawana barabara za uhakika, barabara zimechoka, wananchi kama wa Jimbo langu sehemu za Mwamapuli, Ndurumo, Tyegelo, Luono, Mgilango, Usiulize, Nkotikilanzi, Twike uje mpaka Mgongo ufike Shelui kwenye barabara kuu watafanya mawasiliano kwa njia gani na sasa hivi hali imekuwa mbaya kama hivi mnasema ushuru umeongezeka. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali iangalie suala hili.

Mimi naamini alizungumza mzungumzaji mmoja aliyepita akasema badala yake basi Serikali itoe ushuru kwenye simu zenyewe kwamba unapoleta ile *handset* ikiwa haina ushuru na baadaye mtu akiwa anainunua na muda wa maongezi inaweza ikasaidia sana, lakini ushuru unaingia kwenye *handset* na ushuru tena unaongezeka kwa muda wa maongezi. Naiomba sana Serikali ilitazame suala hili kwa makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala lingine la mazingira. Nina hakika kabisa kwamba Serikali ya Awamu ya Nne, iliingia kwa kasi na hasa kulinda mazingira na kuingia kwa kasi huku kulitokana na hali mbaya ya kuwa na njaa. Kwanza, hii pia ilikuwa ni katika kulinda vyanzo vya maji na mazingira kwenye ile misitu kuvuta mvua.

Mheshimiwa Spika, lakini eneo hili naliona maandalizi yake kidogo bado yana utata hasa kwa wananchi wetu wa vijijini wanaotumia kuni na wanaotumia miti kwa matumizi mengine kama ya ujenzi.

Mimi wananchi wa Jimbo langu, naamini Mheshimiwa Waziri Mkuu anaelewa hilo atakuwa shahidi kwamba nyumba zilizo nyingi ni za tembe na hizi nyumba za tembe zinahitaji lazima uwe na vitu vinaitwa mapawa. Sasa haya mapawa kazi yake huwa ndiyo yanakuja yanatandikwa juu baadaye yanafuata majani, yakishafuata majani na ndiyo unaweka udongo na ndiyo nyumba inakamilika na hii nyumba inaweza kudumu kwa muda wa miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, una wajibu wa kila baada ya miaka mitatu upate miti mipya ili uezeke nyumba ili uweze kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunaongelea bei ya bati aghali, bei ya saruji aghali, sasa leo tunaingia tunamwambia kila mwananchi akitaka kukata miti lazima aombe kibali na huko kuna urasimu kweli kweli. Sasa anapokwenda kuomba kibali kuna hatari wananchi wetu watalala nje. Kwa sababu ya kukosa mahali pa kuishi kama hatutaliangalia kwa makini hili suala. Naomba sana tuliangalie kwa umakini na tufanye maandalizi ya kutosha kuhusiana na suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kwa haraka haraka kuhusiana na suala la kilimo, ni sahihi kwamba kilimo ni uti wa mgongo. Lakini tumekuwa hatutoi kipaumbele kinachohusika au kukabiliana kwa dhati juu ya kulima kilimo endelevu kama tunavyosema kumuendeleza mkulima.

Sasa hivi kuna kilimo cha umwagiliaji kimetangazwa, ili sasa hivi tuendane na kilimo hicho lazima tuwe na kilimo cha mwaka mzima, tuwe na kilimo cha umwagiliaji. Lakini hiki kilimo tunachokwenda kulima hizi *scheme* zinazoletwa huko vijijini ni *scheme* ambazo si endelevu ni *scheme* ambazo yakishaisha masika na yenyewe imekwisha. Sasa naiomba Serikali badala yake kama tunahitaji kilimo cha mwaka mzima lazima tuhakikishe kwamba zile *scheme* ziwe na mabwawa na hayo mabwawa yasiwe mabwawa ya ubabaishaji yawe mabwawa kweli kweli. Mabwawa yaliyotengenezwa kwa viwango ambacho yanaweza sasa yakatunza maji ili hayo maji yaweze kutumika kwa kipindi cha mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwa kasi nizungumzie suala lingine la Utawala Bora. Dhana ya Utawala Bora imesimama katika mihimili mikuu mitatu, ukiwemo ushirikishwaji, uwajibikaji na uwazi. Lakini dhana hii inachangiwa na inaweza ikaleta maendeleo tukawa tumefuta umaskini ambao unawakabili wananchi wetu kama itatumika ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini dhana hii inatumiwa visivyo na hasa watendaji wenye dhamana ya kuwahudumia wananchi hasa Halmashauri za Wilaya. Watumishi wa Halmashauri za Wilaya kwa kweli hawawahudumii wananchi ipasavyo kwa sababu ya kujenga viburi na viburi hivi vinatokana na hao watumishi wa Halmashauri za Wilaya kukaa sehemu kwa kipindi kirefu. Watumishi wa Halmashauri za Wilaya wanakaa zaidi ya miaka 15, 20, mtumishi amekuja ameoa, amezaa na akapata wajukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Luhaga Mpina ameomba achangie katika hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wiki ijayo. Sasa bado kuna muda Balozi Hamis Kagasheki ndiye anayefuatia sijui yupo, hayupo. Mheshimiwa Samuel Chitalilo pia hayupo, Mheshimiwa Athumani Janguo, anaweza kuwa tayari. Ahsante sana Mheshimiwa Athumani Janguo.

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja hizi mbili zilizokuwa mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipochangia kwenye Mkutano wa Tatu mwezi Aprili, 2006 niliwapongeza Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri wote, wewe mwenyewe na Naibu Spika wako na Waheshimiwa Wabunge kwa kuteuliwa na kuchaguliwa katika uchaguzi uliopita. Leo, nataka niipongeze Serikali kwa kazi nzuri ambayo imeanza kuifanya katika Awamu hii ya Nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nataka nirudie kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kisarawe kwa kuweza kunirudisha katika Bunge hili mara tatu mfululizo na kwa ushirikiano wao mkubwa ambao unaniwezesha kutimiza majukumu yangu ndani ya Jimbo na kwa nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazidi kuwashukuru hao wananchi, lakini pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Bunge hili kwa kuweza kunirudisha katika Bunge la Afrika ambako nategemea kwamba mimi na wenzangu mliotuchagua tutatimiza wajibu wetu kwa kufanya yale ambayo mnategemea tuyafanye. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba hizi mbili ni nzuri na wananchi wetu wengi wamezipokea kwa shangwe zinathibitisha azma ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya kutaka kutekeleza Ilani yetu ya Uchaguzi ya mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikianza na hotuba ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji inaeleza wazi kuwa Bajeti ya mwaka 2005/2006 ilitekelezwa vizuri kwani licha ya majanga ya ukame uliosababisha upungufu wa chakula, UKIMWI ulioathiri nguvu kazi, kupanda kwa bei ya mafuta duniani kulikozidisha gharama za mafuta na kuongeza gharama za usafiri, upungufu wa umeme ulioathiri uzalishaji viwandani, lakini bado uchumi wetu uliweza kuongezeka kwa asilimia 6.8 juu ya kiwango cha mwaka uliopita na juu ya wastani wa ukuaji wa uchumi wa dunia na juu ya ukuaji wa wastani wa Afrika na Afrika ya Kusini mwa Jangwa la Sahara. Nasema Serikali tunaipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo ambayo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wetu iliongezeka kidogo kuliko vile ambavyo ingeongezeka kama tungeweza kuweka uzito katika maeneo ya usindikaji wa vyakula ambao ndiyo ungeweza kukuza uchumi wetu kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Vile vile kwenye viwanda kulikuwa na ongezeko, lakini ongezeko hili hatuwezi kujivunia sana kwa sababu lilikuwa kidogo na lilikuwa kidogo kwa sababu maeneo ambayo yameweza kukua ni yale kama tulivyoambiwa katika bajeti, eneo la mabati na uzalishaji wa saruji. Kama tungewekeza zaidi katika usindikaji wa mazao ya kilimo naamini kabisa kwamba uchumi wetu ungeweza kukua zaidi kulikoni kiwango ambacho tumekifikia.

Mheshimiwa Spika, maneno yangu yanathibitishwa na Mheshimiwa Zakia Meghji, anapokubaliana nami pale anaposema katika Ibara ya 53, nanukuu: "Aidha, Sekta ya Viwanda ikiboreshwa na kutilia mkazo usindikaji wa mazao ya kilimo ina nafasi kubwa ya kuchangia pato la Taifa na kukuza ajira."

Mheshimiwa Spika, lakini nafarijika kwamba katika Ibara ya 110 ya hotuba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji hili limezingatiwa. Nami nasema kuwa wananchi wangu wa Kisarawe wanalisubiri suala la kusindika vyakula kwa shauku kubwa, hasa kama viwanda vitakuja ndani ya Wilaya. Kwa sababu tuna vyakula vingi, tuna korosho, tuna matunda mengi ambayo yakisindikwa yataongeza uchumi wa Wilaya na Taifa na pia yataongeza ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijahamia kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha, ninapenda kuipongeza tena Serikali kwa mambo yafuatayo:-

Kwanza, kwa jinsi Serikali ilivyoweza kushughulikia suala la janga la njaa. Lakini nashauri kuwa siku zijazo pawe na usimamizi thabiti wa ugawaji na usambazaji wa chakula hicho ili kiweze kuwafikia walengwa.

Mheshimiwa Spika, pili, kuanzia sasa naishauri Serikali ijitahidi kujenga maghala ikiwezekana kila Wilaya na Mkoa ya kuhifadhia chakula kujikinga na njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile naipongeza Serikali kwa kuleta hapa Bungeni hoja ya Itifaki ya *African Peer Review Mechanism (APRM)* iliyoridhiwa na Bunge lako Tukufu mwezi Februari, 2005.

Pia Serikali imechukua hatua haraka za kuweza kuialika Sekretarieti ya *NEPAD* kuja kuhakiki utekelezaji wa programu ya *NEPAD* hapa Tanzania. Kwa hatua hizi Tanzania imekuwa moja ya nchi chache sana za *AU* ambazo zimeweza kutekeleza matakwa ya programu ya *NEPAD.* Nasema Serikali tunaipongeza kwa hatua hizi. *(Makofi)*

Vile vile nataka tu niishauri Serikali pamoja na kwamba wamepeleka orodha ya miradi ambayo ingeweza kutekelezwa chini ya *NEPAD* kama ilivyoelezwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kwenye orodha ile naishauri Serikali iongeze mambo mawili kama hatujachelewa, la kwanza, ni usindikaji wa vyakula kwa umuhimu ule ambao nimekwishaueleza na la pili, umeme vijijini kwani ninaamini kwamba kueneza umeme vijijini kutasaidia sana kuchochea maendeleo ya vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba suala la umeme vijijini kidogo linatatiza na kuna kupingana baina ya hotuba hii ya Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na majibu ambayo tuliyapata wiki iliyopita kwenye swali namba 24 ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini alitamka kwamba umeme vijijini kwa sasa hivi haiwezekani, usubiri mpaka hapo Serikali itakapopata fedha.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye hotuba hizi tunaambiwa kwamba umeme vijijini utasambazwa. Swali tusikilize majibu ya Naibu Waziri wa Nishati na Madini au tuamini yaliyomo katika hotuba hii? Labda Mawaziri watakapokuwa wanatoa majumuisho wanaweza wakatueleza vizuri.

Mheshimiwa Spika, naupongeza uamuzi wa kuifanya *TIB* iwe Benki ya Maendeleo na kuiongezea mtaji kutoka shilingi bilioni 24.9 hadi bilioni 50. Lakini kama sikosei sijaona katika Bajeti hii wapi Serikali imepanga bilioni 25.1 za kuweza kutekeleza azma hiyo ya kubadili *TIB* kuwa Benki ya Maendeleo. Kama sikosei ningetegemea kuziona fedha hizi katika kasma 50, kasma ndogo 2003 chini ya Msajili wa Hazina. Nilipoangalia pale kwa maana ya uwekezaji hakuna fedha iliyopangwa zaidi ya bilioni 1.5. Swali je, fedha hiyo itatoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimwia Spika, hapa hapana shaka vile vile baadhi ya mapendekezo katika hotuba hii yanaashiria kuyaacha nyuma kimaendeleo baadhi ya maeneo ya nchi yetu hii. Kwa mfano, katika Ibara 35 ya hotuba ya Waziri wa Fedha inazingatia mambo saba muhimu. Mojawapo ni kutenga fedha kwa ajili ya maeneo yaliyo pembezoni.

Mheshimiwa Spika, lakini iko Mikoa ambayo haiko pembezoni na iko nyuma kiuchumi. Sasa kama tunazungumzia Mikoa ya pembezoni kijiografia tutaacha Mikoa kama Mkoa wa Pwani, Singida, Lindi na Rukwa ambayo kwa kweli iko nyuma na inahitaji kutiliwa mkazo katika Bajeti hii. Naiomba Serikali badala ya kutumia neno

pembezoni watumie neno la Mikoa iliyo nyuma ili kuzingatia kwamba iliyo pembezoni ambayo iko nyuma na ile ambayo iko katikati ya nchi itakuwa imewekewa uzito iende sambamba na Mikoa mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kodi mbalimbali zinazopendekezwa nina haya ya kusema:-

Kwanza, naipongeza Serikali kwa kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye petroli, gesi ya kupikia, kahawa iliyosindikwa nchini na kadhalika. Nazipongeza pia hatua zote ambazo zimechukuliwa za kuziba mianya ya ukwepaji wa kodi, haya ninayapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na kupongeza huko tungetegemea kwamba Bajeti angalau ishushe kidogo kiwango cha Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT).* Kwa sababu nafikiri iko juu ingawa tunasema kwamba tunataka kuwa sawa sawa karibu na nchi zilizokuwa jirani. Lakini naamini kwamba ukiipunguza kodi hii katika mazao mengi naamini utapanua wigo wa walipa kodi na pengo litakalotokea kwa sababu ya kupunguza kodi linaweza kuzibika kutokana na wingi wa watu watakaolipa kodi hii.

Mheshimiwa Spika, pili, kupunguza kodi ya mapato kwa makampuni mapya yatakayojiunga na soko la mitaji na kuuza asilimia 35 kwa wananchi ni jambo nzuri. Lakini nasema tumechelewa. Tungefanya hili tangu wakati tulipokuwa tunabinafsishaji Mashirika ya Umma ili kuwapa wananchi wa Tanzania angalau hisa katika mashirika hayo. Lakini kusubiri makampuni mapya ambayo hayajaanza, mimi ninaamini kwamba tutakuwa tumechelewa. Kama tumechelewa hivyo basi yale Mashirika 36 yaliyobaki hayajabinafsishwa nashauri hili lifanywe. *(Makofi)*

Tatu, kuongeza kodi mbalimbali kwa asilimia 7 eti iende sambamba na mfumuko wa bei wa sasa na kuongeza ushuru wa vinywaji baridi ni sawa na kuwakandamiza walalahoi na kuchochea mfumuko wa bei ambao tayari umeshapanda mpaka kufikia kiasi kilichosemekana asilimia 6.9.

Mheshimiwa Spika, sikubaliani kabisa na uamuzi wa kuongeza ushuru wa simu za mikononi. Walionitangulia wamesema hilo. Simu ni kichocheo cha maendeleo ingawa kwangu kule Kisarawe simu hazijafika za mikononi katika sehemu nyingi pamoja na jitihada zangu zote za kuwafuata Mawaziri wa Mawasiliano aliyetangulia na wa sasa bado hazijafua dafu. Lakini nasema mahali pengine simu za mikononi zimefika bora tuziachie ili kusudi wananchi waweze kuwasiliana, *information is power.* Kama watu hawawasiliani sidhani kama kutakuwa na maendeleo. Vile vile sikubaliani na mapendekezo ya kuongeza ushuru wa barabara kwa sababu itaongeza tena mzigo kwa wananchi wetu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nikushukuru tena kwa kuniruhusu niweze kuchangia kwenye hotuba hizi mbili. Naunga mkono hoja zote mbili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda wa kikao chetu kwa asubuhi hii umekwishatimia, nina matangazo machache tu.

Kwanza, kuhusu matumizi ya *microphone*, tunaombwa sote tuwe waangalifu. *Microphone* hizi namna zilivyowekwa ni mbili tu hizi ya Msemaji wa Serikali na hapa na pengine na hii ya Kambi ya Upinzani ndiyo zinaweza zikaingiliana na yeyote anayeongea. Nyingine ikiwa imewashwa kwa bahati mbaya inaweza kuzima ile nyingine ambayo inatakiwa wakati huo anaongea. Kwa hiyo, tunaombwa tuwe waangalifu kwenye hizo *microphone.*

La pili, naomba kuwakumbusha Wajumbe wote Makamishna wa Tume ya Huduma za Bunge kwamba tuna kikao saa 7.30 kwenye Ukumbi wa Spika, taarifa ilikwishafikishwa kwao kwa maandishi. Tume ya Huduma za Bunge leo saa 7.30 mchana.

Tatu, katika utaratibu wangu ule ule wa kuendelea kuwazoesha wenzangu wengine mliowachagua kusimamia Shughuli za Bunge. Leo jioni Wenyeviti wetu humu Mheshimiwa Job Ndugai na Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa zamu kadri watakavyokuwa wamepangiana watasimamisha uendeshaji wa shughuli za Bunge kuanzia saa 11.00 jioni.

Mwisho, kwa udhuru maalum nimeombwa na Mheshimiwa John Cheyo, ambaye alikuwa kwenye orodha namba 60 kuzungumza, analo jambo la kifamilia kule Bariadi na kama kawaida Spika uangalia mtu mwenye udhuru kwa mambo kama hayo, basi anapewa nafasi ya mapema zaidi. Kwa hiyo, yeye ndiye atakuwa msemaji wa kwanza saa 11.00 jioni katika kuchangia hoja ya Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Baada ya yeye kumaliza Mheshimiwa Balozi Hamis Kagasheki na Mheshimiwa Samuel Chitalilo, kama watakuwepo ni vyema, kama hawatakuwepo basi kwenye orodha yangu anafuata Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Charles Keenja na Mheshimiwa Siraju Juma Kabogonya, wajiandae.

Baada ya kusema hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, awali ya yote nataka kukupongeza wewe kwa kushika hicho kiti vizuri ingawaje kwa wewe ni mtani wangu ningeongeza *size* kidogo labda mambo yangekuwa murua zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia na mimi nataka kuungana na Wabunge wenzangu waliompongeza Mheshimiwa Yusuf Makamba, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge, ni vizuri

wazee tukawa wengi katika Bunge hili ili kulisaidia Bunge, kwa hiyo, hongera sana ndugu yangu Yusuf Makamba. Lakini baada ya kusema hayo pia tungependa tujue tu kama ibara ya 67 ya Katiba imezingatiwa zaidi Ibara ya 67(2) (g), kifungu kinachozungumzia juu ya Afisa Mwandamizi kuchaguliwa kuwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni wazi kabisa hilo linakatazwa katika hiyo Ibara lakini kama amesita kuwa Afisa Mwandamizi basi hakuna tena hoja juu ya hilo, lakini ingekuwa vizuri kama Rais ameshamwambia asiwe tena *Regional Commissioner*, asiwe tena Mkuu wa Mkoa, hakuna ubaya kwa Rais kumchagua awe Mkuu wa Mkoa baada ya kuchaguliwa kuwa Mbunge kama vile Katiba inavyosema.

Kwa hiyo, tungependa kujua kama hilo liko sawa au vipi ni mambo tu ya kuelimishana, lakini mimi namuunga mkono kabisa Rais kwa kumteua Mheshimiwa Yusuf Makamba kuja katika Bunge hili. Mbona hampigi makofi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nataka kuchukua nafasi hii kuwapongeza viongozi wote wa Serikali ambao wameendesha Serikali hii mpaka hivi sasa tangu wamechaguliwa, kusema kweli mtu anayeona hali hii mpaka hivi sasa tangu amechaguliwa, kusema kweli wanafanya kazi nzuri sana, nawapa hongera sana na zaidi wakiongozwa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais ameonyesha kitu kimoja ambacho mimi nataka kusema hata bila kusita hata kidogo utaifa wa Taifa hili. Kweli ni mtu ambaye ameonekana ni mtaifa, mtu anayejali watu wake na bila ubaguzi na nasema hili baada ya kumwona mimi Mheshimiwa Rais tulipokwenda kwenye safari ya Amerika nikaona kweli huyu mtu kweli ana mwelekeo wa Kitaifa na jambo hili mimi naona ni jambo la kuigwa na sisi wote Wabunge na pia watu ambao wamekabidhiwa visehemu vidogo vidogo vya Urais kama vile ma-*DC*, ma-*Regional Commissioner* na wengine na zaidi watu ambao wamekabidhiwa shughuli ya haki kama vile ma-*RPC*, ma-*RCO*, ma-*OCD* na wenyewe waige kwamba nchi hii ni nchi moja na mdau wetu ni mmoja ambao ni wananchi wa Tanzania kama alivyosema Rais wakati alipokuwa anafungua jengo letu hili nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi nataka kusema wazi kabisa kwamba Kambi ya Upinzani iko tayari kushirikiana na Mheshimiwa Rais na mimi kwa niaba ya wananchi wa Bariadi tuko tayari kabisa kushirikiana na Mheshimiwa Rais na viongozi wote kuhakikisha kwamba tunapata kile tunachotaka ambayo ni ubora wa maisha ya wananchi.

Pia kabla sijasahau nataka kuwapongeza sana Mheshimiwa Zakia Meghji kwa kutoa hotuba nzuri pamoja na Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, kwa hotuba aliyotoa hapa ndani ya Bunge letu. Lakini bila kusahau upande wa Upinzani Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed wa Kambi ya Upinzani na Mheshimiwa Kabwe Zitto ambao pia wametoa hotuba nzuri, wameonyesha kazi yetu kweli ya Upinzani sio chama pinga, lakini ni kushirikiana katika kutafuta upande mwingine wa shilingi. Kwa hiyo, wamefanya kazi nzuri sana, waendelee hivyo hivyo na zaidi Kambi ya Upinzani nataka kuwaambia mimi nikiwa mmoja wa wachache wa viongozi wa vyama katika Bunge

kuwa sasa tuko katika mstari ulio bora, ambapo wote tumekubaliana kushirikiana na kuweza kuwatumikia Watanzania kama kitu kimoja. Kwa hiyo, hongera sana Kambi ya Upinzani kwa uamuzi huo na jinsi ambavyo tumeamua kufanya mambo yetu.

Baada ya kutoa hizo pongeza ambapo pia ni pamoja na pongezi kwa Kamati ya Fedha na Uchumi, kusema kweli ripoti ya Kamati ya Fedha na Uchumi chini ya Mheshimiwa Dr. Abdallaha Kigoda, imetupa ripoti nzuri na kwa mara ya kwanza tumeona tunaletewa hata jinsi zamani tulikuwa hatutoi waraka huo kwa kila Mbunge, lakini tumepokea hotuba zao na mimi nimezisoma, kweli tuko katika mstari barabara kwa kuhakikishia kwamba sisi kama Bunge tunafanya kazi yetu ambayo tumepewa na Katiba chini ya Ibara ya 65 ambayo ni pamoja na kuangalia Bajeti ya nchi hii na hiyo pamoja na pia na kudhibiti na kusimamia shughuli za Serikali, kwa hiyo, wote hawa nawapa hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hongera naomba sasa nijikite katika mambo ya Bajeti, kwanza nataka wote tujiulize kama hii Bajeti tunayofanya kila mwaka tunakaa karibu miezi mitatu, tunashughulika, tunazungumza je, hizi Bajeti ni kweli zinatekelezeka? Hizi Bajeti ni kweli halisi, hizi Bajeti ni kweli zinausahihi au ni maneno tu watu wanajaza ma-*figures* tu halafu baadaye ukiisha mwisho wa mwaka tunakuja habari nyingine na vitu kama hivyo.

Mimi ningependa kushauri kuwa kwamba Bajeti ambayo kweli itaweza kusaidia wananchi lazima itabirike, iwe na usahihi na ionekane kama sheria yaani *binding, a binding contract*, watu wanazungumzia juu ya Ilani ya Uchaguzi mimi nakubali hii ndio Ilani yenyewe, sasa ni *binding* yaani ndio ukisema ukiniambia utanipa daraja, kweli utanipa daraja sio uniambie maneno hapa halafu baadaye mwisho wa mwaka unakuja *performance* yako sio sawa sawa na hapa mimi nataka kutumia muda kidogo tu ku-*share* maoni yangu juu ya *performance* mbalimbali za Bajeti.

Kwa mfano, Bajeti ya mwaka 2003/2004 tulikuwa tumekadiria kutumia kwa ajili ya *supply vote* tu ya Serikali shilingi *trilioni* 1.8 ni kweli *performance* yake mwaka huo ilikuwa *99 percent* hamna matatizo, mbele ya hela ambayo inakwenda kwa kula kwa watu, hela inapatikana haina matatizo. Lakini kwa upande ambao ndio upande wa maana zaidi kwa upande wa maendeleo tulikuwa tumekadiria tutumie *point* nane trilioni kwa ajili ya maendeleo, lakini tukatumia *point* tano tu *trilioni* ambayo ndio kusema tulikuwa na utekelezaji au *performance* asilimia 69. Sasa hizo ni hela nyingi sana maana yake tunazungumza juu bilioni 300 ambazo hazikutumika. Lakini pia hizi takwimu ni takwimu za kutokana na *CAG* ripoti, lakini kwa bahati mbaya na hii ndio kitu mnasema usahihi na *consistence* sio tu usahihi na *consistence* ya bajeti lazima iwepo. Ukiangalia takwimu za Bajeti ambayo tulipitisha 2003 zinatofautiana na takwimu za *CAG*.

Sasa kwa mfano, mimi nimesema kufuatana na *CAG estimate* ni 1.8 trilioni. Lakini kufuatana na Kitabu tulichopitisha hapa ni trilioni 2.3 na ushehe, kuna tofauti. Hizi ni hela nyingi, kama tunataka kweli Bajeti yetu ionekane kwamba ina usahihi basi ile takwimu zinazotoka kwa *CAG* zifanane basi na takwimu za vitabu tunavyopitisha katika Bunge hili. *(Makofi)*

Hivyo hivyo kuna tofauti kwa fedha ambazo tumeweka kwa mwaka huo huo kwa ajili ya maendeleo na hivyo hivyo mwaka 2004/2005 na 2006. Kwa hiyo, mimi ningesisitiza kwamba Bajeti tunazotengeneza ziwe na usahihi na ziendane na ripoti ya *CAG*, la sivyo tutakuwa vitabu vinavyotengenezwa havina *credibility* yaani mtu akiangalia anasema kwamba labda mnafanya mchezo na hatufanyi jambo linalohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nataka kujikita kwa upande wa mchakato wa Bajeti yenyewe, mimi nashauri jambo ambalo limemalizika sasa hivi Bunge kuweza kushiriki katika Kamati mbalimbali ni jambo jema na naona tu kwamba Serikali inasikia sana tunapokuwa tunashiriki kama Wabunge katika Kamati zetu mbalimbali na jambo hili ningeshauri tu kwamba liendelezwe tena kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama jambo la mafanikio kwa mfano tumeona katika Bajeti ya mwaka 2005/2006 inayoishia sasa, karibu asilimia 90 ya hela ambao tuliwaahidi wananchi waweze wakachukua kama za maendeleo kweli zimepatikana hizo asilimia. Kwa hiyo, ningeshauri tuendelee na huu mchakato wa pamoja kuliko kwamba kitu ambacho hatukifahamu.

Pia ningependa kujikita katika Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, mimi sina matatizo na MKUKUTA. MKUKUTA ni sawa sawa na ninavyoamini mimi ni kwamba hiyo ndiyo kujaza watu mapesa. Ni sawa sawa kabisa. Lakini nina tatizo juu ya misamiati mingi inayotoka kule na misamiati kama *Tanzania Mini-Tiger Plan*, imezungumzwa lini, najua imepitishwa haraka haraka nikiwemo na mimi hapa lakini mikakati inapokuwa mingi ni sawa sawa na mtu kumwita majina mengi. Kwa hiyo hawaelewi tunafuata, MKUKUTA, tunafuata *TMG*, MKURABITA, tunafuata nini. Mimi ningeshauri tupunguze idadi ya misamiati, kwa sababu tumeamua sasa twende MKUKUTA twende MKUKUTA, watu wa Ilani ya Uchaguzi semeni mnachopenda hakuna anayebisha lakini msitumie hela zetu kueneza Ilani ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hilo mimi sina matatizo nayo, ningependa sasa kujikita kidogo kwa haraka haraka kwenye kilimo. Kilimo kimeonyesha watu kuwa fedha ya kilimo imepunguzwa jambo ambalo ni la ajabu, mimi ningependa hili jambo liangaliwe tena upya, lakini zaidi kwenye kilimo juu ya pamba. Kwenye pamba mimi nasema hata ukitaka mambo ya mazingira pamba ndiyo inaweza ikakupa hata chakula cha ng'ombe. Ili ng'ombe waweze kuwapata wazungu wanasema *zero grazing*, mimi naona hili jambo la pamba tungeliangalia kwa ukaribu zaidi ili bwana mazingira ahakikishe kwamba kweli badala ya kutumia fedha nyingi kufukuza ng'ombe tusiwe na ugomvi na ng'ombe, tuwe na upendo wa ng'ombe tuwalishe ng'ombe kwa kupitia pamba.

Kwa hiyo mimi nashauri Serikali ingetenga fedha kwanza ya pembejeo. Kwa nini wanawapa tu watu wa Kusini pembejeo, kwa nini wanaolima pamba wasipewe pembejeo, kwa nini ng'ombe zisihakikishwe kwamba na zenyewe zinasaidiwa na ionekane wazi wazi kwenye Bajeti kwamba zinasaidiwa. Jambo hili halimo kwenye Bajeti na naona hii ni sehemu ambayo tumesahauliwa kabisa. *(Makofi)*

Kuhusu madini, mimi nawashukuru sana, Wizara imefanya kazi nzuri sana juu ya madini, nimeshukuru kwamba kumekuwa na shilingi milioni 750 ambazo juzi Wilaya mbalimbali zimepata kutoka kwenye migodi, hongera sana endeleeni na mtazamo huo, *I think* ni jambo ambalo ni jema.

Kuhusu jambo la elimu, mimi hapa ningependa kusema kitu kimoja, najua tumepata bilioni 105 ambazo ni za maendeleo, lakini lazima tugeuze mitazamo. Mimi mtazamo wa zamani kuwa kwamba elimu ya msingi ni darasa la saba umepitwa na wakati, ni lazima tukubali kwamba kusema kweli sasa elimu ni *secondary school*. Tukikubali sisi wote hivyo basi mikakati yetu yote itaelekea huko huko, na sasa hivi *secondary* unikuta kwa Waziri Mkuu, iko Wizarani, iko kwenye Halmashauri hata haijulikani ni nani kweli mwenye jukumu la jambo kama hili, lakini ni aibu kuwa na watoto milioni 7.5 ndani ya *primary* na walio ndani ya *secondary schools* ni 500,000. Hatuko *serious*, mimi naona tuamue *basic education* ni *secondary school* na sio *primary school* kama zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo ningependa kujikita katika mambo ya miundombinu, hapa zaidi nataka kusisitiza, daraja letu la Simiu aliloahidi Rais, natumaini litatokea katika vitabu, nime-*check* sijaliona lakini mimi nina hakika hata siku moja Rais huyu hajani-*let down*. Kwa hiyo, kwa kuwa ameshatuahidi kwamba daraja letu hilo litapatikana. Pia ametuahidi watu wa Shinyanga kupitia Maswa, Bariadi na mpaka Lamadi tutapata lami nime-*check-check* lakini sioni limeandikwa hilo lakini matumaini yangu vitabu vitaibuka ili vionyeshe kwamba kwa kuwa Rais amesema hilo litakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine juu ya miundombinu, mimi nasema na ni vizuri nimeona Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia juu ya barabara, lakini tuzungumze barabara za vijijini, *conectivity of villages* ndiyo ukombozi, ndiyo MKUKUTA. Kama watu tuliweza kuwaunganisha kwa barabara mbalimbali mimi nina hakika kwamba utakuwa umewasaidia sana katika janga hili la umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ningependa muda zaidi lakini basi nashukuru na nahakikisha kwamba nitashirikiana na Mheshimiwa Waziri kuhakikisha kwamba hii kitu inatekelezwa vizuri sana *(Makofi)*

**MHE. BALOZI HAMIS S. KAGASHEKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii kwanza niseme kwamba nakupa hongera na nafurahi kukuona umekaa hapo ukiongoza shughuli zetu katika kikao hiki cha mchana. *(Makofi)*

Baada ya kusema hivyo ningependa niseme kwamba natoa shukrani zangu nyingi sana, kwa Waziri Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, kwa mapendekezo yake ambayo ametutolea hapa ya mipango ya nchi yetu na pia ningependa nitoe shukrani zangu kwa Waziri wa Fedha kwa kutoa hotuba ya Makadirio na Matumizi ya pesa kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijazungumza mambo ambayo ningependa niyazungumze ambayo ni machache sana naomba nichukue nafasi hii nimshukuru sana Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, nasema hivyo kwa sababu alitutembelea katika Mkoa wetu mwezi wa nne na alifanya kazi kwa kweli ambayo wananchi wa Jimbo la Bukoba Mjini walinambia kwamba nikija hapa Bungeni nitoe shukrani zao kwake kwa sababu ya kasi yake na kazi aliyoifanya na hasa *style* yake wameniambaia hii niiseme hadharani *style* yako ya kuwaweka watu *on the spot. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake wakati wananchi wanaeleza matatizo yao basi unataka wawajibikaji ambao ni viongozi waeleze mbele yako kulikoni. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya watu wa Jimbo langu la Bukoba Mjini na niseme kwamba tunakushuru sana na tunakukaribisha uje tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nichukue nafasi hii kwa kweli kwa kuwa niko katika *television* niwape pole watu wangu wa huko Bukoba katika sehemu ya Nyamkazi katika Jimbo langu ambalo wameunguliwa nyumba, wako watu 116, nyumba zao zimeungua wiki iliyopita na viongozi pale wa Wilaya na Mkoa wanajitahidi kuona ni nini wafanye kuweza kuwasaidia. Kwa hiyo, niliungana nao kwa hiyo bado hapa natoa pole kwa watu hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nimshukuru Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, wakati alipokuwa anataoa taarifa yake imeeleza karibu kila kitu na Waheshimiwa Wabunge wamezungumza mengi kwa hiyo, nisingependa kurudia rudia na nadhani nitapata nafasi nyingine wakati tutakapo tunatizama Bajeti za Wizara mbalimbali kuweza kuweka michango yetu. Lakini kubwa ambalo ningependa niliwekee mchango wangu ni utaratibu wa Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa Bajeti zinavyokuwa *presented* katika Bunge hili na mchango wa Wabunge katika Bajeti hiyo ambayo ni Bajeti kwa kweli ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema kwamba tangu mwaka 1962, naweza kusema kwamba Bajeti zimekuwa zinakuwepo. Suala la kujiuliza nafikiri mwaka hadi mwaka wakati Bajeti zinavyokuwa *presented* na Serikali hizi Bajeti zinatizamwa vipi na kunakuwa na mchngo upi wa wananchi ama Wabunge katika Bajeti hizi? Hilo ndilo suala mimi ningependa kulizungumzia zaidi. Kwa sababu maamuzi ya Bajeti kwa kweli nisingependa mimi mwenyewe kuyatizama kwa urahisi kwa sababu ni maamuzi ambayo yana-*affect* kila Mtanzania katika maisha yake. Lakini kubwa zaidi yana-*affect* hata wale ambao si watanzania lakini wangependa kuja kushirikiana na watanzania hasa katika kufanya biashara. *(Makofi)*

Sasa tunatizama hii Bajeti jinsi inavyotengenezwa. Mimi kwa mtizamo wangu nadhani *in simplified way* nasema kwamba Bajeti ya Serikali inatueleza kama alivyofanya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwamba inahitaji pesa kiasi gani. *This is what they are telling us,* wanatuambaia kwamba wanataka pesa kiasi gani, lakini

wanatuambia kwamba wanataka pesa kiasi gani na wakishatuambia wanataka pesa kiasi gani lakini hapo hapo wanatuambia ni katika maeneo gani wangependa wazitumie hizo pesa.

Sasa kuna suala la pesa, kuna suala la maeneo lakini sasa linakuja suala lingine, hizo pesa zipatikane wapi? *Where do they get that money?* Ukitizama njia za kupata pesa hizo kwa kweli ni finyu, ukitizama uchumi wa nchi yetu na mahala pa kubwa zaidi ni mahala pa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi ziko za aina mbalimbali, lakini ziko za *income tax* ambazo watu wanalipa ziko kodi za wafanyabiashara ambazo wanalipa lakini hazitoshi kodi. *Then* kuna eneo lingine ambalo linakuwa ni eneo la kutafuta mikopo na nafikiri Serikali inakopa kuweza kujaza jaza katika Bajeti yake. Lakini wanakopa na haya yanakuwa ni madeni wakati mwingine yanakuwa ni madeni ambayo Serikali haiwezi kulipa lakini ni madeni yanakwenda katika kizazi kijacho.

Lakini hapo hapo lipo eneo lingine la kuwategemea wahisani kuona wahisani watachanga vipi katika Bajeti yetu kwa hiyo, mimi nayaona kwa haraka haraka ni maeneo matatu. Hizi *source* za kuweza kutengeneza Bajeti yetu, lakini kubwa zaidi ni kiasi gani cha fedha Serikali, inataka kwa matumizi yake lakini katika maeneo gani pia.

Sasa maamuzi haya mimi ninasema tumekuwa nayo kwa muda mrefu na tumeiachia Serikali peke yake wakati umefika wananchi kupitia kwa Wabunge wao wapate fursa ya kutizama hii Bajeti ya Serikali kwa kina kwa kweli kwa sababu ukitizama kalenda yetu ya kutengeneza Bajeti, ni kalenda ambayo ina bana sana huu ni mwezi wa sita tunayo Bajeti hapa, mwaka wa fedha wa Serikali unaanza tarehe moja Julai, vizuri sana tutakuwa na Bajeti ambayo maamuzi yamekwishafanywa ingawa kweli tunaizungumzia Bajeti na ukiitizama ikija kufika mwezi Desemba Wizara zitakuwa zimeshaanza kutumika hapa na pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ikianza mwezi Februari mwaka ujao *process* nzima *machinery* nzima ya Serikali inaanza kutengeneza Bajeti ya mwaka unaofuata, lakini unakuta kwamba mimi nasema *pressure* ni kubwa. Sasa nimeona nizungumzie hilo peke yake maana yake mengine mimi nitazungumzia katika maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningependa nitoe mifano midogo, kwa mfano Waingereza ambao sisi tumerithi *system* yao kwa sababu hawa ndiyo wakoloni walikuwa watawala wetu kwa hiyo walituonyesha jinsi ya kutengeneza Bajeti. Lakini ukitizama sasa hivi Waingereza wame-*move away* wanautaratibu tofauti Bajeti yao inapita Machi kila mwaka ndipo Bajeti inapopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla ya hapo mwaka unaobaki tuseme kwa mfano Novemba ambao wao wanaiita *Mini Budget proposal* inawekwa katika *House of Commons* inazungumzwa pale na *infact* wanaizungumza kwa undani sana. Inaanza Novemba inakuja Desemba, Januari, Februari mpaka Machi na inakuwa *the first Tuesday*

ya mwezi Machi na siku hizi imekuwa W*ednesday* kwa hiyo, hakuna uhakika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, inakuwa ni mwezi Machi kwa hiyo, kuna kipindi cha kutosha kwa *House of Commons even House of Lords* lakini kwa kuitazama sana ile Bajeti nakuona kwamba mawazo ya wananchi ya watu wanaowakilisha yanakuwa *reflected* katika bajeti hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hao ni Waingereza, utaratibu wao ni *more interesting*, Wamarekani mwezi Februari wa kila mwaka Rais anatoa Bajeti yake *to the Congress* na anapoitoa mwezi Februari ile Bajeti inachukuliwa na Kamati mbili za Bunge moja ikiwa ni ya *House of Representative* na nyingine ikiwa ni ya *Senate* na hiyo tunaizungumzia Februari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwezi Aprili zile Kamati za Bajeti zikishatizama mwezi Aprili unakuta kwamba Kamati zote mbili zinakuwa na mtizamo mmoja na zinapeleka mapendekezo yake katia *full house*.

Hawa wanakwenda katika *House of Representative* na hawa wanakwenda katika Senate, *Full House* na hiyo inakuwa mwezi Aprili. Wanaitizama, wakishamaliza, katika mwezi Juni, *both Houses* wanakuja na *resolution* moja ambayo inajaribu ku-*synchronise* na kuweza ku-*balance* na ku-*harmonise position* za hizi *Houses* mbili, *The House of Representative and The Senate*. Inakwenda mpaka mwezi Oktoba, ndipo Bajeti rasmi ya Marekani, tarehe 01 Oktoba, Bajeti inapitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unakuta mchakato mzima unaanza Februari na hakuna cha kuficha kwa sababu ni *proposal* zile. Hawa ni Wawakilishi wa wananchi, wanazitizama zile *proposal*, wanazizungumzia, wanaweka ambayo yanahitajiwa kuwekwa katika hiyo *proposal* na kui-*refine* vizuri na wanafanya vizuri, *both:* The *Government* inafanya kazi vizuri na hawa Wawakilishi wa watu wanafanya kazi vizuri. Unakuta kwamba kwa muda huo wakati wanapofika kupitisha ile Bajeti, inakuwa ni Bajeti ambayo imechukua mawazo ya Wawakilishi karibu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nadhani utaratibu, na hii naweza nikaendelea, kwa mfano Rais wa Ireland anakuja kuhutubia hapa keshokutwa na wao kuanzia mwaka huu Januari wamebadilisha utaratibu wao wa ku-*present* bajeti, vipi Serikali ina-*present* Bajeti yake katika Bunge lao. Kwa hiyo, mimi ninayo ya kusema mengi na kuweza kuweka mifano mingi.

Kitu ambacho ninashauri na hapa katika taarifa ya Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, jana alizungumza vizuri sana, nisingependa kurudia. Kwa sababu alisema kabisa kwamba inavyoonyesha utaratibu tulionao, Bunge letu halina *say* kubwa, wala halina *input* kubwa katika Bajeti. Unakuta Bajeti imekwishatengenezwa, inakuja kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba na ninawaomba wenzangu Wabunge, tuko hapa kuwawakilisha watu wetu huko na tupate nafasi iliyokuwa nzuri

kuweza kutizama Bajeti ya Serikali kwa sababu Bajeti hii ni Bajeti yetu na maamuzi haya ni maamuzi ambayo yanawagusa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nimeona nizungumzie hayo, lakini mengine nitayazungumza wakati tunachukua *sectoral budget*. Lakini la mwisho, naomba nimalizie kwa kuwaomba ndugu zetu wa upande wa pili, Sisi kama wao wanavyosema, Mheshimiwa Cheyo amesema sasa hivi kwamba wanataka ushirikiano. Nadhani hicho ni kitu kizuri, hakuna asiyetaka ushirikiano. Lakini, mimi ninaomba wakati mmo katika Bunge, taarifa zenu na mambo ambayo mnayasema katika Bunge kwa kweli yawe ni mambo ambayo ni ya ukweli, ya uhakika, kwa sababu Bunge siyo *Holywood*, hatuko hapa ku-*act*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko hapa kusema yale ambayo tunaona kweli yatapeleka nchi yetu mbele. Kama wenzetu kwa kweli wanaona wanayo majambo ambayo wanataka kuyasema, basi wayaseme hadharani, lakini wayaseme kama yalivyo. Lakini ni kitu cha aibu, Mheshimiwa umechaguliwa na watu, wameweka imani yao kwako, wamekupa *confidence* yao ukawawakilishe, unakuja hapa mbele ya hadhara hii katika nyumba hii, unaulizwa kwamba hilo ulilolisema unaweza ukalitetea ukalisimamia kwamba ni la kweli! Mwishowe unasema hapana siwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nasema Mheshimiwa Cheyo, tunapenda tufanye kazi vizuri na kweli tutafanya kazi vizuri. Lakini, naona bora na zuri zaidi tujaribu kuwa wakweli katika hoja ambazo tunatoa kwa sababu *at the end of the day* tuko hapa kumtumikia Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninashukuru. Ninaomba niseme kwamba ninaunga mkono hoja ya Serikali mia kwa mia.

**MHE. JUMA SULEIMAN NH'UNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii. Lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana kijana wangu kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais leo kuingia Bungeni. Nashangaa sana watu wanasema Mzee, huyu kijana kabisa huyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine ninaweza nikasahau. Nataka nianze kwa kuunga mkono hii Bajeti ya Serikali mia kwa mia. Baada ya kueleza hayo, niseme tu kwamba Bajeti hii ni nzuri sana, lakini hakuna kizuri kisichokuwa na kasoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti hii imezima kilio cha wafanyakazi wa nchi hii zaidi ya miaka kumi. Nilipokuwa naangalia takwimu, zimenitia moyo sana pamoja kwamba Mheshimiwa Ghasia hajasema chochote, lakini nina matumaini kwamba wafanyakazi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jumla watafarijika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ni ya wakulima na wafanyakazi na ndiyo alama ya jembe na nyundo. Tumeona wafanyakazi, tumeona wakulima. Lakini na wafanyabiashara nao wamefaidika katika Bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasononeka sana, kama nchi hii kwa muda wa miaka 40 imekuwa inasema ukulima au kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa letu, ndani ya bajeti hii uchambuzi wake siyo mzuri kwa wakulima. Yako mafungu yamewekwa tumeyaona yanazungumzia mbolea, lakini bado Serikali haikwenda kwa kina katika suala zima la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilimo hatulizungumzi sisi tu Wabunge, safari hii Mwenyezi Mungu alitukumbusha na ndiyo maana akaleta njaa. Nia yake alikuwa anaiambia Serikali kwamba Watanzania hivi sasa lazima muamke na muanze kuandaa mikakati thabiti mizuri kuhakikisha kwamba kilimo kinakuwa cha kisasa, mavuno yanakuwa makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu katika nchi yetu hii ya Tanzania kuomba au kutaka msaada kutoka Japan. Japan ni nchi ndogo sana. Lakini, kwa sababu wanalima vizuri, wanapanda vizuri, mavuno yao ni mengi. Ni aibu nchi yetu hii kuzungumza suala la ukame.

Kama tungekuwa na utaratibu mzuri wa kuvuna maji ya mvua, maji ya mvua yangevunwa vizuri yakahifadhiwa katika marambo na wakati wa kiangazi watu wangelima. Lakini sijui mpango huo uko wapi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hivyo tu, Watanzania tuna ardhi kubwa sana ya kilimo. Nimemsikia rafiki yangu hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu Lowassa alisema kwamba kuna hekta zaidi ya milioni 42 na hazijalimwa hata robo yake. Lakini, sioni utaratibu mzuri wa kumwezesha huyu Mtanzania kulima kilimo hicho cha kisasa. Nimeona tu maneno mazuri, mambo mengine, Bajeti, lakini hasa kilimo kwamba sasa tunataka kukiinua, hakuna!

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia nzima, Serikali zake zinatoa ruzuku kwa wakulima. Sisi tunatoa ruzuku kwa mbolea. Mbolea ya sehemu inakopelekwa hapajafanyiwa utafiti, ili mradi tu mbolea inaongezwa. Ardhi nyingine mbolea inayopelekwa haihitajiki. Inapelekwa mbolea ya chumvi chumvi, matokeo yake ardhi inaharibika zaidi. Kwa hiyo, tunaharibu mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali, kwa heshima na taadhima suala la kilimo irudi ilifanyie kazi. Sio lazima safari hii, lakini ilifanyie kazi na sisi au na wakulima waamini kwamba limefanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimefarijika sana na nilisherehekea, nilikaa chumbani kwangu siku nilivyosikia Mheshimiwa Waziri Mkuu ametangazwa jina lake Lowassa. Nilisherehekea si kwa sababu tu ya urafiki wetu mimi na yeye. Nilisherehekea kwa sababu Lowassa ni mfugaji. Yeye binafsi, Lowassa ana mifugo ya kutosha. Kama anakataa anisute! Lakini cha kushangaza, Bajeti hii sikuona palipozungumzwa uchambuzi wa mfugaji uko namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfugaji wa Tanzania anasambaa, anazunguka zunguka anaambiwa eti kazi yake kuhamahama. Mfugaji wa Tanzania kazi yake kuhamahama! Mtu ambaye anaweka mazingira mazuri, mbolea ya samadi, umeme ule sijui wa kitu gani, watu wanapikia unaleta gesi, maziwa yanatoka kwenye ng'ombe! Wamarekani, wao wanachunga ng'ombe kwa Farasi na wana jina lao, wanaitwa *cowboy*, leo Watanzania wafugaji wanaambiwa hama. Tunakwenda wapi? Hajui!

Ninaiomba Serikali kwa heshima na taadhima, wafugaji waangaliwe na wapewe heshima kubwa sana. Mifugo ya Tanzania siyo mifugo iliyokuja hivi hivi. Ile ni zawadi ya Mwenyezi Mungu. Tukiichezea zawadi ile, Mwenyezi Mungu anaweza akaichukua hatutaipata tena. Ole wetu! Ninaiomba Serikali katika suala la mifugo iliangalie kwa makini. Kama Waziri anayehusika hana utaalam wa mifugo, basi watafutwe wafugaji. Nilimwona Mheshimiwa Lowassa wakati fulani alikuwa Waziri wa hiyo Mifugo, anakwenda mwenyewe kuchunga ng'ombe wa wafugaji. Anavaa lile kofia, linaitwaje?! Eeh! Lowassa yupo, Mheshimiwa Waziri Mkuu kama uongo anisute! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo tuliyonayo ni zawadi ya Mungu kwetu. Ni vizuri Serikali ikaandaa mkakati wa hawa wafugaji. Kama wanahamishwa katika vyanzo vya maji, waambiwe waende sehemu fulani na hiyo sehemu itengwe, mabwawa yachimbwe vizuri, wahakikishe kwamba ndorobo wanaangamizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwapongeze viongozi wa Zanzibar. Zanzibar kule kwa kushirikiana na Umoja wa Mataifa, ndorobo wa mwisho alimalizika mwaka juzi. Sasa, nashangaa hapa mtu anaambiwa hapa hama, kwenye chanzo cha maji. Niende wapi mzee? Utajua mwenyewe! Alah! Hivi mimi kufuga kwa niaba ya Watanzania imekuwa kosa! Mfugaji aelekezwe wapi awe na mifugo yake, wawepo na Madaktari wa kutibu hawa ng'ombe na ndipo utakapompa ushauri wa kutumia mifugo yake vizuri, ataitumia. Lakini wewe unamwambia hama, ondoka mazingira yanaharibika! Halafu unamwambia punguza ng'ombe, atakwambia na wewe jipunguze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi unaambiwa punguza ng'ombe, akikuuliza wewe kwenye akaunti yako unapunguza Shilingi ngapi? Utamjibu vipi? Maana na wewe anajua huna ng'ombe, ng'ombe yeye ndiyo mazao yake na fedha zake na akaunti yake. Wewe akaunti yako mbona hatuzungumzi namna ya kuipunguza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba sana hili suala la kilimo, kwa ufupi, utafiti wa mifugo, lakini sijapata pia ufafanuzi wa suala zima la uvuvi!

Hapa Tanzania ukizunguka hapo kuna meli zaidi ya hamsini za nje zinavua bila ya kibali na samaki wetu wanaovuliwa hapa Tanzania wanakwenda nchi za nje na wanauzwa kwa bei kubwa sana. Lakini, sisi wenyewe Watanzania, wanapungua protini, samaki hawaonekani, bei juu. Mkakati wa kuvuna hii rasilimali ya uvuvi uko wapi? Au tunaambizana tu mambo yetu mazuri! Bajeti safi na kila kitu. Mvuvi nenda kavue kwa jarife au kwa kitu gani, hakuna utaratibu. Lazima tuondoke hapa tulipo.

Tumekubaliana kwamba hii ni karne ya sayansi na teknolojia na Taifa letu tulielekeze huko, mvuvi avue kisasa, mkulima alime kisasa, utafiti ufanywe vizuri, vyombo vya kisasa viwepo. Hayo ndiyo maana ya uhuru. Siyo leo mvuvi, mkulima bado anavua kwa mtindo wa miaka mia iliyopita, analima kwa jembe la mikono. Tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, kwa heshima na taadhima, Bajeti hii tutasameheana, lakini ijayo tutaulizana, mmefika wapi! Tumepewa kuongoza nchi hii na wenzetu wakatuchagua wakatuamini. Lakini kwa mamlaka na nguvu za Mwenyezi Mungu na kesho Mwenyezi Mungu atawauliza Wabunge, atauliza Serikali, mliwasaidia kiasi gani wenzenu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze kidogo kuhusu uchumi hasa uchumi wa Zanzibar. Kabla sijasema, ninataka nimnukuu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano alipokuja katika Bunge. Alisema hivi: "Nitaangalia upya mchango wa Serikali ya Muungano katika maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii ya Zanzibar bila kuathiri haki na mamlaka kamili ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mambo ambayo siyo ya Muungano."

Sasa hili nimeliangalia humu, nimekuta ule mgawanyo tu wa misaada kutoka nje, sasa hivi Zanzibar inapata mtihani mmoja, mtihani mmoja uko kwenye Muungano. Lazima unapokuwa katika Muungano, uridhie na mambo ya mwenzio hata kama hayo siyo wewe yanayokufaidisha. Lakini, keshokutwa tunaingia katika Afrika Mashariki. Tunazungumza Afrika Mashariki na kila kitu. Tunasema, Mwalimu alisema kwamba kuna hatari nchi ndogo ikamezwa na kubwa. Lazima tuambiane ukweli, nchi ndogo ikamezwa na kubwa.

Zanzibar hivi sasa hali yake ya uchumi siyo nzuri tukubaliane ndugu zangu. Siyo nzuri, pengine kwa sababu hakuna namna ya kutoka pale, maana kodi zinazowekwa hapa na Jamhuri ya Muungano, ndiyo kodi zinazotumika Zanzibar. Hivi tunaulizana, wananchi wa Zanzibar tuseme wako milioni moja. Kama kuna tajiri anaamua kuleta televisheni milioni moja, basi ina maana kila mmoja lazima anunue moja moja mpaka mchange, zitakazobakia kama milioni mbili atanunua nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima tukubali kwamba wananchi wa Zanzibar kwa vyovyote vile uandaliwe mkakati, soko lao liwe Tanzania Bara. Tukubaliane hivyo. La sivyo, viwango vya kodi vya Zanzibar viwekwe vya tofauti, na kama siyo hivyo ujengwe mkakati maalum wa kusaidia. Kwa mfano, Afrika Mashariki kuna mambo mengi hivi sasa yanakuja na yatasadia Jumuiya ya Afrika Mashariki na yatasaidia hao wananchi milioni 30. Lakini hao watu milioni moja ambao wako pale Zanzibar wanasaidiwa vipi? Wanafaidika vipi na Muungano? Maana wananchi wa kawaida hawataki Uwaziri Mkuu hawataki Ubunge, hawataki Uwaziri, wao wanataka kufaidika na maisha yao vizuri. Hali za wale Wazanzibari wale sio nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia ya kwanza ambayo ningeomba, Bandari ya Zanzibar iwe bandari huru katika Afrika Mashariki na Afrika Mashariki ikibali kwamba

Bandari ya Zanzibar ni Bandari huru ili ifanye kazi ya kupokea mizigo yote ya Afrika Mashariki na baadaye isambae katika Afrika Mashariki. Wazanzibari wale watapata kazi na suala la uchumi litakua na Serikali itajiendesha na mgogoro utakuwa hakuna. Si tunagawana! Wewe, kilimo wewe ardhi yako nzuri, wewe na nini, wewe na soko, lakini na wale nao watapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili sijui limefikia wapi! Nilitaka hilo na lenyewe niliweke hapa ili pengine Serikali itakapofanyia kazi, lifanyiwe kazi. Sio lazima lipatiwe jibu. Mnaweza mkalifanyia kazi huko baadaye, sio lazima mseme msimamie. Semeni nyie ndiyo mliosema. Kwa sababu wadogo hawaambiwi hili kasema fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninataka niliseme ni suala la Utawala Bora. Suala la Mihimili Mitatu:- Mhimili Bunge, Mhimili Mahakama, Mhimili Serikali. Kwa muda wa miaka 40 Bunge, Mahakama, vimetiwa mfukoni na Serikali.

Sasa, Mheshimiwa Rais ana maneno mazuri alisema hapa na nilikuwa namsikiliza na nafuatilia sana. Katika ukurasa wa 22 wa hotuba yake, alisema hivi: "Serikali nitakayoiongoza itazingatia na kuendeshwa kwa msingi wa utawala bora, uwazi na uwajibikaji. Tutaheshimu utawala wa sheria na tutazingatia na kuheshimu mgawanyo wa madaraka kati ya mihimili mikuu ya dola yaani Utawala, Bunge na Mahakama. Tutaheshimu uhuru wa Mahakama na Bunge na tutatimiza ipasavyo wajibu wetu na tutawezesha."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ukitizama wenzetu wa Serikali na Bunge na Mahakama, kweli tuko sawa sawa! Tukubaliane! Wenzetu wa Serikali wanakusanya kodi na kupanga mikakati. Maana yake mpaka hili Baraza la Mipango na kila kitu wanakubaliana huko, sisi tunaletewa hapa tupitishe Bajeti. Lakini vipaumbele wamepitisha wao. Wanatutia mfukoni wenzetu. Sasa hilo ni jambo ambalo linatakiwa kusawazishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, Bunge na Mahakama sio chombo cha kuipigia magoti Serikalini katika kuomba Bajeti yake. Kama mwenzio ana uwezo mkubwa na wewe huna uwezo, uhuru huna. Kama yeye anakusanya kodi na halafu wewe unapiga magoti, maana yake Ofisi ya Spika, Bajeti yake iko chini ya Mkurugenzi ambaye yuko Ofisi ya Waziri Mkuu. Sasa, mtaendeshaje mambo yenu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kutamka kabisa kwamba naiunga hii hoja mkono. Pili, nikupongeze kwa kukalia kiti hicho, *cover* yake ya nyuma inafanya tusikuone wakati umekaa hapo, lakini umejaa kwenye kiti hicho vizuri. Hongera sana kwa kukikalia kwenye Ukumbi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Ndugu yangu Yusufu Makamba kwa kuteuliwa kuwa Mbunge. Tumempokea leo asubuhi, ameapishwa na Spika, ni mwenzetu, tunamkaribisha sana. Nasi wa Dar es salaam tunamshukuru sana Rais kwa

kutuongezea Mbunge mwingine mmoja ambaye ni Mkuu wetu wa Mkoa, kwa hiyo tukishayazungumza hapa tukirudi Mkoani, ni kwenda kutekeleza. Tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ninaomba niupongeze sana uongozi wa juu wa hii Awamu ya Nne. Tumeona walivyoshughulikia matatizo makubwa yaliyotupata, walivyoshughulikia njaa. Hongereni sana. Tunaona wanavyoshughulikia ukame na ukosefu wa umeme, tuliona walivyotujali na kutushughulikia tulipopata ajali. Tunawashukuru sana kwa kutujali, ahsanteni sana endeleeni hivyo.

Tunawashukuru pia kwa kuendelea kujenga kwa misingi ile ambayo ilishajengwa huko nyuma, maana nchi hii ni moja na awamu moja itajengwa juu ya awamu nyingine. Kazi za kujenga barabara zinaendelea. Rafiki yangu Mheshimiwa Magufuli alituambia kwamba baada ya muda sio mrefu tutasafiri kwa taxi, nafikiri alikuwa na maana ya gari dogo, kutoka Mtwara mpaka Mwanza. Natarajia siku hiyo itafika, maana kazi zinaendelea kufanyika kwa bidii kabisa ili tuweze kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hotuba ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Nne. Nami naiunga mkono hotuba hii kwa sababu imejielekeza katika yale mambo makuu ambayo tumewaahidi wananchi wa nchi hii kupitia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na kupitia ahadi za Wabunge waliomo ndani humu ikiwa ni pamoja na Rais wetu, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu.

Hotuba hii inatufanyia mambo mengi sana ambayo hayajawahi kufanyika kwa wananchi. Kwa mara ya kwanza nafikiri tumepania kuongeza mishahara ya wafanyakazi kwa kiwango cha kuridhisha. Mfanyakazi wa Tanzania analipwa mshahara mdogo na tulipoona umekuwa mdogo sana tulimruhusu afuge na kulima aendelee kutufanyia kazi.

Sasa, nafikiri tunalenga kuhakikisha kwamba anapata kipato kitakachomwezesha kutumia sehemu kubwa zaidi ya muda wake katika kulitumikia Taifa hili kama ilivyotegemea. Nategemea pia kwamba baada ya marekebisho haya, basi kila mwaka marekebisho yatakuwa yanafanywa ili kufidia punguzo lolote litakalotokana na mfumuko wa bei au matatizo mengine yoyote ya uchumi yakaayotokea ili mfanyakazi huyu apate kipato cha kumwezesha kuishi kwa gaharama zilizomo katika nchi kwa hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii vile vile, zaidi ya kuongeza mishahara, imepunguza kodi za kuturahisishia maisha mpaka *VAT* imeondolewa kwenye petroli kwa kile alichotueleza Waziri, bila kupunguza mapato ya Serikali. Nafikiri kuna miujiza hapa. Nitaomba atueleze ataondoaje kodi ya *VAT* kwenye mafuta na bado mapato yake yasipungue. Lakini kodi hizi zimepunguzwa ili kumwezesha mwananchi kumudu gharama za maisha kwa uzuri zaidi. Njia ya kumsaidia mwananchi ni kumpa kipato, lakini kama huwezi kumpa kipato, kumpunguzia gharama ambazo yeye mwenyewe lazima alipe, Bajeti hii inatufanyia hivyo. Imetuondolea kodi kwenye gesi, lakini tungeomba iondoe kodi kwenye majiko ya kupikia, pia ya umeme na ya gesi, maana gesi peke yake ikiondolewa kodi wakati jiko lenyewe halipatikani, matatizo yetu yatabakia pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hatua mbali mbali zimechukuliwa kuhakikisha kwamba tunalinda mazingira. Kwa hiyo, zimechukuliwa hatua za makusudi kabisa za kupunguza uharibifu wa mazingira na hizi nazipongeza kwa dhati kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, nawapongeza Mawaziri waliowasilisha Bajeti hii hapa Bungeni. Wamefanya kazi nzuri, ndugu yangu Mheshimiwa Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Zakhia Meghji wamefanya kazi nzuri sana kutueleza nini Serikali inakusudia kufanya katika mwaka ujao na hata Upinzani umekubali kwamba Bajeti hii ni nzuri na kwamba tutashirikiana katika kuitekeleza. Nawapongeza pia Ndugu yangu Abdallah Kigoda pamoja na wazungumzaji wengine wote walionitangulia kwa michango yao yote waliyotoa ambayo imeendelea kuboresha shughuli hizi zilizoko mabele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kuna maeneo ambayo nina matatizo nayo kidogo ningeomba nisaidiwe baadae. Reli ya Kati ilijengwa na Mjerumani zaidi ya karne moja iliyopita kwa teknolojia iliyokuwepo wakati ule. Leo tukienda kwenye reli ile tunakuta reli zile zile alizoacha Mjerumani zikiwa zimeandikwa majina yale yale ya Kijerumani. Imefika mahali, reli hii imechoka kiasi kwamba hatuanzii tena safari Dar es salaam, sasa hivi tunaanzia Dodoma. Nafikiri kuna haja ya kuwa na mpango wa makusudi wa kuangalia hii Reli ya Kati, kuipima na kuipangia mpango mpya kwa kuijenga, tena ijengwe kama kitega uchumi cha kuhudumia Mikoa ile inayohudumiwa na reli hii pamoja na nchi za jirani, ikiwa ni pamoja na Kongo, Rwanda, Burundi, naambiwa hata Zambia kwa kutumia meli kwenye Ziwa Tanganyika wangeweza wakatumia reli hii.

Ningeomba Serikali ya Awamu ya Nne iliweke hili kama moja ya changamoto ambayo wataishughulikia na kuikamilisha katika miaka kumi ijayo ili tuwe na reli mpya ya kisasa yenye kasi mpya na yenye uwezo mpya , nguvu mpya ya kubeba mizigo kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma. Tukijenga vizuri, mtu ataweza akatoaka Dar es Salaam asubuhi, jioni akafika Kigoma. Wale ambao wamekwenda Japan, moja ya mambo wanayojivunia sana ni zile *bullet train* zao zinazokwenda zaidi ya kilomita 250 mpaka 300 kwa saa. Sasa ukikimbia mwendo huo, haitakuchukua zaidi ya nusu siku kufika Kigoma. Nasi hatutaki hata kwenda kwenye 300/400 kwa saa, twende mwendo ambao tunaumudu na mizigo ibebwe kwa kasi hiyo ili kutufikisha huko.

Naomba sana Serikali ilitazame hili na ilitilie maanani katika mipango yake ya miaka mitano. Kwa upande wa barabara, tumejitahidi sana. Sasa hivi barabara zetu nyingi zinapitika vizuri. Utatoka Dar es Salaam kwa kasi unayotaka mpaka Dodoma hapa. Tunaendelea kujenga kuelekea Mwanza, tunajenga kuelekea Mtwara, barabara ya Zambia inapitika vizuri. Hongereni sana kwa kazi nzuri sana ambazo tumefanya. *(Makofi)*

Lakini, hili suala la reli hatujalitilia mkazo unaostahili. Hii reli ndiyo ingewezesha mizigo mizito kubebwa kutoka Mwanza, Shinyanga, Tabora, Mpanda na maeneo mengine yote haya kufikishwa bandarini Dar es Salaam ili kusafirishwa. Baadaye tukimaliza Reli ya Kati, tungeangalia ile reli ya Tanga ambayo Uganda wametaka sana

ijengwe ili waitumie kupitisha mizigo yao kupeleka kwao. Kwa hiyo, hivi ni vitega uchumi ambavyo tukivijenga, vitalipa vyenyewe.

Kwa hiyo, ningeomba wakati huu ambapo hatujamaliza kubinafsisha ile reli, tufikiri upya na hata kama ikibidi tuende kwa kasi ndogo zaidi ili tuibinafsishe katika njia itakayotupa kile ambacho tunahitaji. Ningeomba sana hili lizingatiwe kwa ukamilifu kwa kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naomba litazamwe, tumepewa taarifa hapa Bungeni mara kwa mara kwamba kuna mipango ya kutumia makaa ya mawe kuzalisha umeme. Lakini kungekuwepo vile vile na mpango wa kutumia makaa ya mawe kwa ajili ya matumizi ya nyumbani badala ya kukata miti na kuchoma mkaa. Tunaambiwa tuna makaa ya mawe mengi sana katika eneo la Kusini linaloanzia Ruvuma, Iringa mpaka hata sehemu za Mbeya. Mwenyezi Mungu katupa baraka hii, katupa mali hii iko ardhini kwa miaka yote hii haitusaidii.

Kuna mipango tayari imeishafanyika, Kiwira wanazalisha umeme, lakini kungefanyika mipango mikubwa zaidi ya kutumia makaa ya mawe kwa wingi zaidi na hata ikiwezekana kuuza ziada nje. Lakini tuna chuma ambacho kiko karibu sana na makaa ya mawe. Kwa hiyo, tungeweza tukawa na mipango miwili, mmoja wa kuchimba makaa ya mawe na kuyaanda kwa matumizi ya ndani na kuuza nje, lakini wakati huo huo tukachimba kile chuma nacho tukakitengeneza ili kiweze kuuzwa nje. Nitaomba katika mipango tutakayoelezwa na baadaye tutakapozungumza katika Wizara mbalimbali, tutalitazama hili kuangalia ni vipi tufanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine la mwisho, napata tatizo sana na Miji ya Tanzania. Tanzania ni nchi mbayo ina Miji ambayo haikupimwa. Dar es Salaam zaidi ya asilimia 75 haikupimwa. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwamba hatujapatwa na majanga ya vimbunga kama yanayoikumba Marekani, tungepoteza maisha ya watu wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna haja ya kuangalia Miji yetu na kuweka mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba Miji hii inapimwa na inajengwa kwa utaratibu wa watu wengi kuishi pamoja, kwamba Miji hii inajengewa huduma. Ninapotembelea Jimbo langu Makurumla, sijui Mabibo, Manzese, jambo moja linalonisikitisha kupita kiasi ni kukosekana kwa mifumo ya maji ya maji machafu na hata kukosekana kwa maji yenyewe ya kutumia. Kwa hiyo, kuna haja ya kuweka mpango wa makusudi ili ikae inavyopaswa kuwa. Kwa sasa Miji yetu ni mahali pa hatari sana pa kuishi na ambapo panaweza pakawa chanzo cha kueneza magonjwa.

Katika Jimbo langu, yakikosekana maji siku mbili-tatu, kipindupindu kinalipuka. Kikishalipuka, wale wanaosafiri kwenda Mikoani wanapeleka unasikia na huko Mikoani kunatokea milipuko maeneo mbalimbali. Hii inatokana na kwamba mipango yetu haiendani na kukua kwa hii Miji. Tunajenga Miji isiyokuwa na barabara. Miji tunajenga ambayo watu wanajenga kwenye maeneo ya mabondeni kusikowezekana hata kuchimbwa vyoo. Ni hatari kweli kweli kama hatutaishughulikia Miji hii.

Lakini moja nafikiri ni gumu hata kuliko hata mengine. Tunaposhughulikia matatizo katika nchi tunachukulia kwamba watu wa Mjini wana nafuu. Juzi tulikuwa tunashughulikia suala la njaa hapa, watu wa Mijini wana njaa sawa sawa na wenzao wanaoishi Mikoani. Wana umaskini sawa na wenzao wanaoishi Mikoani, kuna wachache wenye nafuu wanaofanya biashara kubwa. Tunapoangalia pato la Miji linaonekana ni kubwa kwa sababu ya viwanda na shughuli nyingine za kibiashara zilizopo katika Miji, lakini wananchi wetu wengi wana matatizo makubwa sana.

Naomba katika mipango ijayo tuwe tunaangalia vile vile katika Miji tutafanya nini ili tuweze kusaidia kupunguza umaskini tuweze kusaidia kuhakikisha kwamba huduma zinazopatikana ni za kukidhi na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuhimiza Elimu ya Sekondari. Sisi wa Dar es Salaam tulikuwa nyuma kabisa. Kutokana na jitihada zake sasa asilimia karibu 73 ya watoto waliomaliza Darasa la Saba na kufaulu watakwenda Sekondari. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Lakini tunahitaji mipango ya kudumu na mikubwa ya kushughulika na hii Miji na katika kila Mji uwepo mpango mkubwa wa kuendeleza Mji ambao ndiyo utakaofuatwa badala ya kila mtu kujipimia kiwanja na kujenga anavyoona inafaa. Tusipofanya hivyo, tutafika mahali Miji hii itatupa matatizo na tutakosa hata kwa kuhamia maana matatizo hayo ukiyakimbia Dar es Salaam utayakuta Dodoma, ukikimbia Dodoma ukifika Mwanza utakuta kule ndiyo yameota pembe kabisa.

Tunaambiwa na Mkutano unaendelea *vancouver* hivi kwamba katika mwaka huu tayari nusu ya watu wanaoishi katika dunia wanaishi Mijini na wingi wa watu wanaohamia Mijini ni katika nchi kama za kwetu zinazoendelea. Kuna haja ya kuweka mipango ya kuhakikisha kwamba mazingira yetu katika Miji ni mazingira yanayolingana na mahitaji ya watu wengi kuishi pamoja. Barabara katika Miji mingi sana hazipitiki pamoja na juhudi ambazo sasa hivi zimeanza kufanywa lakini barabara nyingi hazipitiki. Inafikiriwa tu kwamba hii Miji kwa miujiza fulani itajiendesha?!

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nimalizie hapo, niwaachie na wenzangu wachangie na narudia kuiunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niungane na wenzangu kuchangia mada iliyo mbele yetu, nayo ni Bajeti ya Mipango ya mwaka 2006/2007. Awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru wananchi wa Tabora Mjini kwa kunipa fursa hii ya kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Vile vile, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais, Mawaziri na Wabunge wote kwa ushindi mkubwa waliopata. Aidha, napenda kutoa pongezi mahususi zimfikie Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Mipango kwa hotuba zenu nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naanza kuchangia katika ukurasa wa 41 wa Hotuba wa Waziri wa Mipango. Anapozungumzia kwamba katika kipindi cha mwaka 2006/2007 tutaendeleza utekelezaji wa mradi maalum wa kuboresha miundombinu katika Mikoa sita iliyotajwa pale, nataka kusisitiza neno kuboresha kwa upande wa Mkoa wa Tabora, hatuzungumzii kuboresha, tunataka kuzungumzia kujenga na hii ndiyo ahadi iliyoko kwenye Ilani ya Chama ya Uchaguzi. Vile vile ilisisitizwa na Mheshimiwa Rais, alipotembelea Tabora wakati wa kuwashukuru wananchi wa Tabora, alisema tutajenga barabara ya Itigi -Tabora na Tabora - Nzega. Kwa bahati mbaya haya hayaonekani katika mpango wetu tunaoujadili. Kama yanaonekana yanaonekana kwa kubabaisha kama yalivyo kwenye ukurasa huu nilioutaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 20 wa kitabu cha Bajeti, kwa maana ya Hotuba ya Waziri wa Fedha, naanza na pale katikati panapoainishwa jinsi pato la Taifa litakavyokua. Sasa hivi tunaambiwa linaanzia kwenye asilimia 5.9, litakwenda mpaka kwenye asilimia 7.7 mwaka 2008. Huu ni utani. Ukichukulia yote yaliyosemwa, sasa tuko kwenye asilimia 5.9, kufika mwaka 2008 tutakuwa kwenye asilimia 7.7, maana yake *business as usual* na tukikua kwa kasi hii hatutajikomboa katika tatizo letu la umaskini.

Naendelea pale chini tunapewa ukusanyaji wa mapato ya ndani kwamba ni sawasawa na asilimia 14 ya pato la Taifa. Ningependa kufahamu asilimia 14 ni sawa? Tuko chini kiasi gani na hali halisi? Wenzetu wa Kenya, Uganda wanapokusanya mapato yao yako sawa na asilimia ngapi ya mapato yao ili tuweze kujua kama kipimo hiki kitatusaidiaje kuendeleza juhudi au kupunguza juhudi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la *interest rate disparity* katika mabenki yetu. *Deposit rate* chini *lending rate* juu. Suala tunalopaswa kujiuliza ni kwa nini? Ziko sababu nyingi lakini sababu moja ni kwamba mabenki yetu yana *operate* katika mazingira magumu sana. Wakopaji wengi hawalipi. Wakipelekwa Mahakamani kesi haziamuliki kwa muda mfupi na *injunction* juu ya *injunction* zinaendelea. Matokeo yake mabenki yetu yanakua na vile vinaitwa *non performing assets* katika vitabu vyao katika viwango vya hali ya juu. Katika kujaribu watafidiaje hizo *non performing asset* ndiyo maana inakuwa ni moja ya kielelezo cha *lending rates* kuwa juu. Tufanye nini? Kesi haziendi, Waziri wa Sheria yuko humu ndani, mabenki yanatoa *lending less,* Waziri wa Fedha uko humu ndani, kaeni mzungumze mabenki yako ili yaweze kuteremsha *interest rate* kesi hizi ziishe, ama sivyo ni matatizo. *(Makofi)*

Kumeanzishwa *Commercial Court* ambayo inafanya kazi yake kwa *speed* ya juu, lakini *Commercial Courts* ni ghali, pili hazipo nchi nzima ipo Dar es Salaam tu, vile vile hazichukui kesi za chini ya Shilingi milioni 50 na kesi za wale wanaodaiwa na mabenki ziko katika viwango hivyo. Kwa hiyo, hilo nalo inabidi kulitazama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu hali yake ya uchumi siyo nzuri. Hii inadhihirishwa na *trade account* yetu ilivyo, tuna *deficit* kubwa sana. Tuna *export* nusu tu ya thamani ya *imports* zetu na nchi yetu ni nchi ya wakulima na wafanyakazi. Hii ni nchi moja ambayo asilimia 85 ya idadi ya watu wake wanaishi mashambani kwa kilimo na

kufuga. Wao asilimia 85 hawawezi kujilisha wenyewe na kuwalisha asilimia 15 wanaoishi Mijini. Kuna tatizo kubwa sana. Iweje watu asilimia 85 mshindwe kuwalisha watu asilimia 15? Maana yake ni kwamba kilimo chetu kiko nyuma mno.

Wenzangu waliotangulia walisema hili na nalikazia tu kwamba ni pale tutakapoweza kukipa kilimo kipaumbele kinachostahili na siyo kwa ujumla, leo asubuhi msemaji mmoja alisema tuwe *selective*. Kuna maeneo ambayo tukipeleka nguvu zetu kwa dhati tutajikomboa. Lakini tukiendelea tu hivi hivi kwamba holela, kilimo wote, tukimwagilia wote, hapana. Tutie mkazo kwenye maeneo ambayo yatakuwa *specifically identified* kwa ajili ya kuongeza pato la Taifa. *(Makofi)*

Kwa ajili ya kufanya hivyo, naipongeza Serikali kwa kuanzisha mkakati wa kuanzisha Benki ya Kilimo na kwa maana hiyo Benki ya Maendeleo. Hakuna nchi inayoweza kuendelea kwa kutumia Benki za Biashara. Kama zilivyo Benki za Biashara, ni za biashara, haziwezi kumkopesha mkulima aende akalimie aka-*invest*, haziwezi kumkopesha *industrialist* aende akaanzishe kiwanda.

Kwa hiyo, Benki hii ambayo sasa Serikali inatafakari kuianzisha ilitakiwa ianze siku nyingi, tumechelewa. Tukimbie! Sasa kuna tatizo la mtaji, tunafanya nini? Sasa hapa ni suala la kukuna vichwa, tuna Shilingi bilioni 24 tayari katika Mfuko wa Benki inayotarajia kuwa Benki ya Maendeleo ya Tanzania. Zinatakiwa 50 na kitu, tufanye nini? Labda tuitishe pamoja na kwamba Serikali inaweza kuendeleza kutafuta fedha nyingine, lakini nilikuwa nafikiri tu labda tuitishe *shareholdings* kutoka mifuko ya *pension* nayo ichangie. Kama haitawezekana, basi Serikali itafute uwezekano wa kuongeza mfuko huu ili tuweze kuendeleza *housing loans*.

*Housing loans* nazo tumechelewa. Tanzania ni nchi peke yake katika Afrika Mashariki, siyo kama katika Afrika nzima ambayo watu wake wanajenga nyumba zao kwa fedha zao. Hili ni tatizo kubwa mno na ndiyo maana kuna kuna tatizo la rushwa, majumba yanayojengwa kwa fedha zao ni makubwa mno kuweza mtu kusema amelijenga mwenyewe. *(Makofi)*

Sasa hii Benki ya Nyumba wakati umefika imeanza kufanya kazi, tatizo ni kwamba sheria zetu za ardhi hazikuruhusu bei ya nyumba i-*operate* vizuri. Kwa maneno mengine tulifanya makosa kwanza kuivunja *THB* lakini hayo yamepita na yaliyopita si ndwele tugange yaliyopo na yajayo. *(Makofi)*

Sheria zetu za ardhi tumezirekebisha kwa kiasi fulani, lakini bado kuna Benki zimejaribu kutoa mikopo lakini zikawa zinashindwa. Mbia wetu mkubwa katika Benki ya *NBC, ABSA* kule Afrika Kusini *product* ya kukopesha kwa ajili ya kujenga nyumba ni moja ya *product* yake kubwa sana. Nashangaa hapa Tanzania haja-*introduce* na yeye ndiyo mwenye asilimia 70. *NBC* ni *ABSA,* kwa nini haanzishi hiyo *product?*

Tatizo liko kwenye Sheria zetu za Ardhi na jinsi hasa kama Benki kwa mfano ikishatoa mkopo itakapotaka ku-*foreclose* kwamba atayekopa ameshindwa kulipa

unaanza *process* eti ya kumuarifu kwamba, bwana, umeshindwa kulipa siku 60, zikipita siku 60 unampa *notice* nyingine ya siku 30. Sasa hivi *asset* ambayo ilikuwa ndiyo *security* kama huyu mkopo alishindwa kulipa ataacha ku-*temper* nayo katika kipindi hicho?! Hayo ndiyo mambo ya kuyaangalia katika sheria zetu ili tuweze kuwa na Benki ya Nyumba ambayo itatusaidia.

*Credit guarantee schemes* kwa *exports* na kwa mikopo midogo midogo ni uamuzi mzuri, lakini tumeiweka mahali pabaya Benki Kuu. Benki Kuu ni *institution* kubwa *(is a Central Bank)* kazi yake ni ku-*issue currency*, ku-*control reserve* za nchi na kutoa *licence* na ku-*supervise* mabenki. Tukiipa kazi yenyewe nayo kuwa-*functionally*, kuanza kupekua na kupembua, nani anataka apewe *guarantee*, nani asipewe *guarantee* tumeiweka siyo mahali pake. Tuipeleke kwenye Benki ya Maendeleo tunayokusudia kuitengeneza.

Kazi hii ya *export credit guarantee* na *loans guarantee* Benki Kuu kazi yake iwe ni ku- *supervise* tu na ndiyo kazi iliyopewa kisheria siyo kuwa-*direct functionally* kwa kusema kwamba natoa *guarantee* hapa namnyima huyu. *After all* hizi ni fedha za Hazina. Hazina azipeleke kwenye Benki ya Maendeleo, huko ndiko zinaweza kufanyiwa kazi vizuri zaidi. Aidha, kama ilivyo, mpaka sasa kuna matatizo ya utekelezaji wa hii mifuko miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie mambo ya viwanda. Tabora tulipata bahati ya kuwa na kiwanda kimoja kama chongo vile, kiwanda cha nyuzi. Kiwanda hiki ni moja ya viwanda vilivyojibu dhana ya ku-*export product* ambazo zimekuwa na *value added*.

Kiwanda hiki vile vile kinaweza kuuza nyuzi zake hapa nchini ambavyo vinaweza sasa kutengeneza nguo. Lakini inaweza tu kufanya hivyo ikiwa sheria zetu za kodi zitasaidia wale ambao wanatumia *grey sheeting*, aina ile ya nguo ambayo ni *roll* kutengeneza khanga, vitenge, fulana na kadhalika kama Serikali itahakikisha kwamba hizo *grey sheet* haziingii nchini kiurahisi kwa sababu zikiwekewa kodi ya kuingia nchini kiurahisi wale wanaotumia nyuzi kuifanya nguo ile *grey sheet* watakuwa hawana sababu ya kununua nyuzi za Kiwanda cha Tabora. Tukifika hapo kiwanda cha Tabora kimekufa. Kikifa maana yake hata zile ajira tunazosema tunataka kuzitengeneza hazitopatikana.

Leo hii baada ya kukifufua Kiwanda cha Tabora cha Nyuzi kina wafanyakazi 200 kwa *shift,* tatizo ni soko la ndani. Lakini wenye kiwanda wanaendelea kulitafuta, vile vile wanaendelea kutafuta ku-*export*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya na mengine ambayo nilitarajia kuyasema, nasema sasa naunga mkono hoja ya Bajeti yetu kwa asilimia 100. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kwanza na mimi nianze kwa kweli kuwashukuru watu wa Kigoma Mjini kwa kunichagua kwa kura nyingi na mimi kuwepo hapa leo. Lakini pia

kama walivyoanza wenzangu, na mimi niwapongeze Watoa Hoja, Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na mimi ninayo machache ya kuchangia katika Bajeti hii. Nikianza na Wizara ya Mipango, wakati nasoma kitabu hiki nikakuta ukurasa wa 34, wametupa *statistics* kwamba mwaka 2004 hekta katika kilimo cha umwagiliaji zilikuwa 23,900 mwaka 2005 zikapungua kuwa hekta 22,506. Lakini *page* ya 35 tunaambiwa kuna mkakati wa kufanya mapinduzi ya kilimo cha umwagiliaji. Sasa mimi nilitaka Waziri atusaidie hapa atuambie mikakati hiyo ni ipi na tuweze kuipima tuielewe. Maana mimi naangalia kwa sisi watu wa Kigoma Mungu ametubariki kweli kweli, tunalo Bonde la Mto Luiche. Bonde lile lina hekta zaidi ya 7,000, lakini ukienda kwenye vitabu vyote vya Bajeti huoni chochote kuhusu bonde hilo. Lakini hapa tunaambiwa tunataka kufanya mapinduzi na tunao mkakati wa kilimo cha umwagiliaji.

Kama walivyosema wenzangu, lazima twende kwenye *specific* sasa tuamue ni maeneo gani tuna-*invest, otherwise* hili suala la kwamba tunataka kuinua kilimo, itakuwa ni maneno, *a business as usual* kwamba lazima tuseme tuonekane na sisi kilimo tunakienzi. Lakini hivi, hatuwezi kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tunayo *vision* ya mwaka 2025 kwamba nchi hii tunapofika miaka hiyo itakuwa *semi industrialized*. Sasa mimi nikawa najiuliza, tumefika wapi sasa? Maana kama ni safari ya kutoka Dar es Salaam tunakuja Dodoma lazima tuambiwe sasa tumefika Chalinze na wote tuamini kwamba tumefika Chalinze. Maana kuna *index* ambazo zinatuonyesha kule tunakokwenda.

Kuna mambo ambayo mimi ningependa mimi niambiwe, kwa mfano *GDP gross, USD* yetu ikoje tulikofika sasa. Kuna suala la *GDP per capita, (USD)* tumefika wapi? Maana lazima tujue, maana tukienda tu kwamba kila siku tunaimba tunayo *vision* tutaimba maneno leo MKUKUTA, tutabadilisha maneneo mengi sana nia yake kufika 2025. Lakini lazima tuambiwe tumefika wapi kwenye hizi *index* za uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la *export*. Hakuna nchi iliyoendelea duniani bila ku-*export*. Leo matatizo tuliyonayo makubwa ya fedha yetu kushuka ni kwa sababu *export* zetu hazitoshi. Kwa hiyo, hatuna *USD* za kutosha. Hata leo tukisema *BOT* wa- *intervene* bado hatuwezi ku- *rescue* Shilingi yetu kushuka, kinachoweza kutusaidia ni *export* kupanda. Sasa tuambiwe, tuna mkakati gani wa kupandisha *export* yetu? Kwa bahati nzuri nchi hii Mungu ametujalia kila kitu tulichonacho *from* madini kwenda kwenye mazao, kila kitu kizuri nchi hii tunacho. Tumefika wapi? Tuambiwe na Waziri wa Mipango. *(Makofi)*

Lakini pia ili uende kwenye maendeleo haya tunayosema, lazima *(steel consumption)* tunatumiaje chuma? Tumefikia wapi sasa? Hakuna nchi inayoendelea duniani bila kutumia chuma, haipo! Lakini pia tuambiwe *power consumption, energy* yetu kama matatizo yetu ya *energy* ni haya miaka yote huko 2025 ni hadithi tu, hatuwezi kufika. Kwa hiyo, lazima tuwe na mkakati madhubuti wa kutekeleza suala la *power* nchi hii. *Energy is a crisis*, tukiliacha tunaua uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna suala la mwisho, *human development*, tuna plans zipi za kuendeleza wafanyakazi wetu? Tuna mpango upi? Tuambiwe na tuweze kuelewa.

Lakini pia nilitaka nimwombe Waziri wa Mipango aje na mkakati, atengeneze *priority list* ya nchi hii tuambiwe nchi hii tumeamua miaka hii mitano tunataka tufanye haya na naamini tutayakubali. Lakini tukifanya kidogo kidogo kila sehemu tunagusa *impact* haitaonekana. Unakwenda kwenye kilimo unafanya kidogo, kwenye mifugo unafanya kidogo, *tourism* unafanya kidogo, huku kidogo hutapata maendeleo mwisho wa siku. Kwa hiyo, naomba Waziri wa Mipango atuambie wakati anajibu namna ya kuyatekeleza haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Wizara ya Fedha. Nilikuwa naangalia *page* 37 na 29 wamepandisha bei ya *soft drinks, beer, wine, cigarettes,* sasa nikawa naangalia nafanya hesabu *rate* ya zamani na *rate* mpya nikaangalia nikaona vitu vyote kutoa soda peke yake ama *soft drinks* wamepandisha kwa asilimia saba lakini eti *soft drinks* wamepandishwa kwa asilimia 8.5. Jamani, hivi hata sigara, bia, mimi nadhani soda angalau hata watu maskini wanatumia soda ndiyo hiyo tumepandisha kwa bei kubwa. Sasa nikasema labda haya ni makosa ya uchapaji, Waziri atatuambia lakini sitaki kuamini kama ni kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo jambo langu kubwa ni moja tu ambalo ni barabara. Nataka tuongee tuelewane kuhusu barabara. Naamini nchi hii haiwezi kuendelea bila *infrastructure development*. Ukiangalia Ilani ya Uchaguzi unaona barabara ambazo zimesisitizwa vizuri sana kwenye Ilani ya Uchaguzi, lakini pia ukifuatilia hata Rais wakati anatembea nchi nzima kushukuru ameyarudia haya. Barabara ya kwanza ni Kigoma - Nyakanazi, Mwandiga - Manyovu, Kigoma – Tabora - Itigi - Manyoni, Kanyani - Mpanda, Mpanda - Sumbawanga, Tunduma - Sumbawanga, Mikumi – Kilosa - Handeni - Korogwe, Tanga - Horohoro, Bagamoyo – Sadani – Pangani -Tanga, Masasi – Tunduru - Mbamba Bay, Nyanguge - Musoma, Tabora - Nzega, Sumbawanga - Kasanga, Ipole – Koga - Mpanda, Nata - Mgumu Mto wa Mbu, Dodoma - Babati, Dodoma - Iringa, Mbeya - Makongolosi, Singida - Babati - Minjingu na Shanyanga - Bariadi mpaka Ramati. *(Makofi)*

Hizi ni kilomita zisizopungua 4,776. Tuna miaka 10 ya Rais wa Awamu ya Nne, tuna mikakati gani ya kujenga barabara hizi? Lazima leo tuamue tukubaliane tunapataje fedha za kujenga barabara hii. *(Makofi)*

Mimi ninaamini cha kwanza kabla hatujakwenda kuomba nje tufikirie wenyewe tunapataje fedha. Kuamini kwamba maendeleo ya barabara yataletwa na Wazungu, mimi naamini siyo kufikiri vizuri. *We are missing a point here*. Kuna barabara ukiziangalia nilizozitaja hapa kama hii ya Bariadi 40% ya *production* ya *cotton* inatoka huko. Ukienda Kigoma unapoongelea uchumi wa nchi hii ukitaka kuufungua maana yake una-*tape* uchumi wa *Eastern Congo*, Burundi na Zambia. *(Makofi)*

Lakini hakuna anayeliona hili. Hayupo! Tumeambiwa asubuhi hapa, pale Congo kuna mzigo zaidi ya tani milioni 70, lakini hakuna anayehangaika, wala hakuna linayemgusa. Mimi nasema haya kwa sababu najaribu kuangalia Bajeti zetu. Ukiangalia Bajeti zetu, haya ninayosema hayamo, *you don't see the serious commitment.* Lakini mimi nasema tatizo tulilonalo ni la fedha, tunafanyaje?

Ethiopia waliamua wao fedha yote ya *VAT* ya mafuta wanajenga barabara. Wameamua *road users* wajenge barabara. Hivi sisi tunapata kigugumizi gani? Naomba Waziri Mkuu, muamue leo kwamba kuanzia sasa kodi inayotokana na *petroleum product* tujenge barabara.

Baada ya miaka kumi, nchi hii tutaitana *round* nawaambieni, kwa sababu nikiangalia Bajeti hizi tunazowapa watu wa barabara napata taabu Bajeti ya mwaka huu ya barabara ni 43% ya *requirements* na hii ni barabara, nimetaja barabara mpya, tunataka kuanza, tunao (*back road maintenance)* tuna barabara za nyuma hatujakwenda za Vijijini. Ukienda kwenye Miji barabara *is pathetic*, Miji yote hakuna nchi ambayo Miji yake haina barabara kama nchi yetu. Barabara zetu ni mbaya jamani tukubali haya.

Sasa mimi nasema, kama hali ni hiyo tukubaliane tutumie fedha inayotokana na kodi za mafuta tujenge barabara, *then* tukishatoka hapo tuzipange barabara zetu tuseme barabara hizi tutamwomba baba huyu, tutamwomba mjomba yule, tutamwomba shangazi yule, lakini hizi tutajenga wenyewe na Waziri atuonyeshe kabisa. Kwa hiyo, tutakuwa tunajua barabara hii tunamsubiri *World Bank* akae vizuri, barabara hii tunamsubiri *ADB*, tunamsubiri *OPEC* tuzijue. Lazima tupange hapa. Lakini mimi nasema *source* ya kwanza iwe fedha zinazotokana na mafuta, zote tupewe kwenye barabara, nawaambieni hii nchi tutaijenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nilikuwa naangalia hapa kuna mtu anasema tozo la mafuta limepandishwa kwa shilingi 10 anasema haipaswi kupandishwa nilimwangilia yule Mbunge nikasema hivi huyu anajua anachokisema tusipopandisha tozo ya mafuta barabara hatutajenga na kila siku tutaambiwa tuko kwenye upembuzi yakinifu tutaambiwa hizi lugha siyo kwa sababu hawa viongozi hawapendi kujenga barabara, lakini hawana fedha. Kwa hiyo, lazima tukubali kunyanyaswa tuumie tujenge barabara kwa hiyo, lazima tukubali.

Kwa hiyo, nasema kama hatuchukui fedha yote inayotokana na kodi ya mafuta, basi tozo ya mafuta ipandishwe angalau kwa Shilingi 30. Halafu faini za kuzidisha mizigo zinaweza zikatupa *about 2.2 billion per year*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tumeambiwa na Waziri wa Fedha wamefuta Ushuru wa Leseni za Malori ambayo yanaanzia tani tatu kwenda juu. Barabara hizi zinaharibiwa na malori, kwa nini wasilipe? Kama mabasi yanalipa, kwa nini malori yasilipe? Hao wenye malori wao hawatembei kwenye hizi barabara? Tuamue leo, watu wa malori makubwa naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha waanze kulipa, *SUMATRA* wafanye kazi hii kukusanya pesa hizi zijenge barabara zetu. *(Makofi)*

Tuondoke huko, lakini baada ya hapo sisi wote humu tunanunua magari, tuanzishe ushuru kila anayenunua gari nchi hii iwe ya Serikali, iwe ya mtu binafsi, angalau walipie laki moja tu anapoandikisha tuweze kujenga barabara zetu. Tusipoamua tuchukue maamuzi magumu kwa ajili ya barabara zetu. Bila hivyo kila siku tutamu-*inclusify* Waziri wa Miundombinu kila mwaka kazi yetu itakuwa mbona kwangu barabara sioni, mbona kwangu hakupo, mbona kwangu Mheshimiwa Rais aliahidi mimi mmeniacha. Tutasema maneno hayo kila siku! Lazima tuamue! Mimi nawaombeni sana, tuamue sasa kwamba tuchukue pesa za *Excise Duties* zote za mafuta tukajenge barabara ama tuongeze viwango vyetu vya kutoza pesa ili barabara zetu ziweze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni Bandari ya Kigoma na Kasanga. Kama kweli tunataka ku-*tape* uchumi wa Congo uchumi wa Burundi kama ndiyo nia yetu, basi lazima tuendeleze Bandari ya Kigoma na Bandari ya Kasanga. Lakini ukiangalia kwenye mipango yetu huyaoni haya. Sasa mimi napata shida kidogo, sasa kama hatuyaoni tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni reli ya Kigoma. Ukiangalia mipango ya reli tena wame-*divage* ni Dar es Salaam-Mwanza, eti reli ya Kati ni Dar es Salaam-Mwanza. Kwa nini Kigoma haiwi *mentioned?* Hivi sisi siyo sehemu ya reli? Mimi naamini ni sehemu ya reli hii? Kwa hiyo, maendeleo ya reli hii yaiguse na Kigoma. *(Makofi)*

Hakuna nchi iliyoendelea duniani bila reli. *We will be making a mistake* kama tunaamua reli iende tu. Lakini hiyo Bandari ya Dar es Salaam bila reli haiwezi kuendelea. Bandari ya Mtwara bila reli haiwezi kuendelea. Bandari ya Kigoma tunasema tuijenge bila reli, haiwezi kuendelea. Hata hizi barabara zote tunazozijenga lazima kuwe na *connectivity,* bila reli haiwezi kuendelea kwa sababu moja kwamba njia ambayo inabeba mzigo mkubwa kabisa ni reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi narudia tena, ninawaombeni sasa tukae tukubaliane, tunapataje fedha za kuongeza kwenye Mfuko wa Barabara ili Mfuko huu uweze kujenga barabara zetu? Bila hivi tutapigiana makelele siku zote humu ndani na hatutakwenda. Baada ya kusema hayo, naomba na mimi kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kabla ya kumwita Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu nataka nimjibu Mheshimiwa John Cheyo kuhusu kwamba kiti hiki hakijai sawasawa katika zama hizi za ari mpya. Kwa hiyo, naomba nimwite Mwenyekiti mwenza, Mheshimiwa Jenista Mhagama aje aenee hapa. *(Makofi/Kicheko)*

*Hapa Mwenyekiti (Mheshimiwa Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa tuendelee baada ya kumsikiliza Mheshimiwa Peter Joseph Serukamwa naomba sasa nimwite Mheshimiwa Zungu ili aendelee na ratiba yetu, karibu.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu pamoja na chama changu na wananchi wa Jimbo la Ilala kuweza kunipa fursa ya kuja hapa na kuingia kuchangia na *inshallah* nitachangia Bajeti 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha wa Mipango na *dream team* yake na *tiger team* ambayo kwa kweli wameandaa Bajeti kwa ahadi ya Chama Cha Mapinduzi kwa ahadi mbili kuu tulizozitoa za kuwa na uchumi wa kisasa wa kujitegemea na kuwawezesha wananchi wetu.

Wengi wamezungumzia kuhusu pesa ndogo zilizowekwa kwenye kilimo. Lakini wengi vile vile wameshindwa kutazama *reality* na *obsolute* ya pesa hizi za kilimo. Ukitazama kwenye Bajeti ya mwaka jana 2005/2006 kilimo kilipewa asilimia 3.9. Mwaka huu asilimia 3.2. Lakini kwenye *obsolute* ya *trilion* 2 na milioni 400,060 bado Bajeti ya kilimo imepanda juu. Sio kubwa sana lakini imezidi mwaka jana 2005/06.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hii ninataka kuwatoa hofu wale wote ambao walikuwa wanafikiria kwamba labda Bajeti hii iko chini.

Suala la *food security* ni muhimu sana kwa Taifa letu. Kitu ambacho nakiona kikubwa si kubadilisha Mawaziri wa Kilimo, bali kuwa na sera nzuri ya kilimo, sera ambayo itakaribisha wawekezaji ili tuwe *partners*, nao watusaidie na aina na vyakula vinavyotakiwa pamoja na vyakula ambavyo vitakubalika kwenye masoko ya nje kwenye *export driven rally*. Bila kuwa na *partners* au bila kuwa na sera nzuri ya wawekezaji kutoka nje na sisi tukawa na sheria nzuri za kuhakikisha kuwa hawa wawekezaji baada ya kumaliza Mikataba yao wanaondoka au wanaacha ardhi hii wengi wanakuwa na wasiwasi sasa hivi wanafikiri ardhi itaibiwa na watu kutoka nje. Sio kweli! Tukiwa na mikakati mizuri, ardhi ya nchi hii haitaibiwa. Kama tuna wasiwasi na Wazungu, tuna marafiki zetu wa Kichina, wanaweza kuja hapa wakawekeza kwenye kilimo tukawa na mazao ya kukuza nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bonde la Rufiji. Mahitaji ya mchele katika dunia sasa hivi ni tani milioni 545. Bonde la Rufiji linaweza likachangia mahitaji ya dunia kama tutapata wawekezaji na kama kweli tutakuwa *serious* katika ulimaji katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kuongeza mapato ya Taifa letu, tuna Bandari ya *Dar es Salaam Transit Trade*. Uganda mwaka 2004/2005 wametumia Bandari ya Mombasa kwa mizigo *almost* tani milioni mbili na laki mia nane. Wanaikimbia Bandari yetu kwa sababu gharama za uendeshaji za kupokea mizigo ziko juu sana, wizi katika Bandari yetu umezidi, ucheleweshaji wa mizigo tunaweza tukachukua biashara hii, *transit trade* tukazihudumia nchi ya Malawi, Zambia, Uganda, *DRC* na tukaongeza mapato makubwa sana tufike hadi bilioni 250 kwa mwezi kutokana na kutumia Bandari hii na vyanzo vingine ambavyo tunaweza kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia kuhusu madini pamoja na mikataba ya madini na mimi naungana nao kabisa. Lakini vile vile, hivi hakuna mkataba au masharti ambayo mwekezaji analazimishwa kuweka majengo au kujenga majengo katika nchi yetu? Johannesburg imejengwa na madini. Leo kuna watu wamepewa viwanja katika Mkoa wa Dar es Salaam katika maeneo ya Ohio lakini majengo yale hayajengwi, yanatunyima sisi mapato, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala katika kodi ya majengo, yanatunyima ajira na yananyima sura nzuri ya Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mporomoko wa pesa ya Tanzania sio tu kwa kutoku-*export*. Sababu *investors* tuliokuwanao wanaondoa faida zao zote wanapeleka nje hawa-*invest* katika nchi yetu. Kwa hiyo, tukiboresha maeneo ya migodi na nikasikia *Kahama Mining* wana jengo kubwa ghorofa 18 Mkoani Dar es Salaam mimi nitashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa kufuta vyanzo vya leseni na kodi za kero ambazo zinaumiza wananchi wetu na Serikali inajitahidi kuzifidia Halmashauri. Nawaponga sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa hizi pesa kwenye Halmashauri zetu hauji kwa mpangilio kama sisi tulivyokuwa tunakusanya. Naiomba Serikali na Waziri Mkuu yupo hapa, yeye atusaidie. Kwa Wilaya yetu ya Ilala bado tunaidai Serikali milioni 545. Hii ni asilimia 18 au 20 ya bilioni 2,700 ambazo sisi wenyewe huwa tunazikusanya kwa mwaka kwenye Manispaa yetu kwenye vyanzo vya leseni na kero ambazo zimefutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mpango wa kuboresha Hospitali yetu ya Amana. Sasa kwa vile mwaka huu unakwisha mwisho wa mwezi huu na Waziri upo hapa, kabla haujafunga hesabu zako tutaziomba hizi pesa ili tukamalize jengo la *OPD* ya Hospitali ya Amana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuchangia katika Bajeti hii ni *pensioners*. Ni kweli viwango vya pesa wanavyopata ni vidogo. Lakini licha ya kuwa pesa wanazopata ni ndogo, wakati wa malipo yao wanadhalilishwa wakati wanapokea hizi pesa. Unakuta *Senior Officials* wa Serikali waliostaafu, wanajazana kwenye kituo kimoja na wanasukumana hata ile hamu ya kuwa kweli alikuwa mtumishi wa Serikali hii, anachoka! Utafutwe mpango mbadala wa namna gani wa kuwalipa wastaafu watumishi wa Serikali katika Vituo mbalimbali ili wasipate bughudha na kuteseka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la kuondoa umaskini, wananchi wengi katika nchi yetu wamehamasika. Lakini viwango vya kusajili vikundi hivi viko juu sana. Gharama ya kusajili vikundi kama *NGO* ni Sh.200,000/= na hii inabidi Mbunge alipe. Ukitazama vikundi katika Jimbo, kuna vikundi vingi sana ambavyo watu wanahamasika. Mimi sioni sababu hivi viwango viwe vikubwa sana. Wangeweka sasa hivi viwango maalum isizidi Sh. 20,000/= kwa kila kikundi kujisajili ili kuweza kutambulika kisheria kikundi cha kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo la wafanyabiashara wadogo wadogo. Hakuna Serikali duniani inaweza kufanikiwa kupigana vita na wananchi wake na Serikali ambayo ni makini kama ya kwetu huwa wanatafuta muafaka. Naishukuru Serikali kwa kusitisha uboaji wa maeneo mbalimbali katika nchi yetu baada ya kuona fujo zimezidi. Lakini hawa wafanya biashara wadogo wadogo kwa jina Machinga, *were sitting on goal mine.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweza kuwawezesha wafanyabiashara 100,000 kwa kuwahamasisha kila mmoja wao ambaye ana uwezo wa kulipa Sh.100/= kwa siku tutapata milioni 10 kwa siku, milioni 300 kwa mwezi, 3.6 bilioni kwa mwaka. Mfuko wenyewe wa Machinga wenyewe wanaanza na 3.6 bilioni na Serikali inaweza kuongeza *seed money* ili waweze kujiwezesha na kupunguza adha ya wao kuonekana siyo jamii ya Kitanzania. *(Makofi)*

Wamachinga ni jamii ya Kitanzania na ni watu wanatusaidia sana kuweza kusaidia Serikali kuweka madarakani. Kwa hiyo, lazima tuwaenzi kuwatafutia programu. Mimi nitaiomba Serikali ianzishe programu ya kuwaenzi wafanyabiashara wadogo wadogo katika nchi nzima ya Tanzania. Kuwe na maeneo ya *night markets,* kufunga barabara nyingine ili kuwapa fursa wafanyabiashara katika maeneo mazuri na ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zetu ni mbaya. Mimi naiomba Serikali na Serikali pekee haiwezi Waheshimiwa Wabunge. Lakini Halmashauri zinaweza zikakopa. Kuna mpango wa *World Bank* wa kuboresha kodi za majengo. Sasa Manispaa ya Ilala inaweza kukopa na ikalipa si chini ya *1.5 billion Dolars* kwa mwaka tupewe kibali hiki ili tutengeneze barabara zetu. Lakini kikubwa, naomba Serikali itupie macho barabara ya Uhuru. Barabara ya Uhuru imekuwa ni kero kubwa sana. Hata huyu mgeni wa juzi akipita kwenye barabara ile naye vile vile akasikitika kuiona barabara imeharibika vibaya sana. Tunaomba msaada maalum wa barabara ya Uhuru ambayo ni kilomita nne tu iboreshwe, itengenezwe ili kupunguza msongamano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa *TASAF*. Mimi naipongeza Serikali kwa dhati kabisa. *TASAF* imewafikia wananchi wengi na *TASAF* imefanya mambo mengi. Lakini kuna wababaishaji ndani ya *TASAF* ambao wanapunguza sifa ya Serikali wa mfuko huu kwa upendeleo na ubinafsi ndani ya mfuko huu. Mimi ninaomba, sisi Wabunge tunaweza kuibua miradi vile vile. Tupangiwe asilimia fulani ya *TASAF* kwenye mifuko ya Wabunge ili tuibue miradi katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulisema, juzi kulikuwa na tangazo la Serikali kuhusu wenye viwanja katika maeneo ya Dar es Salaam kutaka kunyang'anywa. Watu wa Dar es Salaam ni watu maskini, kuanza kuwarusha roho sasa hivi wakati Serikali inataka kuanzisha mikopo ya kujenga nyumba, watu wanakuwa na wasiwasi kwamba kumbe kuna hila ya kuwafukuza watu kuleta watu! Tunaomba hili litazamwe kwa jicho maalum. Katika kila mfumo wa uongozi kuna utu na ubinaadamu.

Hawa watu wa Dar es Salaam mkiwanyang'anya, katika viwanja vya Tegeta na Masaki na hasa agizo hili ni Dar es Salaam tu, hakuna maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho nakiomba, Waziri Mkuu wa China anakuja, jana mmesaini mkataba wa kuuziwa gesi na Egypt. Sisi tumejiandaa vipi? Tunawauzia nini na wanaleta kiwanda cha *wireless loop* ambayo sasa hivi ni kitu ambacho kina *market* popote duniani na sisi waje ili na sisi tuweze kupata kiwanda kama siyo cha *wireless loop* ili tuweze kufanikisha masuala yetu.

Suala la maji tumelizungumza sana, hata juzi tulizungumza. Lakini kulikuwa na mipango miaka ya nyuma, kumi, kumi na tano iliyopita ya kuleta maji huko Dar es Salaam kutoka Rufiji. Tukisema kwamba kuna gharama kubwa, ni kweli ina gharama, lakini tui-*spread* tuweke *aggregate* ya miaka 10, 15 kila mwaka tujenge kilomita 10, baada ya miaka 10 tutakuwa na uhakika mkubwa sana wa maji katika Jiji la Dar es Salaam.

Lingine kabla sijakaa chini, kulikuwa na mpango wa chakula kwa wakati wa njaa. Dar es Salaam njaa ipo, maskini wapo. Yale mahindi ya Sh.50/= sisi hatukupata. Kama yapo tunayaomba, kama yamekwisha, basi kipindi kijacho Mungu atunusuru tutaomba isitokee balaa tuyapate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali ambayo bado haijatangaza rasmi, lakini tumeshasikia Kocha wa Michezo ameshachaguliwa wa timu yetu ya Taifa, lakini na sisi Wabunge vile vile tuanzishe mashindano ya michezo katika shule zetu za Msingi na Sekondari. Hatuwezi kusubiri Serikali kutufanyia haya. Kuna vitu vingine, Serikali sio mwarubaini wa kila matatizo. Tulivyosimama kwenye majukwaa tulikuwa tunaahidi maendeleo. Leo tunaiomba Serikali itusaidie, vipi wakati tulipokuwa tunaomba kura hatukusema kwamba Serikali itakuwepo?

Sasa nataka kusema kwamba jamani, Mheshimiwa Mkapa alikwenda kuomba jina, imeyeyuka, sasa chonde hii aliyokwenda kuomba Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, iwe ya kweli kweli mradi huu utekelezwe. Tafadhali sana na mimi naomba wenzangu wote wa Masasi wasubiri ahadi safi zilizotolewa na Mheshimiwa Jakaya Kikwete naamini kabisa zinatekelezeka na maji tutayapata kwa wingi kabisa Masasi. *(Makofi)*

Mwisho upesi upesi ni kwamba, kuna suala la mazingira. Huko sehemu za Mbarali kumekwisha kabisa kwa ajili ya mifugo iliyotoka huko Kaskazini Usukumani, sijui wapi na wapi eti baada kuharibu huko sasa kuna mpango wa kuleta mifugo ile Kusini. Hatutaki! Hatutaki, ieleweke wazi kabisa hatutakuwa tayari kuipokea mifugo ile iliyozidi katika bonde la Mbarali, mkae nayo huko huko, sisi tuko radhi kula maharage yetu, lakini hatutaki mifugo ile ije iharibu mandhari nzuri ya Kusini. Hiyo hatutaki kabisa, hatutaunga mkono.

Naomba sana sana wale waliokuwa wanafikiria watapita pale daraja ya Mkapa, mimi naomba Serikali ya Rufiji iweke kizuizi kuhakikisha kwamba wanarudi huko huko

walikotoa mifugo yao. Sisi tunataka ufugaji wa kisayansi na huo tunaweza kuanzisha kule kule Kusini lakini sio kuletewa haya mang'ombe mengi yasiyo na sababu, magonjwa gonjwa na nini hatutaki! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba kuunga mkono hoja. Lakini Waziri tafadhali barabara ile ya Kusini mtuambie lini itakamilika, namna nyingine itatuwia vigumu kweli kweli sisi watu wa Kusini kuiunga hoja yako ambayo ni nzuri sana. Tafadhali fanyeni hivyo. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Asante sana Mheshimiwa Mrope. Waheshimiwa Wabunge, naomba nifanye masahihisho kidogo. Badala ya Mheshimiwa Mpendazoe, tutaanza na Mheshimiwa Stephen Galinoma, halafu nitaomba Mheshimiwa Elizabeth Batenga ajiandae.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi hii ya kutoa mchango wangu. Napenda nianze kwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Kalenga kwa kuwa na imani nami na kunipa nafasi hii ya kuja kuwawakilisha. Napenda vilevile niwashukuru sana kwa mambo yote, mchakato mzima ambao uliniwezesha kuja hapa. Vilevile, naomba niwape pole kwa matatizo mbalimbali waliyoyapata kutokana na upungufu au uchelewaji wa mvua, matatizo mengi kidogo yamewapata, tuombe tu kwa Mwenyezi Mungu atupunguzie matatizo ambayo tumekwishayaona.

Naomba hapo hapo, nitoe pongezi kubwa nyingi na za dhati kwa Waheshimiwa Mawaziri wawili hawa, Mheshimiwa Zakia Meghji na Mheshimiwa Ngasongwa kwa hotuba zao ambazo zimetupa msingi wa majadiliano haya. Mambo mengi yamezungumzwa na wenzangu na mimi nisingependa kurudiarudia, lakini kuna mambo fulani ambayo ningependa kujikita nayo. Kwanza nianze na suala la kilimo. Kuhusu kilimo, naomba tukumbuke haja ya kuleta mageuzi katika kilimo chenyewe kwa kuondoa kilimo cha jadi cha jembe la mkono na kuleta mageuzi tutumie matrekta, tutumie ng'ombe na kadhalika.

Katika kuunga mkono suala hili ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, mimi ningependa kuongezea tu kwamba katika kuleta mageuzi hayo pengine Serikali yetu ingehamasisha suala hili kwa kuhakikisha kwamba tunapata matrekta mengi kadiri inavyowezekana katika sehemu mbalimbali na hasa Mikoa ile inayosemekana kwamba ni *big four* inayoweza kulisha nchi nzima. Tukiweza kupeleka matrekta mengi ama iwe kwa biashara au kwa msaada, mimi nafikiri ingesaidia sana. Lakini tusifanye kama tunavyofanya sasa kupeleka nyenzo ambazo hatuna *control* nazo, mpango kama huu uandamane na utaratibu mzuri wa ku-*administer* au kudhibiti suala hili zima, kwa sababu siku za nyuma nakumbuka tulianzisha *mechanism agriculture* katika sehemu fulani fulani nchini, lakini matatizo ya utawala wake yalifanya kilimo hiki kikafa na sasa amebaki mtu mmoja mmoja.

Hapo hapo, ningependa nizungumzie kwa ufupi tu suala la mbolea. Imezungumzwa na Wabunge wengi sana, lakini kitu ambacho ningependa Serikali

itusaidie ni kujua kwanini bei inapomfikia mkulima inakuwa ni kubwa kiasi ambacho tunashuhudia sasa. Ningependa Wizara au Serikali ituambie gharama ya mbolea inapofika Dar es Salaam *CIF*, halafu ituambie hatua kwa hatua, kwanini inapomfikia mkulima bei inakuwa ni kubwa sana. Si hivyo tu, msimu uliopita tulikuwa na mbolea za aina mbili za kawaida na za ruzuku, tofauti yake ya mbolea bei yake ni ndogo sana na kwa kweli kulitokea udanganyifu mwingi sana ambao ulitokana na ukweli kwamba wafanyabiashara waliweza kudanganya kuuza mbolea zile za ruzuku kwa bei zile za kawaida hivyo ikawa *impact* yake ni kama hakuna.

Mimi ningeshauri Serikali ifikirie mbolea hizi kwanza. Ruzuku yenyewe ingetolewa kwa mbolea yote, sio Mikoa fulani fulani kama walivyofanya safari hii. Kama haiwezekani kufanya hivyo, basi angalau ipitie katika Vyama vya Ushirika ama hivi tunavyoita siku hizi *SACCOS*. Lingine kuhusiana na suala la kilimo, ningependa kuona Serikali inatukwamua. Kule Jimboni kwangu kuna miradi miwili ya umwagiliaji, mifereji ya umwagiliaji ambayo tumetumia fedha nyingi kiasi cha milioni 300 hivi, lakini kwa sababu mbalimbali, haikukamilika na sasa ningependa Wizara inayohusika itusaidie kutukwamua.

Ningependa vilevile kuzungumzia suala la miundombinu. Katika hili, swali langu ni moja tu, nalo ni barabara ya lami Dodoma kwenda Iringa. Nimekuwa nazungumza hili suala tangu nilipokuwa Mbunge mara ya kwanza mwaka 1995 na kila mara majibu ni kwamba tunafanya upembuzi yakinifu. Sasa sina hakika inachukua muda gani. Sababu za kutaka barabara hii iimarishwe, ziko wazi kabisa. Kwanza kabisa itafungua biashara kati ya Mikoa ya Kusini na Mikoa ya Kaskazini.

Kipindi kile tulikuwa tunazungumzia Mikoa yote ya Kati, ya Kusini na Kaskazini, tulikusanyika tukataka kuishinikiza Serikali itupe msaada barabara hiyo iweze kutengenezwa. Lakini kwa sababu ambazo sizielewi, walikuwa wakitegemea fedha zinazotoka kwenye Mashirika ya nje, sielewi kwanini hatuwezi kutumia fedha za humu ndani kama tunavyofanya katika barabara nyingine!

Kama nilivyosema, barabara hii itafungua uchumi, itafungua mawasiliano, lakini vilevile itaimarisha utalii. Nakumbuka miaka ile Waziri ambaye sasa ni Waziri wa Fedha alikuwa na mpango wa kuimarisha *a Southern Tourist Zone*, ilikoyeyukia mimi sifahamu. Lakini kama tukiimarisha ile barabara itatuwezesha kabisa kufufua uchumi kwa pato linalotokana na utalii. Mwendo huu mpya tuweke mkazo toka *South Africa*, *Cape Town* mpaka Cairo na sehemu nyingi zimekwishatengenezwa isipokuwa kipande hicho kidogo cha maili 142. Mimi nafikiri inawezekana kabisa kama pakiwa na nia.

La mwisho ambalo ningependa kulizungumzia, ni kuhusu upelekaji madaraka Vijijini, kwanza kabisa niipongeze Serikali kwa utaratibu wake wa *TASAF* kupelekwa Vijijini, kwamba uibuaji wa mipango, maamuzi ya nini kifanyike katika maendeleo, yamepelekwa Vijijini. Sio vibaya tukirudi nyuma, hili ndilo lilikuwa lengo la Serikali tangu wakati ule tumeanzisha madaraka Mikoani mwaka 1972 na lengo lilikuwa ni kutoa mamlaka na madaraka kwa Serikali za Vijiji kuibua mipango yao wenyewe. Mimi nafurahi kuona kwamba *TASAF* ni mfano mzuri sana na ningependa Asasi nyingine ziige

mfano huo. Bila hivyo tutaendelea kusuasua. Nasema hivi kwa sababu natambua kwamba katika kipindi kirefu sana tumekuwa tukipeleka fedha nyingi kwa malengo mbalimbali, kwa majina mbalimbali kwa lengo kubwa la kupunguza umaskini.

Lakini ukweli uliowazi ni kwamba umaskini umezidi kujikita, sasa unajikwamua vipi? Nadhani hatua ya kwanza ni hiyo ya kupeleka maamuzi kule Vijijini. Lakini hatua ya pili, lazima tuchukue kila hatua inayowezekana kufanya kile siku hizi kinaitwa *capacity building*, yaani tuwafundishe hawa viongozi wa ngazi zile. Nasema hivi kwa sababu sio siri kwamba uwezo wa wenzetu katika ngazi za Vijiji, za Kata na hata Wilaya sio mkubwa sana na ungeweza kuwa *improved*. Kwa maana hiyo, iko haja kubwa ya kuhakikisha kwamba wote wanaohusika na usimamizi wa maendeleo katika maeneo yale hasa katika ngazi ya Wilaya wanawezeshwa kuelewa nini kinatakiwa na kwa hiyo, waweze kusaidia kusimamia wale walio chini yao.

Papo hapo wale walio chini kule Vijijini, nao lazima tuwawezeshe kujua nini cha kuchagua na nini cha kutenda, kwa sababu bila hivyo, fedha hizi zitatumika kama zilivyotumika nyingine huko nyuma na tusipate *impact* ambayo ni muhimu sana. Hapa napendekeza kwamba zichukuliwe hatua za makusudi kabisa za kutoa mafunzo kwa hali na mali, yaani *capacity building* katika ngazi zote mbili, ngazi ya Wilaya na ngazi za Vijijini ili mradi tuweze kupiga hatua.

Baada ya kusema maneno hayo machache, najua kengele ya kwanza imeshalia, sitaendelea. Napenda tu kusema kwamba ninaunga mkono hoja iliyo mbele yetu moja kwa moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hoja hii. Napenda nimpongeze Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha kwa kuwasilisha hoja hii ambayo tunaijadili hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mawasiliano na uchukuzi ni suala muhimu sana na litazungumzwa na Wabunge wengi, kila mtu kwa maneno yake kwa sababu ya umuhimu wake. Mimi naomba nizungumzie kuhusu reli ya kati. Reli ya Kati ni tegemeo kubwa sana kwa Mikoa ya Magharibi, Mikoa ya Kati na Mikoa ya Kanda ya Kati na Kanda ya Ziwa kwa sababu ya kusafirisha mizigo/bidhaa lakini pia abiria. Lakini inashangaza sana na inasikitisha sana kuona kwamba Serikali, labda kwa makusudi kuzidi kuwarudisha nyuma wananchi wa Mikoa hii. Serikali imezembea kiasi cha kutosha kuitunza reli ya kati kiasi kwamba sasa hivi iko katika hali mbaya sana, hata itakapokodishwa sijui itakodishwa nini ma-*scrap* matupu ndio itakayokodisha sijui mkataba, kwa vile ni siri ya Serikali lakini kama tungeletewa hapa, tungeona nini katika mkataba huu wa kukodisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwamba mabehewa yale wala hayafai, tena hayafai kabisa! Mapanya humo, mende, hata kunguni katika mabehewa hayo yanayosafirisha binadamu. *Engine* zimechakaa sana, zimechakaa kiasi kwamba sasa hivi ni tishio kwa abiria wanaotumia reli hiyo au mabehewa hayo kwa sababu mara nyingine yanashindwa kufanya kazi katika ya safari, hasa inapopanda milima, watu wa Kigoma ni

mashahindi. Watumishi wa reli wamekata tamaa kutokana na mazingira mabaya ya kazi, mishahara midogo na kadhalika, reli yenyewe ni mbovu sana kwa sababu haifanyiwi matengenezo ya kutosha, lakini ubovu huo unaongezewa na watu wanaoiba mataruma ya reli.

Miaka mitatu au miwili iliyopita, nilimhoji Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi wakati tukipitisha bajeti yake kifungu kwa kifungu, kwamba ni kwanini mizigo au bidhaa ziendazo katika Mikoa hiyo niliyoitaja badala ya kupakiliwa Dar es Salaam inaletwa mpaka hapa Dodoma? Sasa na abiria wanaanzia safari zao hapa. Niambie usumbufu ulioje huo! Niambie matatizo wanayoyapata wasafiri hasa wanawake na watoto mimi ninaowawakilisha! Jibu la Mheshimiwa Waziri, alisema kwamba lilikuwa ni tatizo dogo la muda mfupi na litakwisha na hali itarejea kama kawaida, safari ya mizigo na bidhaa itakuwa inaanzia Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa matokeo ya mizigo kuletwa Dodoma na abiria kuanzia Dodoma kwa kweli imekuwa ni mateso makubwa sana na maumivu makubwa sana kwa wananchi wa Mikoa ile niliyoitaja. Kwa sababu bei za vitu zimepanda zaidi sasa karibu inafikia mara mbili ya bei ambayo watu wananunua bidhaa hizo kama Dar es Salaam au pengine hata hapa Dodoma. Kwa mfano *Cement* inayonunuliwa mfuko mmoja Sh.9,000/=, Sh.9,500/=, Bukoba Mjini tunanunua kwa Sh.15,000/=, sasa mfuko huo haujafika Vijijini. Sasa hapo wananchi kweli watajenga! Tunasema kwamba kigezo kimojawapo cha maendeleo ni watu kuwa na nyumba bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nilikuwa naomba sana, sijui sasa kitafanyika nini maana wanasema wanakodisha, huyo atakayekodi, basi tunaomba masharti yatakayowekwa katika Mkataba yawe ni masharti ya kutusaidia ile Mikoa niliyoitaja, Mikoa ya Magharibi, Mikoa ya Ziwa na hata Mikoa mingine hii ya Kati ya Singida na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za nyuma reli ilikuwa inaambatana na bandari za maziwa, lakini sasa walianzisha Kitengo cha Kampuni za Meli. Kwa hiyo, unakuta kwamba reli na sasa hii meli zinafanya kazi tofauti. Kwa hiyo, mwekezaji huyo au mkodishaji huyo kama atapatiwa Mkataba, basi tunaomba uwe ni Mkataba ambao utalenga kutusaidia. Naomba kuhoji na kwa kweli tupate majibu ya kuturidhisha au ya kutusaidia, ni kwanini hiki kipande cha kati ya Dodoma na Dar es Salaam hakiwezi kutengenezwa, ili mizigo na abiria waanzie Dar es Salaam? Hivi hii hawaoni kwamba ni dharura kama dharura nyingine?!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba, kwa kuwa nilikuwa nimekwisha ahidiwa na Waziri wa Mawasiliano wakati ule, basi sasa nadhani tapata jibu ambalo litakuwa ni sahihi zaidi ili na wananchi nao kule ionekane Serikali inawajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme suala la mawasiliano ni muhimu sana. Sasa nizungumzie usafiri katika Ziwa Victoria, ni matatizo makubwa sana. *MV Victoria* tuliyonayo ambayo ni meli ya Shirika la Serikali ni meli ya siku nyingi, lakini angalau tunashukuru kwamba inafanyiwa matengenezo ya hapa na pale. Lakini vyombo vingine

vya watu binafsi vinavyosafiri mle, sisi hatuoni usalama wowote, hatuoni kama Serikali au ile *SUMATRA* tuliyoipitisha humu Bungeni inafanya kazi ya kusimamia ubora na uimara wa vyombo hivi ambavyo vinasafirisha watu. Maafa yaliyotokea siku za karibuni yanajulikana, *MV Nyamageni* ilizama na watu ambao hata idadi yake haifahamiki vizuri. Lakini sisi tuliona kwamba kulikuwa na uzembe wa namna fulani. Hivi hiyo *SUMATRA* haina nguvu za kuweza kusimamisha chombo chochote kwamba kikionywa kwamba kisisafiri, kikatii? Sasa hikiwezi kikakamatwa kisiweze kusafiri kabisa, mpaka watu wazame? Hilo naomba pia lionekane hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tulileteva meli ziendazo kasi, hivi zile meli ziendazo kasi kweli kuna chombo cha Serikali ambacho kilizikagua kikaona kwamba ni meli ambazo zinafaa kuingia ziwani mle kusafirisha abiria?! Mara *engine* zizimike katikati ya Ziwa, mara zimekuwaje, maana yake mpaka sasa hivi wala hazifanyi kazi. Sasa mimi ninaona kwamba Serikali inauzembe wa namna fulani. Sasa maafa yanapotokea, tunashtuka, tunaanza kukimbiakimbia. Mheshimiwa Maua Daftari alikuja meli ilipozama. Mimi kidogo nilijificha hatukuonana, lakini nilikuwepo maeneo. Yaani kwa kweli inashangaza sana. Mimi naona hii Mikoa ya Kanda ya Ziwa Serikali haioni kwamba ni Mikoa ambayo inastahili kupata huduma kama Mikoa mingine.

Sasa nikiendelea na Uwanja wa Ndege wa Bukoba, nilipoanza kuongea Waziri Mkuu akaondoka, lakini nilikuwa nataka nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu kama aliona ule uwanja wa ndege unafaa katika mazingira ya sasa. Hii Mikoa ya mipakani inapaswa kuangaliwa vizuri zaidi na kwa makini zaidi kwa kuzingatia kwamba iko mpakani na matatizo ya mpakani yanaeleweka. Halafu sasa Mikoa ile ina mvua nyingi, pale Bukoba kuna mvua nyingi! Kuna siku moja yatakuja kutokea matatizo tuanze kukimbiakimbia kana kwamba tatizo tulikuwa hatulioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba sana Serikali iwe makini, iwaone wale watu kwamba wanastahili kupata huduma, viwanja vya ndege vimetajwa vingine kabisa, Bukoba sikuona katika Bajeti hii. Lakini katika ahadi za Rais imo. Sasa sisi tunaendelea kupokea ahadi, ni lini tutatekelezewa hizo ahadi? Sasa na sisi tuanze kuhesabu madeni sijui, tuweke penati sijui, au faini, mimi sielewi. Lakini ahadi ni deni. Kwa hiyo, tunaomba watu wa Mkoa wa Kagera waangaliwe, mafuta bei ni juu sana. Sasa hivi nadhani mafuta yatakuwa yamekwishafika Sh.2,000/= kwa lita moja, kwa sababu ya huo huo usafirishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nilikuwa naomba sijui niseme kwa lugha gani, au kwa uchungu gani, lakini ninaomba Serikali ituangalie kwa jicho la huruma Mikoa ile niliyoitaja, Mikoa ya Kati, Magharibi, na Mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sipendi kugongewa kengele, mimi ni Mbunge wa siku nyingi. Kwa hiyo, naomba nimalizie kwa kukushukuru tena. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD S. NYAULAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuweza kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika hoja hii. Awali ya yote ningependa

kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wa Mipango na Uchumi pamoja na Waziri wa Fedha kwa matayarisho mazuri ya Bajeti hii ambayo inalenga kutekeleza sera za Chama cha Mapinduzi. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutekeleza Sera za Chama kunahitaji pesa nyingi sana, na mimi kushiriki katika mchango huu ningependa nitoe mchango kidogo katika mchango kuongeza mapato ili tuweze kutekeleza Ilani ya Chama.

Ningependekeza kwamba ushuru wa forodha ungeongezwa au ungetozwa kwenye nyama inayoagizwa kutoka Australia ambazo zinatumika kwenye mahoteli mengi na kwenye migodi ya madini. Matunda kutoka Afrika ya Kusini mengi sana yanaingizwa katika nchi hii na yanasambazwa sehemu zote, kuna juisi nyingi ambazo zinaletwa kutoka *South Africa* pamoja na *Middle East*, Maziwa vilevile yanatoka *Middle East* pamoja na Afrika Kusini, na samani ambazo natumaini tunaweza kuzitengeneza hapahapa nchini. Ningeomba vitu vyote hivi vingetozwa ushuru wa forodha ikiwa ni njia mojawapo ya kuweza kuongeza mapato na kwa kufanya hivyo tutakuwa tunahamasisha matumizi ya matunda, nyama, juice, maziwa ambavyo vinazalishwa hapa hapa nchini, lakini vilevile na samani ambazo zinatengenezwa hapa nchini.

Vilevile, ningeomba katika kuongeza kasi ya kuongeza mapato kasi ya kuuza hisa zinazomilikiwa na Serikali kwenye Mashirika 124 yaliyobinafsishwa, iongezeke kwa sababu kama Serikali itauza hisa hizo badala ya kuziweka tu, maana yake ni kwamba wanaweza kupata pesa za kutosha ili ziweze kutumika katika shughuli za maendeleo. Lakini vilevile ningetaka kushauri utaratibu uliotumika kubinafsisha *NMB*, inaelekea ulikuwa ni mzuri zaidi. Utaratibu huo kama utakuwa umefuatwa, bila shaka tunaweza kupata pesa nyingi zaidi kwa kubinafsisha Mashirika yetu kuliko utaratibu uliokuwa unatumika huko nyuma kwa sababu katika kubinafsisha *NMB* malengo yalikuwa kupata bilioni tano, lakini Serikali iliweza kupata bilioni 33. Natumani makisio hayo na hali halisi ni tofauti sana na ninategemea kwamba kutokana na ubinafsishaji uliokuwa na utaratibu mzuri ndiyo uliosababisha kiasi cha bilioni 33 ziweze kupatikana badala ya bilioni tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetaka kutoa pongezi kubwa sana kwa Serikali kuweza kutenga Shilingi 4,350 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa uwanja wa ndege wa Songwe. Nina imani kwamba uwanja huo baada ya kuchangia pesa hizo unaweza kukamilika na ukaanza kutumika sawasawa. Lakini nina imani kwamba uwanja huo hautatumika sawasawa bila ya kuwa na barabara nzuri zinazounga Wilaya ya Mbeya kwenda Ileje kwenda Chunya kwenda Makete na vile vile kuunganisha Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Rukwa. Nina imani kabisa kwamba bila kuwa na kilimo ambacho kinawahusisha wakulima wadogo wadogo kwa kutumia *Contract Farming* ili kuweza kuzalisha mbogamboga, maua pamoja na matunda ambayo yanaweza kuuzwa katika nchi za nje uwanja huo hautatumika sawasawa. Nina imani vilevile kwamba bila kuwa na mahoteli ya kisasa na bila kuwa na Kumbi za Mikutano katika Wilaya ya Mbeya, basi inawezekana kwamba matumizi ya uwanja huo hayatajitokeza.

Lakini la mwisho, nilitaka kusema kwamba bila  kuwa na *cold storage facilities* pamoja na kuligeuza eneo  la Iwambi la ekari 2,500 ambalo lipo katikati ya Mji na sasa linategemewa kugawanywa katika viwanja 15 ili liweze kuuzwa.  Ningeomba Serikali isiliuze eneo hilo, badala yake lipewe Jiji la Mbeya ili yote haya tunayozungumza kuhusu mahoteli ya kitalii, kuhusu Kumbi za Mikutano, kuhusu *cold storage facilities* pamoja na uanzishwaji wa *Special Economic Zone* ziwe katika maeneo hayo, kwa sababu kwa kufanya hivyo tutakuwa tumejenga miundombinu madhubuti ambayo inaweza kuhudumia uwanja huo. Kama hakutakuwa na miundombinu madhubuti, nina uhakika uwanja huo utakuwa ni *white elephant,* hautatumika kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo basi, ningeomba kwa kuwa uwanja huo haugusi Wizara moja ya Miundombinu tu, bali inagusa Wizara nyingi, Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, zote zinahusika katika suala hili, kwa hiyo, mchango wangu hapa ni kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama ikiwezekana aweze kuteua Kamati ambayo itajaribu kuhamasisha maendeleo na ukuzaji wa miundombinu ili uwanja utakapofunguliwa, basi uweze kutumika sawasawa.  Lakini pasipokuwa na matayarisho haya, fedha zote ambazo ni zaidi ya bilioni 28 zilizotumika kwa ajili ya kujenga uwanja huo hazitaleta matunda kwa muda mrefu ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wetu.  Naipongeza Serikali kwa kutenga shilingi bilioni 195.5 kwa ajili ya shughuli hiyo.  Hilo ni ongezeko la Shilingi bilioni 36.8 kutoka kiwango cha mwaka jana, 2005.  Sasa ingawaje kiwango hicho kimeongeza lakini ni dhahiri kwamba  uwiano wa kiasi kilichotengwa kwa ajili ya kilimo kutoka mwaka jana, 2005 kimeshuka kutoka asilimia 8.8 mpaka asilimia 8.1 ya matumizi yote ya Serikali.  Kwa hiyo, fedha taslimu zimeongezeka lakini kwa uwiano pesa hizo zimepungua.  Katika Mkutano wa Garborone ambao ulikuwa ni wa *SADC,* Marais wa *SADC* mwaka 2005 huko Garborone, walikubaliana kwamba itakuwa ni vizuri kama Serikali zitakuwa zinatenga kiasi cha asilimia 10 ya Bajeti nzima kwa ajili ya kuendeleza kilimo chetu ili tusije tukapata matatizo ya njaa, lakini vilevile tuweze kuongeza *exports* zetu.

Sasa naona kwamba huu mchango wa fedha zilizotengwa kutoka mwaka jana kwa asilimia zimepungua kutoka asilimia 8.8 mpaka 8.1.  Nashauri, kufuatana na hayo makubaliano ambayo viongozi wetu walikuwa nayo, mchango ungeweza kuongezeka katika suala la kilimo ili liwe asilimia tisa na itakapofika mwaka 2008 kufuatana na makubaliano, basi tuweze kuwa tumefikia asilimia 10.

Vilevile, ningependa kuchukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali na hasa Waziri Mkuu pamoja na Rais kwa kazi nzuri ambayo waliweza kulishughulikia suala la njaa. Suala la njaa lilikuwa ni kubwa na linagusa wananchi wengi na walikuwa hatarini kupoteza maisha yao, lakini lilikuwa limechukuliwa kwa nguvu mpya, Kasi Mpya na kwa kweli matokeo yameweza kuonekana.  Wananchi wote wanashukuru kwa kazi nzuri iliyokuwa inafanyika. Lakini bila kuwa na juhudi za kuongeza kilimo bado tutakuwa na matatizo.  Kwa hiyo, nilikuwa nataka kushauri vitu vifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbalizi kuna eneo la ekari 5000 lililokuwa chini ya *Tanganyika Perkars* sasa hivi halifanyi kazi kwa sababu kuna mgogoro wa kuweza kulitumia. Ningeiomba Serikali iwaruhusu wananchi wa eneo hili waweze kulitumia mpaka hapo Serikali au Wizara ya Mifugo itakapokuwa tayari kujenga Kiwanda cha Nyama. Napenda kuwapongeza wananchi wa Mbeya, Rukwa pamoja na Songea na Iringa kwa kulima mahindi mengi sana.

Nina uhakika kwamba safari hii Mikoa hii ya Kusini itauza chakula kwa sehemu nyingine ambazo hazitakuwa na chakula cha kutosha. Hii inawezekana tu endapo Serikali itanunua mahindi hayo kwa bei nzuri na kuyaweka katika *strategic grain reserve.* Wasinunue kwa bei mbaya kwa sababu kivutio pekee cha mkulima ni pale ambapo anaweza kupata bei nzuri ya mazao yake. Nina hakika kama Serikali itanunua mahindi kwa bei nzuri watahamasika na kulima zaidi na kulisha nchi nzima na tukaepukana na matatizo ya njaa.

Kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo, ningetaka kupendekeza kwamba bila kuwa na kiwanda cha mbolea, bado hatutakuwa tunapiga hatua yoyote. Ilani ya Chama imeeleza kwamba kiwanda cha mbolea kinastahili kuwepo na nilikua napendekeza zile fedha ambazo zilikuwa zimechangiwa na wananchi kwa kutumia *Unit Trust* ambazo zimefika bilioni zaidi ya 90, zingeweza kutumika kujenga Kiwanda cha Mbolea ambacho kinamilikiwa na wananchi wenyewe. Kwa kufanya hivyo tutakuwa na uhakika wa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetaka kuipongeza Serikali kwa kutenga Shilingi bilioni 891 katika suala la elimu ambalo ni suala la msingi sana. Waratibu wa Elimu wanapewa nyenzo za kutosha kama pikipiki ili kuweza kusimamia masuala ya elimu katika ngazi ya Kata, kwa sababu wanakaa karibu zaidi na Shule zetu za Msingi na Shule za Sekondari.

Shule za Msingi walimu wengi hawafundishi sawasawa, wanatumia muda mrefu kwenda kutafuta mishahara. Siku moja au mbili hutumiwa kwenda kutafuta mishahara.

Katika hilo ningeomba na ningeshauri kama ikiwezekana mishahara sasa ingeweza kulipwa kwenye ngazi ya Kata kwa kupitia kwa Waratibu hao. Mratibu angeweza kwenda kukusanya mishahara kwa siku moja kuliko kuwachukua Walimu wote wa Shule za Msingi, wa Shule za Sekondari wawe wanakwenda Mjini kutafuta mishahara. Ukichukua muda unaopotea, ni muda mrefu sana kwa ajili ya kuweza kufanya kazi hiyo. Nina uhakika kwa kufanya namna hiyo, Walimu wengi wanaweza kupata mishahara yao mapema zaidi. *(Makofi)*

Ningependa kumpongeza Waziri wa Elimu kwa mafunzo maalum ya vijana 3,500 ambao watapata mafunzo safari hii. Lakini ningetaka kusema, washiriki katika kuongeza elimu ya hao Walimu wakibaki hapa hapa natumaini hawatakuwa wazuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ningeomba kumalizia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda wetu, sasa umefikia wakati wa kuahirisha Bunge. Ninaomba nichukue nafasi hii niahirishe Kikao chetu cha Bunge cha leo na tutaonana tena kesho siku ya Jumatano saa 3:00 asubuhi.

*(Saa 01:39 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano Tarehe 21 Juni, 2006 saa 03:00 asubuhi)*